

Walioitwa...
Wateule
Mungu Amekuwa na Watu wake Daima
Ken McFarland

# Walioitwa…
# Wateule

*Mungu Amekuwa na Watu Wake Daima*

Ken McFarland

Mchoro kwenye Jalada “Yesu wa Njia Nyembamba” na
Elfred Lee
Ubunifu wa mpangilio wa kurasa na Ken McFarland

Nakala Hati miliki ya Makumbusho ya Ellen G. White
Haki zote zimehifadhiwa. Imetumika kwa ruhusa

Hatimiliki © 2009 ya
Alice Scarbrough

Imechapishwa nchini Marekani
Na
Review & Herald Graphics

Mhariri: Mch. Stephen Ogola Akeyo

Nukuu zilizo tumika katika kitabu hiki zinapatikana kwenye
Biblia ya kiswahili tafsiri ya kiunguja kama ilivyo tafsiriwa
na United Bible Society ya mwaka © 1952

ISBN 978-0-9799648-4-8

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Dibaji | 4 |
| Neno la Awali kwa Msomaji | 9 |
| Utangulizi | 11 |
| Hapo Zamani za Kale | 15 |
| Kuchagua Upande Katika Vita ya Vita Zote | 27 |
| Mfululizo Wa Waaminifu Usiokatika | 39 |
| Kuwarejesha Waasi kwa Njia ya Upendo | 50 |
| Kukosea Katika Kumtazamia Mfalme | 62 |
| Mlipuko wa Moto | 70 |
| Leta Mvua | 80 |
| Mwanamke wa Nyikani | 96 |
| Huu Ndio Msimamo Wangu | 112 |
| Kutoka Kwenye Majivu Kwenda Kwenye Ushindi | 124 |
| Mashujaa wa Ukweli | 138 |
| Zawadi Isiyofanana na Zawadi Yo Yote | 151 |
| Sisi ni Nani? | 165 |
| Wewe ni Nani? | 184 |

# Dibaji

Daima ni vizuri kuwa na mtazamo mpana. Mara nyingi tumebanwa katika ulimwengu wetu wa mawazo finyu kwa sababu ya changamoto na ugumu unaotuzunguka na kutufunga. Tunaanza kuangalia zaidi kamba za viatu na vitu vidogo vinavyotuzunguka baadala ya kutazama juu zaidi kuliko upeo tunaoweza kuona. Kwa mujibu wa maandiko matakatifu, tunapaswa kuwa na mtazamo mkubwa, wakati huo huo tukishughulikia mambo madogo yanayotuzunguka. Katika kitabu cha Luka 16:10; Yesu anasema: "Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia." Katika Luka 21:28 pia anasema; changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia. Kuwa mnyenyekevu na mwaminifu katika mambo madogo maishani ni muhimu kama ilivyo muhimu kuwa na mtazamo mpana.

Kitabu hiki cha pekee – Walioitwa… Wateule: Mungu amekuwa na watu wake daima – kitasisimua moyo wako unapofuatilia mkono wa Mungu usiokoma kuwalinda na kuwaongoza waaminifu katika historia yote. Kitakuonesha wazi dhana ya pambano kuu. Kama Mwadventista – Msabato, utafuatilia mizizi yako kutoka kwenye mwanzo wa Historia na kuona jukumu la namna ya pekee Mungu alilonalo kwa kuliteua kanisa lako, na kazi ambayo kanisa linapaswa kufanya katika nyakati hizi za mwisho wa historia ya dunia. Ni hakika Yesu anarudi mapema na mstari

mrefu wa wafuasi waaminifu wa Mungu umefikia kilele mbinguni kwa kuanza mwendo wa majaribio ya kanisa la Waadventista Wasabato. Kutokana na ishara za Biblia pamoja na Roho ya Unabii tunajua kwamba hili ni kanisa la masalio la watu wa Mungu – kanisa lake la masalio ambalo linapaswa kutangaza ujumbe wa malaika watatu kwa nguvu za Roho Mtakatifu, kuwaeleza watu kuhusu Kristo na wokovu wake, maungamo na haki ya Kristo, ibada ya kweli ya Mungu na habari za kurudi kwa Kristo mapema. Tafakari maneno haya yenye nguvu kutoka kwenye Roho ya Unabii:

> "Nimeagizwa kuwaambia Waadventista Wasabato duniani kote, Mungu ametuita kama watu kuwa hazina yake pekee. Ameteua kanisa lake duniani kuunganika kikamilifu na Roho Mtakatifu pamoja na Bwana wa majeshi hadi wakati wa Mwisho" – 2SM 397.

Kama umewahi kuwa na mashaka juu ya ujumbe na madhumuni ya kanisa la Waadventista Wasabato ambalo ndilo kanisa lako, usiwe na mashaka tena. Tumeingia kwenye kipindi cha wakati ambao hauwezi kulinganishwa na wakati wo wote wa historia duniani – wakati ambao Bwana atawatumia walio wake kwa njia ya nguvu ya pekee kuutangaza ujumbe wa Ufunuo 14 na kuwaandaa watu, kwa rehema za Kristo, kwa ajili ya kuja kwake mapema. Kanisa lako limeitwa kufanyakazi hiyo. Umeitwa na Mungu kufanya hivyo hivyo. Kitabu hiki cha Walioitwa…Wateule, kimeandikwa na Ken McFarland, kutoka kwenye njozi ya

mtazamo mkuu wa Hollis Scarbrough ambayo inathibitisha na kauli ifuatayo:

> "Waadventista Wasabato wameteuliwa na Bwana kama watu pekee, waliojitenga na ulimwengu. Kwa upanga mkuu wa ukweli amewakata kutoka kwenye mawindo ya ulimwengu na kuwaunganisha pamoja naye. Amewafanya kuwa wawakilishi wake na amewaita wawe mabalozi wake katika kazi ya mwisho ya wokovu. Utajiri mkuu zaidi wa ukweli ambao haujawahi kukabidhiwa kwa mwanadamu mwenye asili ya kufa, maonyo ya dhati kuu na yakutisha ambayo hayajatolewa kwao kwa ajili ya kuuonya ulimwengu" – 7T 138.

Je, unaweza kufikiria wajibu ambao Mungu ametupa mimi na wewe katika kipindi hiki cha maana cha siku za mwisho za pambano kuu kati ya Kristo na Shetani? Hii ndiyo maana tunahitaji kutumia muda kwa uangalifu katika kujifunza Biblia na Roho ya Unabii, katika kuomba kwa ajili ya uwezo wa Roho Mtakatifu na kushuhudia ujumbe huu wa pekee na kuutangazia ulimwengu wote rehema za Mungu. Kamwe usiwe na mashaka juu ya imani yako na urithi wa ukweli tuliopewa na Mungu. Kitabu hiki kitadhihirisha ushawishi wako kwamba Waadventista Wasabato wana agizo la kiroho lililovuviwa kuushuhudia ulimwengu. Tafakari changamoto moto hii kuu:

> "Kwa namna ya pekee Waadventista Wasabato wametengwa katika ulimwengu kuwa walinzi na

> wabeba nuru.. kwao wamekabidhiwa onyo la mwisho kwa ulimwengu unaoangamia. Kwao ni nuru ya pekee ya Neno la Mungu. Wamekabidhiwa kazi ya taadhima kuu –kuhubiri ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na watatu. Hakuna kazi nyingine ya maana kama hii. Hawahitajiki kuruhusu kitu cho chote zaidi kishaharabu usikivu wao" – 9T 19.

Kwa kadri unavyosoma kitabu hiki na kuona jinsi Mungu alivyoongoza watu wake katika historia hadi wakati huu, utaona kwamba Bwana alijua kwamba, kanisa lake la masalio la wakati wa mwisho litahitaji mwongozo pekee kutoka mbinguni. Alitoa Roho ya Unabii ambayo inatuelekeza kwenye Biblia. Alitoa hii kwa ajili ya kanisa la Waadventista Wasabato, kwa sababu kanisa hili ni chombo teule kutoka mbinguni kwa ajili ya kutangaza ujumbe wa onyo la mwisho kwa ulimwengu na kuwaelekeza watu kwa Kristo, juu ya kurudi kwake na ibada ya kweli ya Mungu, ambayo itadumu milele zote. Mungu ameonyesha katika Ufunuo 12:17 kwamba kanisa lake la siku za mwisho litakuwa na tabia mbili za pekee: litatunza amri za Mungu, ikiwa na pamoja na siku ya Sabato; amri ya nne, na watakuwa na ushuhuda wa Yesu, ambayo ni Roho ya Unabii. Wewe ni sehemu ya maendeleo/mwendo huo, na kwa kadri unavyosoma kitabu hiki unakumbushwa katika kila mwisho wa sura kwa maneno haya yaliyovuviwa:

> "Katika kila kizazi, Mungu amekuwa na watu wake – waaminifu, wanyenyekevu, walioitwa na walioteuliwa – na

bado ana watu pekee leo."

Inasisimua kiasi gani kuwa sehemu ya watu wa Mungu, ambao wana upendeleo wa pekee na furaha ya kushuhudia upendo wa Mungu na kurudi kwa Kristo mapema kwa ulimwengu wote. Kama Ken McFarland anavyosema katika kitabu hiki cha kuvutia: "Wewe ni mmoja wapo wa wajumbe wa masalio wanaojua namna ya kutoka katika sayari hii mkiwa hai na mna ujumbe na upendeleo wa kushuhudia kwa watu wengine. Ni mmoja wa wateule wa mwisho wa Mungu." Ubarikiwe, ufarijike, utiwe nguvu, na ujazwe na Roho Mtakatifu kwa ajili ya ujumbe wa kitabu hiki unaposoma jinsi Mungu alivyowaongoza watu wake katika siku zilizopita na atakavyotuongoza katika wakati ujao hadi katika maisha ya umilele – yote katika jina lenye nguvu la Yesu Kristo. Ni baraka kiasi gani kuwa sehemu ya kanisa hili.

Ted N. C. Wilson
Makamu Mwenyekiti
Makao Makuu ya Kanisa la Waadventista Wasabato
Ulimwenguni.

## Neno la Awali kwa Msomaji

# Kisa Kikuu Kisicho Na Kifani

Kitabu hiki ni jina la kisa.

Ni kisa cha pambano la muda mrefu baina ya wema na uovu lilianza miaka maelfu iliyopita na bado haijaisha. Kisa cha wanyenyekevu wachache waliosimama thabiti upande wa wema katika kila karne. Na hasa kisa cha waliosimama imara mwishoni kwenye zamu zao wakisaidia kumaliza vita kuu.

Hiki ni kisa cha *walioitwa – walioteuliwa*. Kisa cha wale ambao Mungu amewaita kutoka kwenye uovu na uasi na kuingia kwenye ukweli na unyenyekevu. Kisa cha wale ambao Mungu amewaita ili kuuambia ulimwengu ukweli wake na kuuonyesha ulimwengu jinsi Mungu alivyo hasa.

Fahamu kwamba kitabu hiki sio historia pana na kamilifu. Kila sura katika kitabu imegusia kidogo sana juu ya sehemu za historia iliyoelezwa kwa ndani zaidi kupitia katika vitabu vingine vingi vilivyobora.

Badala yake, kusudi letu hapa ni kutoa muhtasari - kuangalia kwa haraka matukio ya nyakati na kuona jinsi

wafuasi waaminifu wa Mungu, waliopo sasa, walivyo kiungo cha mwisho katika mfululizo wa waaminifu wake usiokatika tangu wakati wa Adamu. Kitabu hiki pia hakihusishi tanbihi (vitabu vya rejea) wala sio maandishi ya kiakademia ya kisomi. Badala yake, kitabu hiki kinahusu utu, kuhusu watu, na kulenga zaidi juu ya uhusiano kati ya Mungu na wafuasi wake.

Kitabu hiki ni ufupisho zaidi kisa kile kile kizuri kilichoelezwa na Ellen White katika mfululizo wa vitabu vyake juu ya pambano. Bali yanayolinganishwa mwendelezo wa kisa kilichoandikwa humo, pamoja na safari ya watu wa Mungu katika miongo iliyopita tangu mfululizo ulipoandikwa.

Lusifa na Mikaeli, Adamu na Hawa, Noa, Musa, Petro na Paulo, Wawaldensia, Martin Luther, James na Ellen White na wengineo; hawa wote utawakuta katika kitabu hiki ikiwa ni pamoja na wewe mwenyewe.

UTANGULIZI

# Ukweli Dhidi Ya Bandia

Wewe ni Mwadventista Msabato.

Kwa vyo vyote vile uwe umekulia kanisani au umeingia kwa ubatizo ukiwa mtu mzima umeshafundishwa kwamba kanisa la Waadventista ni kanisa teule la masalio, ni chombo ambacho Mungu mwenyewe amekiinua juu kwa ajili ya kuwaita wafuasi wake wa kweli watoke nje ya Babeli iliyochanganyikiwa, ya makanisa mengine.

Je, unauhakika wa jambo hili?

Una uhakika kabisa?

Hata hivyo seti ya vitabu vinavyotoa taarifa kuhusu Ukristo ulimwenguni (the *World Christian Encyclopedia*) inaonyesha dini tofauti tofauti 10,000 ulimwenguni. Kati ya hizo mojawapo ni Ukristo ambao una madhehebu tofauti 33,830 ulimwenguni kote.

Kila moja ya madhehebu hayo zaidi ya 33,000 wanaamini kuwa ni moja ya kanisa la kweli la Mungu duniani. Chunguza neno kanisa la kweli kwenye mtandao mkuu wa kimataifa wa kikompyuta (Google) na utapata zaidi ya mapendekezo nusu ya milioni juu ya hilo.

Uliza Mormon, Mashahidi ya Yehova, Kanisa Katoliki

la Kiroma – kila mmoja wa washiriki hao, atakuhakikishia haraka haraka kwamba kanisa lao ndilo kanisa la kweli pekee duniani. Hivyo ndivyo washiriki kutoka katika kila madhehebu watakuhakikishia. Washiriki wa imani ya kiyahudi watafanya hivyo pia. Waislamu, Wabudha, na Waanglikana pia watakuthibitishia hivyo hivyo pia.

Lakini, inawezekana kila mmoja anasema sawa?

Na kama kweli Mungu ana kanisa la kweli duniani, anaweza kuwa na uhakika kuwa kanisa lako la Waadventista Wasabato ndilo la kweli?

Labda umeshajibu swali hili wewe mwenyewe na huna mashaka yo yote juu ya hilo. Kama ndivyo, kisa ambacho karibu kitasimuliwa katika kurasa hizi, bila shaka kitakuimarisha katika uhakika ulio nao. Vilevile kisa hiki kitafungua kwa uwazi zaidi juu ya jukumu lako binafsi ulilоitiwa na Mungu kushiriki katika pambano kuu dhidi ya wema na ubaya; na dhidi ya ukweli na uongo.

Labda, hata kama bado unapambana, angalau mara kadhaa juu ya swali hili kama kanisa lako la Waadventista Wasabato ndiyo nyumba hasa ya Mungu ya ujumbe wa siku za mwisho na wafuasi wateule. Unashangaa wakati mwingine kama dai hilo sio ujeuri tu, ubaguzi na hata majigambo. Unakumbuka jinsi Waisraeli wa Agano la Kale pamoja na kuwa wateule wa Mungu na hazina ya Ukweli wa Mungu, pamoja na kuwa walijiingiza katika matendo yao ya kikafiri na kipagani, bado walijiona nakujidhania kuwa bora kiroho kuliko mataifa yote.

Kama bado hujapata jibu sahihi la swali la jukumu

la kanisa lako, kisa utakachosimuliwa katika kurasa hizi kitakupa habari za uhakika zaidi ambazo zitakusaidia katika kugundua jibu lako mwenyewe.

Katikati ya miaka ya 1950 katika nchi ya Marekani kulikuwa na mchezo wa TV uliojulikana kama "Kusema Ukweli." Katika njia mbalimbali, ulirushwa hewani kwa kurudiwa rudiwa. Kipindi kirefu kilipita ambapo mchezo huu ulisitishwa hadi mwaka 2002 ulipo rushwa tena hewani.

Pengine yawezekana kuwa uliwahi kuangalia mchezo huu ulionyesha wagombeaji watatu ambao kila mmoja alidai kuwa ni mgombeaji yule yule – lakini wawili kati yao walikuwa matapeli. Jopo la waamuzi lingewauliza washindanaji swali na kupiga kura kwa ajili ya mmoja waliyedhani alikuwa mtu halisi.

Baada ya kura, mwendeshaji wa mchezo aliuliza, "Je, mgombeaji halisi (na hapo jina lake lilioneshwa) anaweza kusimama? Tafadhali?

Leo, tunaweza kuulizwa pia, "Je, kanisa halisi la kweli linaweza kusimama, tafadhali?"

Je, kupata jibu la swali hilo, tunahitaji kufanya utafiti wa imani zote za duniani 10,000 za dini, pamoja na zaidi ya makundi 33,000 ya Kikristo? La, hasha! Hatuhitaji kufanya hivyo. Nani ana muda wa namna hiyo? Na njia hiyo italeta kuchanganyikiwa hasa.

Hapa kuna pendekezo. Badala ya kuchunguza kila dini mojamoja duniani ilikugundua ipi inafundisha ukweli, hebu twende tu kwa Biblia na kugundua ndani yake alama ambazo inatupa ili tutambue kanisa la kweli la Mungu.

Katika mtandao wa mawasiliano ya kimataifa ya kompyuta (United States Secret Service Internet Website) unaweza kupata sehemu inayoitwa "Namna ya kugundua fedha za bandia. Inasema hivi: Angalia pesa unazopata. Linganisha noti ya fedha halali…. Chunguza utofauti, sio mambo yanayofanana."

Bila shaka, ili ufuate ushauri huu, ni lazima uwe na noti ya fedha halali ambayo utakuwa ukilinganisha na noti nyingine za fedha. Unapaswa kujua kitu halisi kinaganaga. Wakala mzuri wa huduma za siri katika kitengo cha bandia hutumia muda mwingi sana katika kujifunza na kujua nakala halisi na sio katika kuangalia nakala bandia. Anapofanikiwa kufahamu nakala halisi ilivyo, kutambua ile iliyo bandia huwa kazi rahisi kwake.

Katika kurasa za mbele, tutagundua jinsi Biblia inavyosema ukweli dhidi ya bandia, kuhusu ukweli dhidi ya uongo.

Kila kisa kina mwanzo. Je, unasemaje tuanzie pale?

SURA YA 1

# Hapo Zamani Za Kale

Ukisha sikia hapo zamani za kale, unajua kwamba kisa kinafuata.

Wakati filamu ya kwanza ya vita vya nyota (Star Wars) ilipoanza mwaka 1977, ilianza hivi, “Hapo zamani za kale… katika kundi la nyota la mbali, mbali sana” – watazamaji walijua kwamba kisa kinakuja.

Halafu kulikuwa na kisa; wakati fulani baba aliniambia hivi.

Wakati huo huo ambapo filamu ya vita vya nyota ilipoanza, “Mizizi” (Roots) – mfululizo mfupi; uliotungwa na Alex Haley juu ya mababu zake wa Africa ilianza pia. Kwa muda wa wiki kadhaa, kikundi kikubwa cha watu waliokuwa wakiangalia mchezo wa utekaji nyara.

Ghafla, somo la kujifunza asili ya mtu (One’s roots) liliwafanya Wamarekani wengi sana waanze kufanya uchunguzi juu ya nasaba zao, miongoni mwao ni wazazi wangu.

Wakati mwafaka, Baba alihitaji kunieleza aliyojifunza kwa undani zaidi. Hivyo siku za Jumamosi na Jumapili mchana niliendesha gari hadi nyumbani kwake na kukaa chini na kumsikiliza. Nilipokuwa nimeketi vizuri kwenye

kiti, nilijiandaa kusikia akisema kwamba mababu zetu waliishi Scotland. Lakini hakusema hivyo.

Nuhu alikuwa na watoto wa watatu, alianza.

Nilijua kwamba kisa kilikuwa kinakuja. Na nilijua kuwa utakuwa mchana mrefu sana.

Sasa usikubali nikusikitishe, kwa vile hiki siyo kitabu kikubwa. Lakini nina kisa cha kukuambia. Na kisa ninachohitaji kukusimulia kimeanza zamani zaidi kabla ya Nuhu. Kusema kweli, kimeanza zamani sana sawa na vita vya nyota, muda mrefu uliyopita sehemu ya mbali, mbali sana. Mahali panapoitwa mbinguni.

Kisa ninachotaka kukuadithia katika kurasa hizi ni, kwa kutumia kichwa cha kitabu cha Fulton Oursler cha mwaka 1949 juu ya maisha ya Yesu, "kisa kikuu ambacho hakijawahi kusimuliwa ni:"

Kisa cha ukweli dhidi ya Uongo.

Ni kisa cha Upendo dhidi ya Ubinafsi.

Ni kisa cha Nuru dhidi ya Giza.

Ni kisa cha Wema dhidi ya Uovu.

Ni kisa cha Mikaeli (Yesu) dhidi ya Lusifa (Shetani).

Ni kisa cha wafuasi wa Kristo dhidi ya wafuasi wa mwovu.

Wazo kuu la kitabu hiki litakuwa juu ya hao wafuasi wa kweli wa Kristo, kufuatia historia yao ya hapa duniani tangu kabla ya anguko la mwanadamu hadi atakaporejeshwa katika ulimwengu mkamilifu.

Daima, Mungu amekuwa na wafuasi waaminifu, walio waaminifu katika ukweli wake na wamejitoa kikamilifu

kufuata mapenzi yake.

Siku zote, Mungu amekuwa ana wafuasi wake waaminifu wanaotangaza ukweli wake kwa ujasiri.

Siku zote, Mungu amekuwa ana watu wake hapa duniani wachache walio waaminifu, walioitwa na wateule, watetezi na watangazaji wa ukweli wake.

Na Mungu bado ana watu. Tutawaangalia zaidi katika sura zinazofuata.

Kwa sasa hebu tuanze katika mwanzo.

Fuatana nami sasa, jitahidi kutafakari – wakati ambapo hapakuwa na dhambi duniani; hapakuwa na shida wala uasi. Sura za kwanza za Biblia zinatupeleka nyuma katika kipindi hicho cha zamani, zamani za kale, huko mbali, mbali mno. Mahali tunapoita mbinguni.

Hapa mbinguni kipo kiti cha enzi cha Mungu. Kutoka katika kiti hiki cha enzi anaungalia ulimwengu wote aliouumba. Malaika wasio na idadi, wanaometameta, wenye akili sana, viumbe wasio na dhambi ambao pia waliumbwa – wakiimba kwa furaha na upendo mbele za Mungu. Lakini Mungu alipowaumba malaika hawa alichagua kujihatarisha. Unaona, alitaka viumbe wake wampende kwa sababu wanahitaji kufanya hivyo kwa sababu wamechagua kufanya hivyo na si kwa sababu ya kulazimishwa.

Hivyo alimwumba kila malaika na kipaji cha pekee cha utashi. Hakuwaumba katika utaratibu wa kikompyuta kwamba ni lazima wampende. Walikuwa huru kuchagua kumpenda na kumtii mwumbaji wao. Lakini uhuru huo wa kuchagua ulikuwa na maana pia kwamba walikuwa huru

kuhitilafiana naye. Hivyo ndivyo Mungu alivyojihatarisha.

Kwa kuonyesha utaratibu wake mkamilifu wa upendo, kila malaika alipewa kazi pekee. Na malaika mkuu kuliko wote aliitwa Lusifa "anayeng'aa". Lusifa aliitwa ni kerubi wa kufunika aliyesimama karibu sana na Mungu. "Ulipakwa mafuta kama kerubi mwangalizi; Mungu alisema hivi juu ya Lusifa katika kitabu cha Ezekieli 28:14.

"Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye nami nilikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, ulitembea huko na huko kati ya mawe ya moto." Fungu la 12. "Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri."

Katika ukamilifu wa amani bila dhambi miaka ya umilele iliendelea. Lusifa alikaa mbinguni kwa muda gani baada ya kuumbwa? Biblia haitwambii lolote juu ya hilo labda maelfu ya miaka. Pengine mamilioni ya miaka.

Lakini kadri muda ulivyoendelea, Lusifa alianza kujisikia zaidi juu ya uzuri na hekima yake. Na sasa alijisikia kwamba angepandishwa juu kufikia kimo cha mbinguni katika madaraka.

Kulikuwa na wengine wawili tu huko mbinguni ambao walikuwa sawa na Mungu baba, Yesu Kristo – Mungu Mwana, na Roho Mtakatifu. Lusifa kwa kujua kwamba Mungu ni wa haki na mkweli, bila wasiwasi wo wote alifikia uamuzi kwamba mapema Mungu atatambua kukua kwake, sifa zake, mambo aliyokamilisha na kumpandisha cheo ili awe sawa na Mungu Mwana na Roho Mtakatifu.

### *Kiburi – Halafu Anguko*

Ezekieli 28:17 "Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; Umeiharibu hekima yako." Kwa maneno mengine Lusifa alikuwa afikiri sawa. Uamuzi wake uliharibiwa kwa sababu ya mtazamo mpotovu juu yake yeye mwenyewe alioutengeneza na kuchagua kuuamini. Kwa sababu ya hekima, nafasi (cheo) na uzuri wake. Taratibu taratibu Lusifa alianza kujiona yeye mwenyewe kama ni muhimu zaidi katika mpango wa vitu vya mbinguni kuliko jinsi alivyokuwa hasa. Alianza kujivuna. Alijiona kuwa yeye ndiyo yeye.

Kiburi – hisia ya kukuza umuhimu wako binafsi, inamweka mtu juu kwa ajili ya anguko. Na kweli, Lusifa alianguka; baada ya anguko lake Mungu angemwelezea katika Ezekieli 28:15 "Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipo oenekana ndani ya moyo wako."

Na katika cha Isaya 14:12-14, Mungu aliongeza maneno haya:

> "Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu, Nami nitaketi kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini, Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu."

Kujipandisha cheo kwa Lusifa hakukufaulu. Kama angekuwa anafikiri sawa, asingepoteza mtazamo wa kweli juu ya Mungu kwamba alikuwa Mwumbaji, na Lusifa alikuwa kiumbe tu. Hivyo aliendelea kusubiri huku mashaka yakiongezeka ya kutumainia jambo ambalo lisingetokea kamwe.

Kwa kadri muda ulivyoendelea kupita bila Mungu kuonyesha kwamba alikuwa anajiandaa kwa ajili ya kupandishwa Lusifa mapema, mkuu wa malaika alistaajabu kwanza, baadaye alikatishwa tamaa na mwishoni alijawa na hasira pamoja na wivu.

Kwa wakati huu, Lusifa angefanya uamuzi wa jambo moja tu kati ya mambo mawili. Pengine tatizo lilikuwa upande wa Mungu au lilikuwa kwa Lusifa. Kwa Lusifa aliamini tatizo halikuwa upande wake, basi alishawishika kwamba tatizo lilikuwa la Mungu.

Pamoja na ushahidi wa wazi kuwa kinyume naye, Lusifa alifikia uamuzi kwamba Mungu hupendelea, hatendi haki na wala sio mkweli. Ilionekana wazi kwa Lusifa kwamba kumpa Yesu heshima za pekee, fadhila na mamlaka; Mungu Baba alikuwa anafanya upendeleo. Mungu sio kama anavyojitambulisha mwenyewe kwa ulimwengu. Hivyo kerubi mwangalizi aliamini kabisa mawazo yake ya uongo juu ya tabia ya Mungu yana kubalika kama kweli.

Kwa muda mrefu, alifanya kazi ya kushawishi malaika kwamba mtazamo walionao juu ya Mungu si sahihi, kwamba kwa hakika Mungu kiasi fulani hakuwa mwenye haki na kiasi fulani muongo. Hatimaye kutoridhika kwake

kukapanda kwa kiwango cha juu sana na kugeuka uasi. Biblia inaeleza katika Ufunuo 12:7-9

> "Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake, nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, yule mkubwa, yule nyoka wa zamani, aitwae Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye."

Ufunuo 12:3,4 anasema kwamba theluthi nzima ya malaika walikubali na kuamini uongo wake.

Vita kuu dhidi ya Kristo na Lusifa – ambaye kwa sasa anaitwa mwovu au Shetani ilianza. Vita ambavyo ni msingi wa vita vyote – vita ambavyo vinahusisha kila vita na ni sababu ya kila vita iliyowahi kupiganwa duniani vilianza kusukasuka.

Lakini ni jinsi gani ambavyo mimi na wewe tunavyohusika katika vita hii kuu baina ya Mungu na serikali yake ya upendo – na Shetani pamoja na jeshi lake la uasi la ubinafsi? Jinsi gani hili pambano kuu lilitoka kwa malaika hadi kwa binadamu?

Kama vile mpangaji mwovu aondolewavyo na mwenye nyumba, ndivyo Shetani na malaika zake walivyo fukuzwa kutoka mbinguni. Shetani na waasi wake waliweka makao yao makuu ya serikali yao mpya ya upinzani katika katika sayari ndogo iitwayo dunia na wakajifunga wenyewe kwa

kiapo cha chuki ya milele na hatimaye kumuua Mwumbaji wao.

Kitabu cha kwanza cha Biblia – Mwanzo – kinatuambia katika dunia hii, Mungu aliamua kuumba viumbe vya aina nyingine, sio wenye nguvu kama malaika lakini waliumbwa kwa mfano wake. Katika siku ya sita ya uumbaji kutokana na Mwanzo 1:26,27, Mungu alisema: Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu... Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba.

Mungu aliwaumba wanadamu wa kwanza – Adamu na Hawa wakiwa na uhuru wa utashi kama ule ule aliowapa malaika. Pia aliumba bustani nzuri iitwayo Edeni kama nyumba ya wazazi wetu wa kwanza. Mungu hakumruhusu Shetani aliyeanguka kuwa na uhuru kwa mwanaume na mwanamke aliowaumba. Badala yake Mungu alimzuia kutoka kwa mti mmoja tu wa katikati ya bustani. Naye Mungu akamwonya Adamu na Hawa wakae mbali na mti huo, akawaamuru kuwa kamwe wasile tunda la mti huo.

### *Msiba*

Hatimaye siku ya huzuni ilifika ambayo ilibadili dunia na historia ya binadamu milele. Hebu niwasimulie kisa hicho.

Kamwe Hawa asingekusudia kutanga mbali na mumewe Adamu; lakini kwa namna fulani kwa furaha akiwa ametingwa na kazi zake, ghafla alijikuta yuko mwenyewe, akiutazama mti ambao mwanzoni kabisa

Mungu alishawapa maonyo juu yake.

Maonyo yake yalikuja kwenye fikira zake:

"Unaweza kula tunda kutoka kwenye mti wo wote kutoka kwenye bustani ya Edeni, lakini usile tunda kutoka kwenye mti uliopo katikati ya bustani. Kama ukila, hakika utakufa."

Akiwa bado yuko karibu na mti ule, Shetani kupitia katika mfano wa nyoka naye alikuwa akimsubiri amlaghai. Na kwa njia ya udanganyifu na ushawishi wa kumfanya hawa kutokuamini nia ya Mungu ya kuwaonya (Adamu an Hawa) kuwa mbali na mti; Shetani alimwingiza Hawa kwenye majaribu kuchukua tunda kutoka kwenye mti na kula. Kabla siku haijaisha, Hawa alikuwa anampatia Adamu tunda kutoka kwenye mti wa katikati ya bustani.

Baadaye siku hiyo hiyo, wakati Lusifa na jeshi lake wakisherekea kwa shangwe kuu kwa ajili ya ushindi mkuu, Adamu na Hawa walimsikia Mungu akiwaita katika bustani ya Edeni. Kwa kawaida alipoita kabla ya tukio hilo, walikuwa wanakwenda mbio kwa furaha kukutana naye. Lakini jioni hii, Biblia inasema katika Mwanzo 3:8, kwamba walijificha kwenye miti ya bustanini Bwana Mungu asiwaone.

Mko wapi? Mungu aliwaita.

"Nimesikia sauti yako," Hatimaye Adamu alijibu, "na nikaogopa."

Adamu – kumwogopa Mungu?

Wengi wetu tunaoishi leo tuna njia ya kumrudia pia, ikiwa tunasikia haja ya kumrudia tena. Tangu siku ile

katika bustani ya Edeni, sisi kama viumbe wake mara nyingi hatuna wepesi wa kuwa pamoja na Mungu – hata tunamwogopa. Kwa namna fulani dhambi inafanana hivyo. Dhambi inavunja uhusiano kati yetu na mwumbaji wetu ambayo inasababisha tusimwone Mungu kama alivyo hasa, bali katika mtazamo mpotovu hasa.

Sijui picha halisi uliyonayo sasa kuhusu Mungu. Bali ninajua kwamba ikiwa unaogopa kidogo kuwa naye, una hasira dhidi yake, huna wepesi wa kuwa karibu naye, ni kwa sababu ya mtengano wa dhambi unakuzuia usimwone Mungu alivyo halisi.

Mara nyingi tunapotengwa mbali na Mungu, tunaanza kutafakari mambo mengi juu yake ambayo siyo kweli. Tunaanza kumlaumu kwa ajili ya maumivu yaliyoletwa na dhambi zetu sisi wenyewe. Tunaanza kumwona kama yuko kinyume chetu hasa – hakimu wetu mkali au baba mwenye hasira, na adui yetu mkuu.

Na kwa kuwa na mtazamo huu potovu juu ya Mungu, tuna msada mwingi. Shetani, Lusifa aliyeanguka, yuko kazini daima kumpaka Mungu matope, kuchafua sifa zake na kuchora picha kumwonyesha Mungu kama mwovu mkuu. Shetani ameharibiwa kwa lengo la kumfanya Mungu aonekane mbaya na kutuambia uongo juu yake. Hivyo matatizo yanapo vamia maisha yetu, misiba, maumivu, na maombolezo yanapotupata, mara moja tunapeleka lawama kwa Mungu.

Ushahidi wa upendo mkuu wa Mungu kwa ajili ya mwanadamu umerekodiwa katika mafungu machache

tu baada ya kisa cha huzuni cha Adamu na Hawa cha kuangukia dhambini. Katika Mwanzo 3:15 Mungu anazungumza na Shetani, na kumwambia kwamba “Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.

Haya ni maneno ya awali ya ahadi ya Biblia kwamba Mungu kwa namna fulani atawaokoa wanadamu aliowaumba. Atatayarisha njia ili mtu fulani abebe adhabu ya dhambi yao.

Mungu aliweka uadui kati ya Shetani na Hawa, na kati ya uzao au wafuasi wa Shetani na uzao wa Hawa. Na mmoja katika uzao wa Hawa, atainuka na kumponda Shetani kichwa wakati Shetani atamponda kisigino tu. Hapa inamaanisha kwamba, kutakuwa na jeraha la mauti kinyume cha jeraha la kuumia kisigino.

Uzao ambao ungemgonga Shetani kichwa ni Yesu, mwana wa Mungu. Siku ilikuja ambapo ahadi aliyoahidi Mwokozi kwamba atachukua dhambi zote zilizotendwa na mtu ye yote tangu ulimwengu ulipoumbwa. Alichukua yeye mwenyewe uasi wote, ubinafsi na kiburi cha wanadamu waliogeuka nyuma na kumwacha Mungu. Juu ya msalaba wa aibu alibeba adhabu nzima ya kifo. Alitoa damu yake na maisha kumwokoa Adamu na Hawa.

Kuokoa uzao wao.

Kukuokoa wewe.

Kuniokoa mimi.

Vita dhidi ya Mungu ilianzishwa mbinguni na malaika

aliyejawa na kiburi huko mbinguni. Vita hii ilihamia duniani, ambako wanadamu pia waliasi na kufuata njia zao wenyewe. Habari njema ni kwamba siku moja ya karibuni, vita itaisha kabisa milele na milele.

Lakini katikati ya mwanzo wa vita kuu na mwisho wake, Mungu amekuwa ana watu - hata sasa anao - na ataendelea kuwa nao - walio amua kusimama upande wake wa vita, ambao ni waaminifu hata kufa, kwa ajili ya ukweli wa Mungu na kutetea tabia yake.

Kisa cha vita hii kuu ni kisa cha hao wafuasi waaminifu.

Nani waliokuwa wa kwanza katika waaminifu?

Ni akina nani ambao wamekuwepo katika historia?

Ni akina nani leo?

Majibu kwa maswali hayo matatu hayajafungwa kwa siri.

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 2

# Kuchagua Upande Katika Vita Ya Vita Zote

Hebu tuseme kwamba wewe ni mwandishi. Umetumia muda mwingi kama miezi au miaka kadhaa kwa ajili ya kuandika kitabu. Ukitumaini kwamba umetengeneza kitabu ambacho kimekuwa namba moja katika soko la uuzaji vitabu na umepeleka kwa shirika la uchapishaji wa vitabu.

Kinapofika kwenye meza ya mhariri, umepeleka kwa haraka haraka kutafuta kama umeweka neno "hicho."

Hicho?

Naam, una maelezo mazuri mazungumzo mazuri, wahusika wa kuvutia, maelezo mazuri na sifa zote za uuzaji. Bali si muda mrefu mhariri hajagundua kwamba haipo na unapewa stakabadhiya kazi yako kukataliwa. Uliacha nini?

*Ushindani.*

Kama kisa hakina mgongano, kimekufa kinapofika. Mgongano hupatikana katika mifumo mbalimbali. Watu wema dhidi ya watu wabaya. Nchi njema dhidi ya nchi yenye uovu. Visa dhidi ya maumbile ya asili (tufani ya upepo wa kimbunga, mnyama wa porini n.k). Hata kisa cha mtu anayepigana vita ya ndani ya moyo (tabia mbaya, jaribu la kufanya mambo yasiyo halali).

Mgongano ni kitu kimoja ambacho hakihitaji kabisa ulazima mapatano katika kisa. Kwa nini? Kuishi tu kwenye dunia hii ni mgongano. Ni msingi wa maisha halisi katika sayari ya dunia. Kwa hakika huwezi kuishi siku nzima bila kuupitia uzoefu wa kukabiliwa na hicho MGONGANO.

- Inawezekana kuwa ni watoto wadogo wawili wa shule wanashindana kwenye uwanja wa michezo.
- Labda ni mwanaume na mke wake wanabishana kwa maneno makali.
- Inawezekana ni wanamasumbwi wawili wa kulipwa ulingoni kila mmoja anataka kumpiga mwenzie ngumi sawa sawa.
- Inawezekana ni kelele za vichwa vya mazungumzo ya TV yakisababisha ubishi mkuu kati ya raia wa kawaida kuliko wanasiasa wenye uzoefu na mada husika.
- Ndivyo ilivyo kila wakati, unafahamu mapambano yanayoendelea sasa hivi ndani yako; mapigano dhidi ya upande wako mwema na upande wako usio mwema (mwovu).

Bali Mungu ni Mungu wa amani, sio wa mgongano. Aliuumba ulimwengu wenye amani kamili – yenye amani kamili baina ya watu. Hapo mwanzo hata wanyama wenyewe walikuwa na amani na wanyama wenzao. Na Biblia inaweka wazi kwamba wakati unakuja upesi, ambapo dunia hii tena itakuwa ni mahali penye amani kamili.

Mgongano ni uvamizi, ni mkengeuko, ni mabadiliko.

Mgongano ni tunda halisi la dhambi. Na dhambi kwa halisi ni ubinafsi. Dhambi haikuwepo hadi Lusifa alipoamua

kujitanguliza juu yeye mwenyewe badala ya mwumbaji wake.

"Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, ewe nyota wa asubuhi, mwana wa alfajiri!... Ulisema moyoni mwako

Nitapanda mpaka mbinguni;

Nitakiinua kiti changu kuliko nyota za Mungu;

Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano;

Nitafanana na yeye Aliye juu" Isaya 14:12-14, mkazo umewekwa.

Lusifa alikuza tatizo la umimi na kila wakati ubinafsi unapotangulia mgongano ndiyo matokeo yake. Maisha yote yanakuwa juu ya umimi. Ubinafsi unainuliwa, unatunzwa, unatetewa, unachungwa na matokeo yanaonekana mtu anapopigana ili kutunza nafasi yake. Na ukitishiwa ubinafsi unapigana.

Hivyo Biblia inasema kulikuwa na vita mbinguni Pambano kuu dhidi ya Lusifa na Mwumbaji lilikwisha anza. Na vita hii kuu ambayo imesha shabikiwa karibu na muda wa miaka 6,000 ni msingi wa vita vyote.

Tuseme umepelekwa kwenye nyumba ya sanaa ya tajiri mkuu ukiwa umefungwa kitambaa usoni usione na umepelekwa inchi moja au mbili kutoka kwenye kuta zake. Wana kuondolea kitambaa na unaulizwa kuelezea kile unachoona. Unajibu kwamba unaona rangi – rangi ya manjano kidogo na alama ya kahawia. Unapelekwa nyuma inchi chache. Sasa unaona mpangilio wa rangi. Hatimaye unarudishwa nyuma futi chache na sasa unaona kwamba unatazama chapa ndogo ya mchoro wa Leonardo da Vinci

mashuhuri wa Mona Lisa, ambao nakala yake ya awali imetundikwa katika nyumba ya makumbusho ya Lovie Paris, Ufaransa.

Inasaidia kuona picha kubwa.

Na pambano kuu baina ya Lusifa (sasa Shetani) na Yesu NI picha kubwa. Kila mgongano, kila vita, kila mapigano hapa duniani ni sehemu ndogo tu, sehemu ndogo sana – ya picha kuu. Ni mkwaruzano mdogo katika vita kuu ambayo ni chanzo cha vita vyote.

Mgongano unatokea wakati 'mimi' inapofanywa muhimu.

Kama 'mimi' niko sawa wewe hauko sawa.

Kama 'mimi' nikitishwa sita simamishwa na kitu cho chote kujilinda mwenyewe.

Kama 'mimi' nikitaka kitu, ninapaswa kukipata hata kama nikichukua kwa nguvu ikiwezekana.

Kabla dhambi (ubinafsi) kuingia ulimwenguni, mgongano haukuwepo. Wakati Mungu atakapo iondoa dhambi milele na kuiumba upya dunia yetu, mgongano hautatokea tena. Upo hapa kwa muda katika kipindi kifupi.

Kabla dhambi haijaja, hapakuwa na upande kama upande uliopo sasa na upande niliopo. Kabla ya dhambi viumbe vyote vilivyoumbwa na Mungu vilikuwa pamoja naye. Baada ya dhambi viumbe wengine walianza kuwa kinyume na Mungu. Hivyo miaka 6,000 au zaidi sasa, kumekuwa na pande mbili, upande wa Mungu na upande wa Shetani.

Angalia vizuri hakuna upande wa tatu. Ziko pande

mbili tu. Kila wakati na katika kila siku, kila mmoja wetu anaweza kuchagua upande mmoja tu kati ya hizo pande mbili.

Maisha – au mauti
Wema – au uovu
Nuru – au giza
Ukweli – au uongo
Kutumaini – au kuwa na mashaka
Upendo – au ubinafsi
Jambo la kujenga – au jambo la kubomoa
Kristo – au Shetani

Yupo mtu anapinga, katika vita hii dhidi ya viongozi wakuu wawili wenye kanuni tofauti kabisa, anasema mimi sichagui upande wo wote. Mimi ninajitegemea. Ni mnyenyekevu kwangu mwenyewe. Mwache Kristo na Shetani wapigane. Mimi sihusiki.

Hebu natuwe wazi bila kuchanganyikiwa. Kuna pande mbili tu. Na hakuna mtu ye yote ulimwenguni anayeweza kubaki katikati. Hakuna anayeweza kukaa pembeni mwa mistari. Kwa nini? Kwa sababu usipohusika kikamilifu katika kuchagua upande ulio sahihi kwa kupuuuza, utakuwa umejichagulia upande mbaya. Hii ndiyo kusema kwamba, kutochagua upande wa Kristo katika pambano hili mara moja unakupeleka upande wa Shetani. Unaona ukijaribu kuwa sehemu ya tatu, sehemu ya kujitegemea, hiyo nayo vilevile inaangukia upande wa kundi la Shetani.

Kisa cha pambano kuu dhidi ya Kristo na Shetani – ambacho ni kisa kikuu cha kitabu hiki – ni kisa cha pande

mbili katika pambano. Hivyo ni kisa cha namna watu, kutoka kwa wazazi wetu wa kwanza, Adamu na Hawa hadi kwako na mimi na kila mtu anayeishi sasa – chagua ni upande gani utasimama katika pambano hii.

Je, tupo upande wa Kristo – au wa Shetani?

Je, tuwaaminifu kwa ukweli – au kwa uongo?

Je, tunaongozwa na upendo – au ubinafsi?

Ni rahisi na hakika kama hivyo.

Wengine wanao jivunia uwezo wao kielimu, wanaweza wakapinga wakisema hii inafanana sana na kufikiri kwa mtazamo finyu. Wanaweza kusisitiza kwamba linapokuja suala la haki na uovu, ukweli na uongo, kuna vivuli vya kijivu, hakuna kitu kamili.

Lakini huwezi kama Biblia inavyofafanua; kuwatumikia mabwana wawili. Yakupasa kuchagua mmoja. Kristo? Au Shetani? Chagueni hivi leo ni nani mtakayemtumikia" – Yoshua 24:15

Kuna ukweli kamili usiochanganywa na uongo. Kuna upendo usio changanywa na ubinafsi. Kuna uaminifu kabisa kwa upande wa Mungu bila kuhusika na upande wa uovu.

### *Utusitusi wa Kijivu*

Changanya hata kidogo tu rangi nyeusi katika rangi nyingi nyeupe, utaishia kupata utusitusi kwa kijivu kidogo. Kwa kadri rangi nyeusi inavyoongezeka ndivyo kivuli kinaendelea kuwa na giza.

Mungu hakuumba utusitusi wo wote wa kijivu. Ukweli wake hauna uongo ndani yake. Upendo wake hauna

ubinafsi ndani yake. Nuru yake haina giza ndani yake. Mungu ni nuru na ndani yake hakuna giza kamwe – 1 Yohana 1:5 (imesisitizwa).

Hakuna uwanja wa katikati katika hili pambano kuu. Hakuna utusitusi wa kijivu kati ya wema na uovu, ukweli na uongo, ulio na maafikiano kati ya nuru na giza. Hakuna kusimama kwa kutagaa katika ua. Inaweza kuonekana machoni pako kwamba, waweza kuchagua pande zote, lakini haiwezekani kabisa, kama vile mafuta na maji visivyoweza kuchangamana.

Mada kuu ya kitabu hiki ni kwamba, Mungu amekuwa na watu watiifu kwake na kwa ukweli wake siku zote. Katika historia yote kumekuwa na watu ambao wamechagua kusimama imara upande wake katika pambano kuu. Hao ambao wamechagua upande wa Mungu daima wamekuwa ni wachache – na wakati fulani wamekuwa ni wachache sana.

> "Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba," Yesu alisema, "maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao *ni wengi* waingiao kwenye mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, nao waingiao *ni wachache*" – Mathayo 7:13, 14, (imesisitizwa).

Tayari unajua kisa hivyo hakuna haja tena ya kukueleza kwa undani zaidi. Unajua kwamba Mungu aliumba viumbe wake mbinguni na kuwapatia uhuru wa kuchagua, hivyo

wangeweza kumtumikia kwa sababu wanataka na sio kwa sababu wamelazimishwa. Unajua kwamba Lusifa alitumia uhuru wake wa kuchagua na akachagua kujiweka yeye mwenyewe mbale zaidi ya Mungu. Unajua kwamba hii ilisababisha vita mbinguni na kufukuzwa kwa Shetani pamoja na theluthi ya malaika waliokuwa wamedanganywa kutoka mbinguni. Unajua kwamba Mungu aliumba dunia kamilifu na ndani yake akaweka wanadamu wawili, wakamilifu, ambao pia aliwapa uhuru kamili wa kufanya uchaguzi. Unajua pia kwamba kwa huzuni, wao pia walifanya uchaguzi mbaya kabisa ambao ulifungua milango kwa ajili ya dhambi katika sayari yetu.

### *Asili ya Majani Kibichi Kugeuka kuwa Kahawia*

Adamu na Hawa walionekana kuangamia. Walipo yaona maua yakianguka na kufa .... majani yakigeuka rangi hatimaye kunyauka na kupukutika kutoka kwenye miti, waliomboleza sana kuliko watu wanavyoomboleza wakati wapendwa wao wanapokufa. – *Patriachs and Prophets* uk, 62. Walisononeka nakuwa wanyonge kabisa, na ghafla walifahamu hasara yote waliopata. Waliangamia kwa majuto na kufahamu kuwa hawakuwa na matumaini. Uchaguzi mmoja wa ubinafsi, ulikuwa umewaletea kifo – kana kwamba hawakuwahi kuwepo kabisa.

Mungu angewafutilia mbali kabisa, na wangine wasema ilimpasa Mungu kuwafutilia mbali kabisa. Alikuwa na kila haki ya kuwaruhusu kuvuna walichopanda. Lakini tunajua kwamba Mungu alichagua njia nyingine. Aliingilia kati

katika uchaguzi mbaya na hatimaye matokeo yake. Alimpa kila mtu nafasi nyingine ya kufanya uchaguzi.

Kwa huruma Mungu aliwaeleza Adamu na Hawa mpango wake wa kuwaokoa. Aliwafahamisha kwamba ingawa hawakupaswa kupona kutokana na uchaguzi wao wa ubinafsi, atawaokoa kutoka kwenye matokeo mabaya ya asili ya kifo cha milele kwa gharama ya kutisha ambayo ingemgharimu yeye mwenyewe.

Mungu aliwapa Adamu na Hawa nafasi nyingine ya uchaguzi.

Nakila mmoja katika kizazi chao, ili mradi kama angeishi, angepewa nafasi ile ile. Nafasi ya kuchagua upande anaotaka, kuchagua upendo au ubinafsi. Ukweli au uongo, Kristo au Shetani.

Tayari tunajua kwamba Adamu na Hawa waliishi muda mrefu na kwamba walitumia nafasi yao ya pili kwa hekima. Japokuwa walikuwa wameharibika na sio tena wakamilifu, kila siku walichagua kusimama imara katika upande wa Mungu.

Pia tumeshafahamu kwamba mara moja watu wa kizazi chao kila mmoja wapo alianza kufanya uchaguzi wa kuwa upande gani. Abeli mtoto wa Adamu na Hawa, kama ilivyoelezwa, alipeleka kafara ya mwana kondoo madhabahuni, akimwakilisha Mwana kondoo wa Mungu aokoae ambaye siku moja angelipa gharama yote ya dhambi. Nduguye Kaini pia aliamua kupeleka matunda ya kazi yake madhabahuni kinyume cha Mungu alivyo agiza, akionyesha kwamba anatumaini zaidi katika jitihada zake mwenyewe

za kibinadamu kuliko wokovu wa bure wa Mungu. Mungu alikubali sadaka ya Abeli na kukataa sadaka ya Kaini, Kaini alichukia sana, na mauaji ya kwanza ya mwanadamu yalitokea. Kaini alimwua Abeli.

Angalia wazo hili muhimu juu ya tukio hilo la kutisha – na ina maana gani kwako na kwangu, tunaoishi leo.

> "Kaini na Abeli wanawakilisha makundi mawili yatakayo kuwepo hadi wakati wa mwisho. Kundi moja wakinufaika na kafara ya ukombozi ya mwana kondoo, na kundi lingine likitegemea haki zao wenyewe. Sadaka yao haina uwezo wa upatanisho wa kiungu, na hivyo haina uwezo wa kumleta mwanadamu katika fadhila za Mungu. Ni kwa njia ya uwezo wa Kristo tu dhambi zetu zinaweza kusamehewa. Wale wasio na haja ya damu ya Kristo, wanaona kwamba bila hisani za kiungu wanaweza kuwa katika kazi yao wenyewe kupata ukubali wa Mungu, wanafanya makosa yale yale aliyofanya Kaini. Kama hawakubali damu ya utakaso wa Kristo, wako chini ya hukumu. Hakuna njia nyingine iliyowekwa ambayo kwayo wanaweza kuokolewa kutoka kwenye utumwa wa dhambi.
>
> "Kundi la waabuduo wanafuata mfano wa Kaini unajumuisha kiasi kikubwa sana cha ulimwengu kwa maana, karibu kila dini ya uongo imejengwa juu ya kanuni hiyo – kwamba mwanadamu anaweza kutegemea jitihada zake mwenyewe kwa ajili ya wokovu. Baadhi ya watu wanadai kwamba mwanadamu hahitaji ukombozi, bali maendeleo – yanayoweza kutakasa, kuinua na kujibadilisha

> yenyewe. Kama Kaini alivyofikiri kupata hisani za kiungu kwa kutoa kafara isiyo kuwa na damu, hao pia wanatarajia kumwinua mwanadamu kufikia kiwango cha Mungu, bila kutegemea upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu. Historia ya Kaini inaonyesha yatakayokuwa matokeo yake na jinsi mwanadamu atakavyokuwa bila Yesu. Wanadamu hawana nguvu za kujibadilisha wenyewe. Hakuna kwenda juu kuelekea katika utakatifu, bali huelekea chini, katika mambo ya kiShetani. Kristo ndio tumaini letu pekee. "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" Matendo ya Mitume 4:12 – *Patriachs and Prophets*, pp 72, 73.

Tangu mwanzo, kuna pande mbili tu. Upande aliochagua Abeli na wazazi wake – na upande aliochagua Kaini. Upande wa Kristo – au upande wa Shetani. Upande wa imani – au upande wa kazi za mwanadamu. Upande wa wanotii – au upande wa wakaidi. Upande wa wanyenyekevu kwa Mungu – au upande wa wanao nyenyekea kazi za mikono yao wenyewe (na kwa upanuzi, adui mkuu wa Shetani). Upande wa imani katika ukweli kuhusu Mungu – au katika upande wa uongo wa Shetani ambao ameutangaza juu ya Mungu.

Leo, pande hizi mbili tu ndizo zinaendelea kuwepo. Na kila mwanadamu anayeishi na kupumua amepewa nafasi ya kuchagua upande wa kusimama.

Adamu na Hawa walichagua.

Kaini na Abeli walichagua.

Kila mtu aliyewahi kuishi katika wakati uliopita, amefanya uchaguzi.

Leo hii, kila mtu duniani anafanya uamuzi huo huo. Wewe unachagua upande gani?

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 3

# Mfululizo Wa Waaminifu Usiokatika

Je, Mungu anaelekea kushindwa katika pambano kuu? Lusifa ambaye alikuwa malaika mkuu wa mbinguni – alijibadili mwenyewe kwa ajili ya uchaguzi wa ubinafsi kuwa Shetani, mwovu – kwa namna fulani inaweza kuonekana kana kwamba anashinda vita aliyoianzisha. Siyo kwamba tu alichukua theluthi ya malaika kutoka mbinguni, bali tangu mwanzo ameshinda kwa kuwa na watu (mateka) wengi zaidi.

Shetani alichagua. Adamu na Hawa walichagua – halafu wakachagua tena. Kaini na Abeli walichagua. Kutoka mwanzo kila mwanadamu aliyezaliwa imempasa kufanya uchaguzi wa namna hiyo hiyo. Na leo tunapohesabu kutoka mwaka 2000, idadi kubwa ya watu kati ya watu bilioni 6.5 waliopo ulimwenguni wapo kinyume cha Mungu na wamemchagua Shetani ambaye ni adui wa Mungu.

Bali wafuasi wa kweli na waaminifu wa Mungu wamekuwa wachache, na daima wataendelea kuwa wachache hata siku za mwisho. Waaminifu ni wachache. Hao wanaochagua njia nyembamba iendayo juu. Hao wanaosimama upande wa Mungu, haidhuru ni kiasi gani cha gharama watalipa kwa kufanya hivyo.

Kitabu hiki kinahusu mfululizo wa wafuasi halisi wa Mungu kuanzia Adamu na Hawa hadi wale wanaochagua kuwa upande wake leo.

Hebu turudi nyuma sasa na tuanze kufuatilia kisa hiki cha waliochagua kuwa upande wa Mungu, ingawa watu wengi zaidi wamechagua kuwa upande wa adui wa Mungu.

Baada ya kifo cha Abeli, Mungu aliwapa Adamu na Hawa mtoto mwingine. Seti alichagua kuwa mwaminifu kwa Mungu, kama vile Abeli kaka yake alivyochagua. Ukoo wa Seti katika vizazi mbalimbali walifuata nyao zake, walichagua kumfuata Mungu ambaye yeye mwenyewe alitembea na baba yao Adamu. Adamu aliishi karibu miaka elfu moja – muda mrefu kutosha kusimulia kisa cha huzuni, kilicho mhusu yeye mwenyewe, na kutumia kisa hiki kuwaonya watu wa kizazi chake kuhusu matokeo ya kutisha yaliyoletwa na uchaguzi huo.

Wakati huo huo watu wa kizazi cha Kaini walichagua kuwa na eneo lao, na kizazi baada ya kizazi waliamua kumwasi Mungu.

Lakini kwa kadri muda ulivyoendelea kizazi cha Kaini na Seti walianza kuchangamana kwa njia ya kuoana. Baada ya muda si mrefu watu wengi katika ukoo wa Seti walianza kuacha uaminifu wao kwa Mungu na kuanza kuchagua msimamo wa uasi wa familia kuu ya Kaini. Muda mfupi tu, watu wengi zaidi walijitoa kwa upande wa adui wa Mungu. Ingawaje, “ uasi ulikuwa unashinda, bado kulikuwa na ukoo wa watu watakatifu walioamuliwa na kufanywa kuwa waungwana kwa kuunganika na Mungu, waliishi katika

ushirikiano wa kimbingu" – *Patriachs and Prophets*, uk. 84.

Ukoo wa watu watakatifu.

Ukoo ulioanzishwa na Adamu na Hawa.

Ukoo uliodumu, bila kukatika kwa karne nyingi, yapata muda wa miaka 6,000 hivi sasa

Ukoo unaoweza kupatikana hata leo.

Katika ukoo huo wa watu watakatifu, mmoja wa watu wa zamani sasa, Biblia inasema alikuwa Henoko, – vizazi saba kutoka kwa Adamu. Alizungukwa na ongezeko la haraka la watu ulimwenguni, ambao wazi wazi walimwasi Mungu na kudhihaki ukweli wake, Henoko alitembea pamoja na Mungu. Wakati waovu wengi wa dunia hawakuwa na uhusiano na Mungu, Henoko aliendelea kumfahamu Mungu kwa undani zaidi.

Na Henoko hakuacha kuwasiliana na wale waliokuwa wamechagua kuwa kinyume na Mungu. Hakujifungia mwenyewe mlimani akijificha kwa ajili ya kutafakari na kuomba kwa muda wa saa ishirini na nne kila siku na hivyo kuwa mtakatifu. La, hasha badala yake alituachia kielelezo sisi tunaoishi katika ulimwengu unaozidi kumwasi Mungu, namna ya kuishi katika ulimwengu huu, wakati huo huo tusiwe watu wa ulimwengu. "Kutembea kwa Henoko na Mungu hakukuwa kwa kupagawa au njozi bali katika majukumu yote ya maisha yake ya kila siku. Hakuwa mtawa, akajifungia mwenyewe kabisa kutoka kwa ulimwengu, kwa sababu alikuwa na kazi ya kufanya ulimwenguni" – *Patriarchs and Prophets*, uk. 85.

Kwa Muda wa miaka mia tatu. Henoko alimwandama

Mungu kwa shauku kuu na umakini wa nafsi yake. Alimjua Mungu kabisa. Halafu jambo la kushangaza lilitokea.

### *Alitoweka!*

"Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye alitoweka; maana Mungu alimtwaa." Mwanzo 5:24

Henoko alipazwa – alichukuliwa kutoka duniani kwenda mbinguni, bila kufa – alikwenda kwa Mungu mara moja.

Kuwepo kwa Henoko kulipotea kabisa duniani, upepo ulisikika. Bali kutokana na muujiza huo Mungu alikuwa na mafundisho muhimu sana kuwafundisha wafuasi wake waliobaki duniani.

> "Kwa kutwaliwa kwa Henoko, Bwana alikuwa amepanga kufundisha somo muhimu. Kulikuwa na hatari kwamba mwanadamu angekata tamaa kwa sababu ya woga uliotokea kwa ajili ya dhambi ya Adamu. Wengi walikuwa tayari kuguta, 'tunapata faida gani kumcha Bwana na kutunza amri zake, kwa sababu laana nzito iko juu ya jamaa ya mwanadamu na kifo ni sehemu yetu wote?' Lakini maelezo ambayo Mungu alimpa Adamu, ambayo yalirudiwa na Seti na kufanyiwa kazi na Henoko, yalifutilia mbali utusitusi na giza, na kumpa mwanadamu tumaini, kwamba kwa kupitia Adamu kifo kilikuja, hivyo kwa kupitia kwa ahadi Mwokozi maisha na kutokufa vitakuja. Shetani alikuwa akiwaambia wanadamu kwamba, 'hakuna thawabu kwa wenye haki au adhabu kwa waovu, na kwamba haiwezekani mwanadamu kutii amri takatifu.' Bali

kwa kisa cha Henoko, Mungu anatangaza kwamba 'yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu watu wamfuatao,' Waebrania 11:6. Anaonyesha kwamba atafanya kwa wale wanaotunza amri zake. Wanadamu walifundishwa kwamba inawezekana kutii sheria ya Mungu; kwamba hata kama wanaishi katikati ya wadhambi na waovu, wanaweza kwa neema ya Mungu, kuyashinda majaribu, na kuishi maisha safi na Matakatifu. Waliona katika mfano wake baraka za maisha na kutwaliwa kwake kuwa ulikuwa ushahidi wa ukweli wa unabii wake juu ya maisha baada ya haya, pamoja na thawabu ya furaha na utukufu wa maisha ya kutokufa kwa mtiifu, na maangamizo, laana na kifo kwa mwasi" – *Patriachs and Prophets*, uk. 88.

Hivyo mafundisho makuu katika maisha ya Henoko hadi wakati wa kutwaliwa yalilenga juu ya kitu gani?

- Kutwaliwa kwa Henoko kulileta matumaini kwa waaminifu waliopo duniani.
- Ilihakikisha kwamba wenye haki hupata thawabu – kama vile waovu walivyo na adhabu ya mwisho.
- Maisha ya Henoko yalionyesha kwamba inawezekana kutunza amri za Mungu na kushinda majaribu, hata kama umezungukwa na ulimwengu mwovu na ulioasi.
- Kutwaliwa kwa Henoko kulikuwa ni mfano mdogo wa thawabu ya mwisho itakayofurahiwa na wafuasi waaminifu wa Mungu katika maisha ya baadaye; baada ya maisha haya ya duniani.
- Mafundisho haya hayakuwa tu kwa marafiki zake Henoko waliobaki kuendeleza uaminifu baada ya

kutwaliwa kwake.

Ni kwa ajili yako na ni kwa ajili yangu. Kuchagua upande wa Mungu kuna thawabu kwa sasa na hata katika maisha ya umilele ambayo karibu yataanza. Maisha ya Henoko yalidhibitisha kwamba inawezekana kuwa waamifu na watiifu kwa Mungu, bila kujali ni jinsi gani ulimwengu unaotunzunguka umeasi.

Kumbuka kwamba, kuishi maisha ya utiifu si matokeo ya uwezo wa utashi wetu jitihada na dhamira. Hebu tuangalie tena sentensi kutoka kwenye nukuu ya karibu katika sura hii.

> "Wanadamu walifundishwa kwamba inawezekana kutii sheria ya Mungu; kwamba hata kama wanaishi katikati ya wadhambi na waovu, wanaweza *kwa neema ya Mungu*, kuyashinda majaribu na kuishi maisha safi na matakatifu." (imesisitizwa).

### *Msamaha na Nguvu*

Neema ya Mungu. Neema hiyo ina mambo mawili. Ni msamaha – kuwiwa radhi – kwa dhambi yetu ya asili – jinsi tulivyo, pia kwa ajili ya dhambi tunazotenda na yale tunayo yafanya.

Neema pia ina uwezo wa kufanya tusitende dhambi. Tunahitaji yote mawili. Na kwa sababu chachu ya dhambi - ya ubinafsi - siku zote itakuwa ndani yetu tukiwa hapa duniani, bila kuondolewa hadi Yesu atakaporudi, tutahitaji neema katika mambo yote mawili.Wakati huo huo

Mungu anatuhitaji tena na tena tuweze kuwa kama yeye tunapokuwa katika neema, – hii ni kwamba, kwa kadri tunavyojifunza kila siku tunamtegemea zaidi na zaidi kwa ukamilifu.

Kama unahitaji kujifunza ukoo mwaminifu, soma tena sura ya tano ya kitabu cha Mwanzo. Hapo kuna kizazi baada ya kizazi. Biblia inafuatilia moja kwa moja wafuasi waaminifu wa Mungu kutoka kwa Adamu hadi kwa Nuhu. Katika ukoo huo utagundua kwamba kabla ya kutwaliwa kwake, Henoko alikuwa na mtoto aitwaye Methusela – anajulikana kama mtu aliyeishi muda mrefu kuliko watu wote duniani. Methusela aliishi umri wa kushangaza wa miaka 969. Mwana wa Methusela, Lameki ndiye alikuwa baba wa Nuhu.

Hakuna haja ya kuwa na maelezo zaidi juu ya maisha na huduma ya Nuhu. Kila mtoto wa shule ya kikristo anajua kwamba nuhu alihubiri miaka 120 akiwa anajenga safina. Dunia ilikuwa imekuwa na uovu zaidi ya vile inavyoweza kuelezwa. "Bwana akaona yakuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake *ni baya tu siku zote*" Mwanzo 6:5 (imesisitizwa).

Kabla uaminifu haujashindwa kabisa na uovu Mungu aliingia kati na kuleta gharika ambayo iliangamiza kizazi kiovu chote duniani. Waliosalia walikuwa wanafamilia wa Nuhu nane tu waliongia katika safina na kuendeshwa nayo na hatimaye kutoka salama kwenye gharika.

Wanadamu walikuwa na mwanzo mpya – kuanza

kupya.

Hata hivyo Nuhu na familia yake walibeba virusi vya dhambi, hivyo haikuchukua muda mrefu kabla baadhi ya watu katika ukoo wa Nuhu kuacha kufuata mfano wa maisha na mafundisho yake, wakachagua kuwa kinyume na Mungu na kufuata matakwa yao ya ubinafsi. Hatimaye, hawa wafuasi wa Shetani waliongezeka na kuenea duniani kote.

Hawa waasi dhidi ya Mungu waliongezeka duniani kiasi kwamba, uasi zaidi, upagani na mambo mengi ya upagani nayo yakazidi. Kujitenga wenyewe kutoka kwa waaminifu wa Mungu, walikuwa wakae kwenye uwanda mkubwa sana na kudhamiria kujenga mji mkubwa kuliko miji yote duniani wenye ishara ya mnara mrefu sana ambao ungekuwa ni ajabu ya ulimwengu.

Mnara mkuu wa Babeli ulianza kupanda angani. Shetani, ambaye anakuwa nyuma ya jukwaa, anawachochea watu kuasi na kufanya kazi kupitia wao ili kufanikisha mipango yake, alikuwa lazima aridhike sana kwa maendeleo ya mji wa Babeli. Lakini Mungu hajawahi kamwe kuruhusu adui mkuu kuendeleza vita bila kuvipinga. Kabla ya mnara kumalizika, Mungu aliingilia kati na kuchafua lugha za wafanya kazi waliokuwa wakijenga mnara huo. Ghafla, ujenzi ulilazimika kusimamishwa.

> “Mipango ya wajenzi wa Babeli iliisha kwa aibu na kushindwa. Kumbukumbu ya fahari yao ilikuwa ya ukumbusho wa upuuzi wao. Hata sasa bado watu

wanaendelea kufanya mambo yale yale ya Babeli – kutegemea ubinafsi, na kukataa sheria ya Mungu. Hii ni kanuni ambayo Shetani alijaribu kuendeleza mbinguni, kanuni hiyo hiyo iliyomwongoza Kaini katika kutoa sadaka yake.

"Kuna wajenzi wa mnara katika siku zetu. Makafiri wanabuni nadharia kutoka kwa kinachodhaniwa kuwa sayansi, na kukataa wazi wazi neno la Mungu. Wanakusudia kuihukumu serikali adilifu ya Mungu, wanadharau sheria yake na kujivuna na uwezo wa mwanadamu wa kufikiri " – *Patriachs and Prophets* uk. 123, 124. (imesisitizwa).

***Wajenzi wa Mnara***

Mnara wa nadharia ya uibukaji (evolution). Mnara wa fikira za mwanadamu. Mnara wa sayansi inayoinuka kuliko neno la Mungu. Mnara wa ubinadamu unaobuni kanuni za maadili na kukataa sheria ya Mungu. Bali minara hii pia itaanguka mwishowe. Naam, Babeli mpya inainuka hata leo, lakini pia itaanguka kwa uhakika. Kitabu cha Ufunuo ni mkazo: kamwe Mungu hatamruhusu Shetani pasipo kumpinga, katika ujenzi wa Babeli yeyote mpya.

Kutokana na gharika, ukoo mwaminifu umepewa nafasi mpya kuishi – na kuendelea kuishi. Sura ya 11 ya kitabu cha Mwanzo inachukua ukoo, inafuatilia kutoka kwa mtoto wa Nuhu, Shemu, hadi vizazi vinavyofuatia kwa mmoja wa mashujaa wakuu wa imani katika Agano la Kale: Abramu ambaye baadaye aliitwa Abrahamu.

Inadhaniwa kwamba wasomaji wa kitabu hiki wanafahamu vizuri kisa cha Abrahamu: agano la ahadi aliyofanya Mungu kwake kwamba atakuwa baba wa taifa kubwa. Mungu alimwita aache kila kitu na kuondoka – bila kujua alikokuwa anakwenda – kufuata mwongozo wa Mungu hadi kwenye nchi ambayo Mungu angemwonyesha. Kuokolewa kwa mpwa wa Abrahamu (Lutu) kutoka Sodoma, mji ambao ulikuwa umejitoa kikamilifu kwa uovu pamoja na mji jirani wa Gomora, Mungu aliamua kuwafutilia mbali watu wa miji hiyo toka uso wa dunia. Na bila shaka kuzaa kwa namna ya ajabu Abrahamu katika umri wa miaka mia moja – na mke wake katika umri wa miaka tisini – walipopata mwana wa ahadi Isaka.

Baadaye Isaka alizaa mapacha wa kiume – Yakobo na Esau. Watoto hawa pia walipewa na Mungu nguvu ya uhuru ya utashi ya kuchagua kufanya maamuzi ya maisha yao. Esau aliasi na kujiweka mwenyewe kwenye upande wa adui wa Mungu – Yakobo – kwa namna ya hila ya wazi katika mambo fulani aliweza kuendelea katika ukoo mwaminifu. Baada ya usiku mrefu wa mwereka pamoja na malaika – malaika aliyegeuka kuwa Mungu mwenyewe – Yakobo alipewa jina jipya la Israeli.

Watoto kumi na mbili wa Israeli walikuwa baba wa mataifa kumi na mbili ya wana wa Israeli. Israeli kwa namna ya pekee alichaguliwa na Mungu kuhifadhi, kulinda na kushuhudia, ulimwengu mwovu uliowazunguka juu ya ukweli kuhusu tabia ya Mungu. Njozi ya Mungu na kusudi lake, kwa taifa la Israeli, ilikuwa ni ya kushangaza.

Aliwachagua kuyaeleza mataifa yanayowazunguka yasiyoamini juu ya nguvu za pendo na neema za Mungu. Aliwachagua wawe ni waangalizi wa ukweli wake – sio kuhodhi bali kutunza hata wanaposhuhudia kwa watu wa mataifa wanaowazunguka. Aliwachagua kutayarisha njia ya mwokozi kuinuka kutoka kwao.

Ukoo wa waaminifu ulioanza kwa Adamu na Sethi – ambao ulisafiri hadi kwa wazee akina Henoko na Methusela na Nuhu, Abrahamu, na Isaka, na Yakobo – na sasa ulifika kwa taifa zima ambalo kwa namna ya pekee lilichagualiwa na Mungu kumwakilisha duniani.

Wangewezaje – waliwezaje –kuinuka kufikia majaliwa yao?

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 4

# Kuwarejesha Waasi Kwa Njia Ya Upendo

Kujiweka katika nafasi ya Mungu, hii ni, kufikiria kuwa (au kujaribu kutumia) nguvu zake na nafasi (nyadhifa) za kiungu – ni kufuru.

Bali ni jambo jingine kabisa kujiweka katika nafasi ya Mungu, kwa maana ya kujaribu kuangalia mambo katika mtazamo wake. Albert Einstein wakati fulani alisema kwamba sayansi ni "kufikiri fikira za Mungu baada yake." Lakini hatuhitaji kuwa wanasayansi ili kufanya hivyo.

Hivyo kwa muda kitambo, jaribu kujiweka mwenyewe katika nafasi ya Mungu! Fikiria kwamba wewe umeumba ulimwengu mkamilifu. Umeumba malaika wakamilifu na wanadamu wakamilifu. Na umewaumba na utashi – na uhuru wa uchaguzi.

Kwa kuwapa uhuru wa utashi ina maana kwamba wanaweza kukutumikia na kukuabudu kama wakitaka kwa kufanya uchaguzi na siyo kwa sababu wanapaswa kufanya hivyo. Lakini kwa kuwapa uhuru kunakaribisha uwezekano wa kupata hasara ama pata potea. Wangeweza kuchagua kuwa kinyume na wewe. Kwa huzuni ndivyo wanavyofanya. Katika dunia kama ilivyo sasa wanadamu waovu wanaendelea kuongezeka, wengi wao wameasi dhidi

yako. Hata hivyo pamoja na asili yao ya dhambi, waaminifu wachache wanachagua kukuabudu kama Mwumbaji wao. Katika nguzo za awali za imani kuna watu wanaoishi umri wa miaka – 700, 800, na 900 kabla ya kufa. Dunia inazidisha uovu kiasi kwamba unaamua kuleta gharika kuu kuwaangamiza watu wote waovu na kuanza upya na wafuasi waaminifu wachache – familia ya Nuhu tu. Lakini wakati mfupi tu, wanadamu wanaongezeka tena na kuenea duniani kote, wengi wao wanakuwa kinyume na wewe.

Unawarudishaje waasi?

Unawafikiaje waovu, watu wasio mcha Mungu, wapagani?

Je, unawatuma malaika walio upande wako waende kuwahubiri hawa waovu? Je, unawaita wafuasi wako waaminifu wachahe duniani ili waende kuwaonya watenda dhambi – kuwabembeleza, kuwahubiri na kuhukumu dhambi zao?

### *Wazo la Mungu*

Kama tatizo lingekuwa langu au lako, kulitatua tungeweza kuchagua njia moja wapo ya hiyo. Bali Mungu alikuwa na wazo tofauti.

Alijifunua wazi yeye mwenyewe kwa waasi. Aliwaonyesha tabia yake ya upendo na kutegemea nguvu za upendo huo kuwavuta tena kwake mwenyewe.

Bali hakuweza kufanya yeye mwenyewe. Alifanya kwa kupitia wafuasi wake waaminifu waliopo duniani. Wakati ulifika ambapo kazi hiyo ya kuufikia ulimwengu mwovu

ilikuwa ngumu sana kwa watu wachache. Hivyo Mungu hakuwaagiza watu wachache tu waliotawanyika duniani kufanya kazi hii bali kwa taifa zima, taifa alililoliteua na kulibariki kwa kila kitu wanachohitaji kuonyesha upendo kwa majirani zao wasioamini.

Kwa awali Mungu alifunua mpango wake kwa Abramu wakati fulani kama 1800 K.K. Akiwa amezungukwa na upagani na uabudu sanamu na uasi. Abramu – kama alivyokuwa akiitwa kwa wakati huo – alibaki kuwa mwaminifu kwa Mungu.

Abramu alipokuwa na umri wa miaka 75, Mungu aliongea naye na kufanya ahadi ya kushangaza naye: "Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe utakuwa baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe na jamaa zote za dunia watabarikiwa" Mwanzo 12:2, 3.

Pamoja na ahadi hii kuu, Mungu pia alimpa amri: "Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha" Mwanzo 12:1.

Abramu alimtii Mungu, bila kusita sita na bila swali. "Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijuwe aendako. Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, alikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile" Waebrania 11:8, 9.

Hivyo Abrahmu alihama kutoka katika nchi ya jamaa zake Harani kwenda katika nchi aliyo onyeshwa na Mungu;

Kanani.

Sio kusudi la kitabu hiki kufuatilia kwa undani historia ya Israeli kutoka wakati wa Ibrahimu katika mwaka 1800 K.K. hadi kufikia wakati wa maisha ya Yesu duniani. Mfululizo usiokatika wa waaminifu ulianzia kwa Adamu na kuendelea katika vizazi mbali mbali hadi kwa Ibrahimu ukaendelezwa na mwana wa Ibrahimu Isaka, na mwana wa Isaka Yakobo – aliyeitwa baadaye Israeli. Na bila shaka watoto kumi na wawili wa Isaka walikuwa waanzilishi wa makabila kumi na mbili ya taifa la Israeli.

Kama Mwadventista, kuna uwezekano mkubwa kwamba tayari unajua vizuri historia ndefu ya wana wa Israeli; Mashujaa wa imani, manabii, wafalme, kipindi kirefu cha utumwa Misri, kutoka miaka arobaini ya safari jangwani, safari ya kwenda kwenye nchi ya ahadi, kuchukuliwa utumwani Babeli na mwishowe kugawanyika kwa Israeli katika tawala mbili; kaskazini na kusini.

Yawezekana pia kwamba unafahamu vizuri juu ya pasaka na Bahari ya Shamu, juu ya Sinai na hekalu la jangwani, juu ya kuasi kwa mara kwa mara kwa Waisraeli na kuungama, na juu ya majina makuu ya Historia ya Israeli: Yusufu, Musa, Daudi, Sulemani, Samweli, Danieli, na wengine wengi.

Waaminifu wachache wanaweza kupata tuzo kama inavyoonyesha katika historia ya taifa la Wayahudi kutoka katika kitabu cha Mwanzo 11 na kuendelea – au katika vitabu vya Mashujaa wa Imani na Manabii na Wafalme.

Lengo kuu la sura hii sio juu ya historia ya Israeli –

utaratibu wa kupanga miaka na matukio, na viongozi, tarehe na mahali, nyakati za pande zote mbili za uaminifu na uasi. Badala yake, kwa mara nyingine tena tunaendeleza mbele kisa cha wafuasi wa Mungu wanyenyekevu – waaminifu wachache ambao wamekuwa wakweli kwa Bwana tangu wakati wa Adamu hadi wakati huu.

### *Kuchaguliwa – kwa Kusudi*

Katika aya chache, tumezungumzia juu ya Israeli kama taifa teule la Mungu – na juu ya sababu ya Mungu kuwachagua.

Mungu alikuwa na kusudi kuu kwa taifa la Israeli. Aliwakabidhi mibaraka na ahadi ambazo zilikuwa ni za kushangaza sana kuzielewa kikamilifu. Lakini mibaraka na na ahadi hizo zilikuwa zenye masharti. Kama wangemtii Mungu kikamilifu na kuishi kulingana na masharti hayo – wangekuwa ni taifa la kushangaza sana katika mataifa yote ya duniani. Kama sivyo wangeshindwa hata kuwa mateka wa maadui zao.

Tayari tumeshajua kwa sehemu tu – na ni sehemu tu ya wakati – inayo onyesha jinsi wana wa Israeli walivyo kamilisha mpango na kusudi la Mungu kwa ajili yao. Na tayari tumeshajua kwamba hatimaye, walimkataa Mungu kabisa – katika umbo la Yesu – na hata walishiriki katika kumuua Mwumbaji wao.

Lakini wakati Israeli ilikuwa duni – wakati wa uasi wao mkuu – daima kulikuwa na Waisraeli wachache waaminifu, wanyenyekevu na wafuasi wa kweli wa Mungu. Imekuwa

hivyo baada ya taifa la Israeli.

Uchaguzi ule ule ambao kila mwisraeli alipaswa afanye, ndio wewe na mimi tunatakiwa tufanye leo. Je, tutasimama imara na kwa unyenyekevu kamili katika upande wa Mungu wetu? Je, tutabaki upande wake kwaukamilifu hata kama wakati mwingine itaonekana si ulimwengu tu uliomwacha, bali watu wengi kanisani pengine hata ndugu zetu – watamwasi?

Kuangalia tena mpango mkuu na kusudi la Mungu kwa Israeli kunatusaidia kuangalia tena kusudi lile lile la Mungu kwa kanisa la leo – mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yako na yangu.

Kusudi hilo lilikuwa nini?

> "Walipaswa kufunua kanuni za ufalme wa Mungu. Katika ulimwengu huu mwovu ulioanguka, walipaswa kuwakilisha tabia ya Mungu. Kama shamba la mizabibu la Bwana walipaswa kuzaa matunda tofauti na mataifa ya kipagani .... Ilikuwa ni wasaa wa taifa la wayahudi kuwakilisha tabia ya Mungu" *Christ's Object Lessons* (COL), p. 285.

> "Ilikuwa ni kusudi la Mungu kwamba kwa njia ya Ufunuo wa tabia yake kupitia Israeli, watu wengi wangevutwa kwake" – COL, p. 290.

Ujumbe wa Israeli? Sababu ya Mungu kuwachagua? Kuwakilisha tabia ya Mungu kwa mataifa yasioamini na kuasi. Na kama Mungu alivyo onyesha tabia yake na wema

wake, wema unao jumuisha rehema neema na upole, ukweli na msamaha. Hatimaye, wema wote wa Mungu unapatikana katika upendo wake.

Mungu alihitaji kuurejesha kwake ulimwengu ulioasi dhidi yake. Mpango wake ulikuwa ni kuwarudisha kupitia kwa taifa teule. Kusudi lake ilikuwa kwamba Israeli iinue tabia ya Mungu katika maisha yao –na kwamba kwa kupitia taifa la Israeli angeupenda ulimwengu tena.

> "Kwa kupitia taifa la Wayahudi ilikuwa ni kusudi la Mungu kutoa mibaraka mingi kwa watu wote. Kwa kupitia taifa la Israeli njia ilikuwa inatayarishwa kwa ajili ya mtawanyiko wa nuru yake kwa ulimwengu wote. Mataifa ya ulimwengu, kutokana na matendo ya ufisadi, yalipoteza elimu ya Mungu. Lakini bado kwa rehema zake Mungu hakumfutilia mbali kabisa. Alikusudia kuwapa nafasi ya kumjua yeye kwa kupitia kanisa lake" –COL, uk. 286.

Kumbuka vizuri jinsi ambavyo Waisraeli walipaswa kuyarudisha mataifa yote kwa Mungu. Je, ilikuwa ni kuwahukumu kwa ibada zao za miungu, uovu, na njia za kipagani?

### *Kitu Bora*

Mara kadhaa leo, hata wahubiri maarufu wanahukumu hadharani dhambi za watu walio mwacha Mungu katika maisha yao. Wanawatisha wadhambi na hukumu ya ghadhabu ya Mungu. Au maafa ya asili yanapotokea,

wanawaambia kuwa ni ushahidi wa hasira na kutofurahishwa kwa Mungu.

Je, hiki ndicho Mungu alituita tufanye? Je, ndicho alichowaitia wana wa Israeli kufanya?

> “Watu waulimwengu wanaabudu miungu ya uongo. Wanapaswa warudishwe kutoka kwa ibada ya uongo, siyo ya kusikia shutuma za sanamu zao, bali kuangalia kitu fulani bora. Wema wa Mungu unapaswa kuelezwa wazi” COL, p. 299.

Naam, hao wanaishi mbali na Mungu wapo katika dhambi za kuchukiza mno. Lakini kama ni Waisraeli wa zamani au watu wa Mungu wa leo, je, ni ujumbe wa wafuasi wa Mungu kuhukumu, kushutumu, kuiita hukumu ya Mungu?

Au badala yake ni kuonyesha ulimwengu kitu kilicho bora? Na nini kilicho bora? Wema wa Mungu. Tabia yake. Upendo wake.

Katika kuufilia ulimwengu wa dhambi kwa kupitia wafuasi wa Mungu, je, Mungu amewahi kuutishia ulimwengu ili umrudie? Kuwarudisha kwa hasira na shutuma? Kwa kuwatisha na dhambi zao?

Au sio kwamba badala yake Mungu ana njia moja tu ya kuwarudisha waasi: kuwaonyesha upendo wake kwa uwazi zaidi iliwasijizuie kumrudia.

Kama usemi wa wahenga usemavyo: unashika nzi wengi kwa kutumia asali kuliko kwa kutumia siki. Na kama

hivyo ni kweli kwa nzi wachafu, wabaya, ni kweli pia kwa wale waliokwama katika uchafu wa dhambi.

Mungu hahitaji zaidi wanasheria waendeshe mashitaka. Anahitaji zaidi mashahidi watakoeleza ukweli juu yake.

Kusudi la Mungu kwa ajili ya Israeli ya zamani lingefanikiwa kama Waisraeli wangeshirikiana na Mungu. Mungu asingewapa tena wateule wake kitu kingine zaidi ya walichohitaji ili kuwa wawakilishi wake. Mungu hakuzuia chochote.

> "Mungu alitamani kuwafanya watu wake Israeli sifa na utukufu, kila faida ya kiroho aliwapa. Mungu hakuzuia kitu chochote chema kwa ajili ya matengenezo ya tabia waliyohitaji ili kuwa wawakilishi wake," – COL, uk. 288.

Lakini pamoja na ahadi zote za mibaraka ya Mungu – pamoja na uwezo usio na kikomo aliowapa Mungu, bado walishindwa kutimiza masharti aliyoweka Mungu, walikosa kabisa mibaraka ya Mungu.

Tafakari yale ambayo wana wa Israeli wangefurahia:

> "Kama watiifu, wangelindwa kutokana na maradhi yaliyowapata mataifa mengine, wangebarikiwa na uwezo wa pekee wa kiakili. Utukufu wa Mungu, ufahari na nguvu zake vingefunuliwa katika mafanikio yao yote. Walikuwa wawe ni utawala wa makuhani na wana wa kifalme. Mungu aliwapa kila kitu kilicho hitajika kwa ajili ya kuwa taifa kuu duniani" – COL, uk. 288.

- Ulinzi kutokana na maradhi.
- Uwezo pekee wa kiakili.
- Mafanikio.
- Kila mbaraka unaoweza kufikiriwa.

Israeli ingekuwa ni maajabu ya ulimwengu – taifa kubwa kuliko yote duniani. Lakini kwa huzuni, wametumia karne nyingi kwa kushindwa na kuwa mateka wa vita. Maneno sita (saba katika kiingereza) yanayorudiwarudiwa, maneno yana onyesha hatima ya kushindwa kwa Israeli:

> "Lakini Israeli haikukamilisha kusudi la Mumgu" – COL, uk. 290.

Iliwezekanaje – ingewezekanaje hili kutokea?

> "Walimsahau Mungu, na kupoteza mtazamo wao kama wawakilishi wa Mungu. Mibaraka waliyopokea haikuleta mibaraka kwa ulimwengu. Faida zote zilitwaliwa kwa ajili ya utukufu wao binafsi. Walimtolea Mungu wao huduma iliyo duni kukinganishwa na ile aliyohitaji kutoka kwao, na kwa kufanya hivyo walishindwa kufikisha kwa binadamu wenzao uongozi wa kidini na kielelezo kitakatifu" – COL, uk. 291, 292.

Kama taifa, Israeli wangekamilisha ujumbe kutoka kwa Mungu kwa kiwango kikuu kamwe isingeweza kutweka. Bali kushindwa kwao ilikuwa ni balaa kuu.

> "Wayahudi walithamini wazo la kwamba walikuwa

> wapendwa wa mbinguni, na kwamba daima waliinuliwa kama kanisa la Mungu. Walikuwa ni wana wa Ibrahimu, walitangazwa, na hivyo kwa ujasiri msingi wa mafanikio yao ulionekana kana kwamba wamepata haki yao ya kurithi mbingu na nchi. Bali kwa maisha yao ya dhambi yaliwaandaa kwa hukumu ya mbinguni na utengano na Mungu" – COL, uk. 294.

Pamoja na kwamba taifa la Wayahudi lilijiondoa lenyewe kutoka kwa Mungu, ulimwengu huu haukuachwa bila wanaume na wanawake waliodumu kuwa waaminifu kwa Mungu – wale waliompenda kwa mioyo yao yote na kumtumikia kwa uaminifu, bila kujali lo lolote.

*Mfululizo wa waaminifu haukuwahi kukatika.*

Yesu alipokuja katika dunia hii kama mtoto mchanga, wachache, baadhi ya waaminifu hao walikaribisha kuzaliwa kwake kwa shangwe na utambuzi, pamoja na kwamba kundi kubwa kabisa walimkataa au hata hawakumtambua.

Katika miaka ya ukuaji wa Kristo na miaka mitatu na nusu ya huduma yake, ulimwengu huu kamwe haukukosa kabisa kuwa na watu waliompenda Mungu, wale waliokuwa tayari kufa kuliko kumwasi muumbaji wao na masihi.

Kisa cha kitabu hiki ni kisa cha waaminifu wachache – kisa tunachofuatilia kutoka kwa Adamu hadi wakati huu wa mwisho. Ni kisa ambacho ni zaidi ya ufupisho tu wa historia. Kwa sababu kisa hiki kinakuhusu wewe – na mimi, inabidi tuchague upande tutakao kuwa. Haijawahi kutokea, mwaka huu, mwezi huu, leo hii – kuna pande mbili tu

ambazo kwazo inabidi tufanye uamuzi.

Unaweza kuchagua kuwa mwaaminifu na mnyenyekevu kwa Mungu, au kuwa upande wa wale wanaochagua kwenda njia zao wenyewe.

Ni uchaguzi ambao lazima uukabili tena kabla ya siku ya leo kupita, na kabla hujaamka kukabili siku nyingine.

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 5

# Kukosea Katika Kumtazamia Mfalme

Fikiria unaenda kazini asubuhi, halafu unaporudi nyumbani jioni unakuta familia yako haikutambui wewe ni mgeni kabisa!

Au fikiria unakwenda kwenye sherehe ya kifamilia, unakuta kwamba hakuna mtu anayekufahamu hata kidogo kwamba wewe ni nani.

Hebu tuwe na tumaini kwamba jambo la namna hiyo halitatokea kwako. Lakini lilitokea kwa Yesu.

> "Alikuwako ulimwenguni; hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuweko, *wala ulimwengu haukumtambua*. Alikuja kwake wala *walio wake hawakumpokea*" – Yohana 1:10, 11 (imesisitizwa).

Tafsiri nyingine ya Biblia inasema hivi:

> "Ingawa ulimwengu uliumbwa naye, *ulimwengu haukumtambua alipokuja*. Hata katika nchi yake na miongoni mwa watu wake, *hakukubaliwa*" – New Living Translation, (imesisitizwa).

Ilikuwa vibaya sana kwamba ulimwengu haukumjua

Yesu alipokuja duniani. Hata hivyo alikuwa Mwumbaji wao pia, wamtambue au wasimtambue –alikuja kuleta wokovu, sio kwa ajili yake mwenyewe bali kwa ajili ya ulimwengu.

Naam, ilikuwa vibaya sana kwamba ulimwengu haukumtambua. Bali jambo lisiloweza kuaminika, hata waliowake walimkataa.

Mungu alitoa unabii maalum angalau mara mia tatu kueleza kuja kwa Yesu, na bado watu wake walimkataa.

Kwa kupitia Maandiko Matakatifu walifahamishwa jinsi gani, wapi na lini Yesu angekuja, watu wake walimkataa.

Lakini sio wote!

Hebu tuangalie vizuri tena. Kutoka mwanzo, Mungu amekuwa na ukoo wa wafuasi waaminifu walio mfahamu, walio watiifu kwake, na walio mtumainia na kumpenda. Na kutoka mwanzo wamekuwa wachache. Ni "wachache" wamtafutao na kusafiri katika njia nyembamba inayoongoza juu kwenda uzimani. Wengi wanachukua njia rahisi nakutembea kwenye njia pana iongozayo kwenda mautini.

Wengine wanaweza kufikiri kwamba kama – wakati historia ya ulimwengu itakuwa imekwisha – wachache tu wakiwa wameokolewa na kuwa na uzima wa milele, wakati ambapo wengi wamepotea na kuangamizwa kabisa halafu tena Shetani lazima ashinde na Mungu lazima ashindwe.

Ni kweli kwamba wakati muda wa duniani utakuwa umekwisha na umilele unaanza, kati ya mabilioni ya watu waliowahi kuishi duniani watakao okolewa watakuwa ni wachache sana lakini kumbuka vitu hivi vitatu:

1. Maisha ya kuokolewa kupitia kifo cha Yesu vimeleta

wokovu wa bure kwa kila mtu. Mungu ni mvumilivu kwetu, maana hapendi *yeyote* apotee, bali *wote* wafikirie toba" – 2 Petro 3:9 (imesisitizwa). Hivyo Mungu hachagui kuwaokoa wengine na wengine kupotea. Kila mtu – kwa kutumia uwezo wa uhuru wa uchaguzi ambao Mungu alimpa kila mtu katika uumbaji – hatimaye anachagua mwisho wa safari yake ya maisha.

2. Mwisho wa pambano kuu kati ya wema na uovu – kati ya Kristo na Shetani – haujafika bado. Mwishoni pambano litaonyeshwa wazi wazi kabla ya kurudi kwa Yesu, kundi kubwa sana watawaunga wafuasi waaminifu wa Kristo. Baadhi watatoka upande wa adui, wengine waliojizuia kufanya uchaguzi watafanya. Hatuwezi kuacha kusema tena kwamba; tukilinganisha na watu walio jaza dunia hii, ni wachache wataokolewa – kundi dogo sana la kusikitisha. Hata hivyo, Yohana katika ufunuo – akiangalia mbinguni – aliona "*mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu*, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi na mbele za Mwana – kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao" – Ufunuo 7:9 (imesisitizwa).
3. Hatimaye, nabii Isaya anasema kwamba wakati pambano litakapokwisha, "Yesu mwenyewe ataona mazao ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika" – Isaya 53:11. Kafara kubwa mno aliyoifanya Yesu kuwaokoa

wanaume na wanawake, ataridhika wokovu wa watu hao unastahili kafara aliyoitoa, maumivu aliyopata na hata kifo chake msalabani.

Hivyo hatupaswi kujali kwamba wafuasi waaminifu wa Yesu ni – na wamekuwa daima – wachache katika idadi. Na Yesu atakaporudi hapa duniani kwa ajili ya utimilifu wa ahadi na unabii, wale woliokuwa wake kweli walikuwa wachache sana kiasi kwamba kwa usahihi Biblia inaeleza kwamba walio wake – taifa alilochagua kumwakilisha hapa duniani hawakumpokea.

***Macho yasiyoona, Masikio Yasiyosikia***

Walikuwa na unabii. Mungu alihakikisha kwamba hakuna maelezo yo yote ya undani kuhusu kuja kwa Yesu hayakutolewa kwao. Lakini uasi wa muda mrefu wa kurudiwarudiwa ulipofusha macho ya taifa teule la Mungu hasa viongozi wake. Walikuwa na macho ya kusomea, lakini hawakuweza kuona. Walikuwa na masikio ya kusikia manabii, bali hawakuweza kuelewa.

Wakiongozwa na roho ile ile iliyomsukuma Lusifa kujiinua mwenyewe, walijawa na shauku kuu ya kuwa taifa kuu ambalo lingeweza kutawala na kuongoza mataifa yote. Lakini ukuu wa taifa ambao Mungu alikuwa akihitaji kwa ajili yao ilikuwa ni ukuu wa utumishi sio nguvu, ya utawala wa kijeshi.

Naam, Waisraeli waliamini juu ya kuja kwa Masiha, lakini waliingiza mawazo yao wenyewe waliyotamani katika

unabii wa kuja kwake. Hawakuhitaji – na hawakutazamia – Masiha ambaye angekuja akiwa masikini na mnyenyekevu, aliye zaliwa katika zizi na wazazi maskini sana ambao wasingeweza kulipa gharama ya chumba cha kulala wageni. La hasha, walitaka mfalme ambaye angeliwaokoa kutoka kwenye utumwa na utawala waliouchukia wa Warumi.

Walikosea kumtafuta Masiha, hivyo alipokuja hawakuweza kumtambua.

Lakini sio kwamba kila mtu hakumfahamu.

### *Baadhi Walimtafuta Mfalme wa Kweli*

Kwa wachungaji wanyenyekevu, malaika alitokea na kutangaza kuzaliwa kwa Kristo. Wakiwa wamejawa na kicho, wachungaji walisafiri kwenda kumwona Mfalme aliyezaliwa. Mamajusi kutoka mashariki waliona nyota tukufu angani usiku wakaifuata hadi mahali alipozaliwa Kristo na kumwabudu.

Na katika maisha yake yote katika dunia hii wanyenyekevu wachache waliomwamini Yesu na kumfuata. Wazazi wake, Yohana Mbatizaji, na wengi waliyokubali mahubiri yake, kama vile Mariamu, Martha, na Lazaro na hata wanafunzi kumi na wawili. Watu wasio na idadi wenye mioyo ya uaminifu katika Israeli waliosikia mafundisho ya Yesu, waliona miujiza yake na kujitoa wenyewe kwa ushawishi wa Roho Mtakatifu – hawa pia walichukua nafasi katika ukoo usiokatika wa waaminifu. Wakati ambapo maisha na huduma ya Yesu vilipofika katika kilele cha malengo yake, Ijumaa moja yenye giza katika

msalaba wenye sura mbaya sana, sio wote katika kundi la wenye wazimu walipenda kifo chake. Simeoni Mkrene alibeba msalaba wa Yesu, na hatua zake zilimpeleka katika upande sahihi, wa kweli na wa wokovu. Askari wa Kirumi alichagua upande gani wa kujiunga. Kwa upande mwingine wa Yesu, mwizi alifanya uchaguzi huo huo – kama wengi walivyofanya katika kundi lenye ghasia chini ya msalaba.

Ni nani awezaye kujua hasa, ni watu wangapi (isipokuwa Mungu) walifanya uchaguzi kumpokea Kristo wakati wa maisha yake hapa duniani? Naamini siku moja tutafahamu – na bila shaka tutashangazwa tutakapofahamu.

Yesu alipomaliza na kukamilisha kile kilichomleta hapa duniani, Biblia inasema kwamba alipaa kurudi mbinguni, kukaa mkono wa kuume wa Mungu Baba. Lakini kabla hajaondoka hapa duniani alianzisha aina ya Israeli mpya na tofauti na ile ya taifa moja, alifungua taifa hili jipya la kiroho la Israeli kwa kila mtu, akimwalika kila mwanaume, mwanamke, na mtoto kumfuata.

Yesu alianzisha kanisa lake – lenye wafuasi wake wale waliobeba jina lake – hawa walijulikana kama Wakristo. Kwa kupitia kanisa lake, Yesu angehakikisha na kuendeleza ukoo wa waaminifu katika siku za baadaye. Kanisa lake lingeendelea kutoka kupaa kwake hadi kurudi kwake mara ya pili.

Kanisa lilianza na mafanikio makuu sana. Maelfu waliongolewa kwa siku, ukweli na upendo wa Yesu ulienea ulimwenguni kama moto wa msituni. Lakini kama ilivyokuwa kwa Israeli, kanisa pia lilipingwa na Shetani.

Mafundisho ya uongo yalipenyezwa. Kanisa lilifanya maafikiano na ulimwengu ulilolizunguka. Liliingia katika uasi, kuabudu sanamu na mafundisho ya uongo mpaka tena waaminifu wachache walipatikana ndani ya kanisa. Inasikitisha sana – hata kuhuzunisha, unapopitia upya historia ya Israeli na kuona jinsi walivyoshindwa katika kutimiza kusudi la pekee la Mungu. Inaweza pia kuwa jambo la kusikitisha sana kujifunza historia ya Israeli ya pili ambalo ni kanisa lake, na kufuatilia kuasi wake wa mara kwa mara kutoka kwenye kusudi la Mungu.

Lakini zingatia sana: Wakati wa giza kuu zaidi – wakati wa maasi makuu – daima kulikuwa na waaminifu wachache katika Israeli ambao walikuwa hawajampigia magoti Baali. Na historia ya kanisa inahakikisha kwamba katika uasi mkuu zaidi, daima kumekuwepo, waaminifu wachache waliomfuata Yesu kwa imani isiyoweza kutikiswa.

Hebu sasa turudi nyuma katika kuzaliwa kwa kanisa la kikristo na kufuata njia yake hadi karne yake ya awali. Na tukigundua – kama tutakavyo gundua – kwamba mara tu baada ya kuanzishwa, kanisa katika mfululizo wa wakati lilianguka na kulalia upande wa uasi, halafu badala ya kuomboleza kwa ajili ya mkasa huo, hebu tugundue na kusherekea waaminifu wachache waliosimama thabiti katika upande sahihi, kwa namna iwayo yote. Kwa sababu hawa ni babu zetu wa kiroho. Watu hawa ni viungo thabiti katika mfululizo usiokatika ambapo sisi pia tunaweza kuwa viungo.

Kama unavyosoma maneno haya watu wote wa

ulimwenguni karibu bilioni 6.5, wako upande mmoja wa pambano kuu au upande mwingine. Kwa kuchagua au kwa kushindwa kuchagua, jambo la kuhuzunisha ni kundi kubwa wanachagua upande mbaya. Bali Mungu ana waaminifu wake hata katika wakati huu. Wanao mpenda kwa ari kuu. Hawa watasimama kwa ajili ya kweli yake na kutetea tabia yake hadi pumzi yao ya mwisho.

Je, umechagua – bila kuangalia nyuma – uko upande gani katika pambano kuu hili? Kama siyo, kwa nini usubiri – kwa nini usifanye leo ndiyo siku ya kufanya uamuzi?

Na kama umeshafanya uamuzi wa kumpokea Yesu, leo inaweza kuwa siku nyingine ya kuitangazia dunia na ulimwengu wote kwa uhakika juu ya upande unaosimama.

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 6

# Mlipuko Wa Moto

Nilipokuwa kijana mdogo, wakati wa kiangazi nilikuwa ninafanya kazi katika misitu ya Oregon – kaskazini magharibi ya bahari ya Pacific ya Marekani – kazi ya kukata miti kwa ajili ya mbao. Siku moja wakati wa majira ya kiangazi, ilikuwa ni mchana wenye joto kali la mwezi wa nane. Kama futi hamsini kutoka niliposimama kamba iliyotengenezwa kwa waya ulikatika na kugonga mwamba. Mara moja kulikuwa na mlipuko wa cheche za moto zilizo kwenda kwenye nyasi kavu chini ya msitu. Mara moja miali ya moto ililipuka, halafu ghafla moto ukaenea kila upande.

Nikakimbia, nikararua kofia na fulana nikijaribu kuvitumia kupungia moto ili uzimike bila mafanikio yoyote. Moto ulikuwa tayari umesonga mbele na kufanya mduara mpana ambao usingeweza kuzimishwa.

Kazi ya kukata miti kwa ajili ya mbao ilisitishwa huku, wafanyakazi wote wakijaribu walivyoweza kuuzima moto, lakini kulikuwa na joto kali sana siku hiyo, nyasi zilikuwa zimekauka sana na miti pia ilikuwa imekauka sana. Kufikia jioni ndege kubwa zilidondosha zana za kuzimia moto toka angani katika moto ambao sasa ulikuwa umeshashambulia ekari mia moja kadhaa. Ilichukua siku kadhaa kabla moto dhibitiwa kabisa.

Tangu siku hiyo na kuendelea, siwezi kufikiria Pentekosti bila kukumbuka ule mlipuko wa moto katika milima ya Oregon.

Yesu alitumia miaka mitatu na nusu katika kutoa huduma akiwa hapa duniani. Hakujaribu kufundisha injili kwa watu wake wateule, Waisraeli, hakujaribu kuwafundisha injili watu wasioamini, wapagani. Naam, kando kando ya bahari na kando ya mlima, aliwaambia mifano – visa rahisi vilivyowasaidia watu kuelewa ufalme wake wa kiroho. Lakini hakufanya mikutano ya kiuinjilisti, hakwenda huku na huko kama amepagawa kwa ajili ya kuuvuta ulimwengu, hakufanya miujiza kwa ajili ya kumfikia kila mtu duniani kwa ujumbe wake wa upendo na neema.

Badala yake, Yesu alijimimina mwenyewe kwa wanafunzi wake, watu wanyenyekevu kumi na wawili waliomtumainia kiasi cha kuacha makazi yao na kumfuata, wakijifunza juu yake – zaidi kidogo ya miaka mitatu. Walimfuata alipokuwa akitoa huduma yake, kwa kadri alivyowaponya vilema na vipofu, kwa kadri alivyowaambia ukweli kuhusu Mungu, alieleza jinsi upendo unavyofanana kwa ukaribu zaidi.

Aliweka chembe chembe ya moto kwa kila mmojawapo wa wanafunzi kumi na wawili. Lakini mioyo hiyo ilikuwa bado haijakauka na kuwa na kiu ya kutosha kulipuka katika miali ya moto. Walikuwa kama miti mibichi, haijakauka. Kwa kadri huduma ya Yesu ilipofikia kilele chake katika msalaba, mmoja wa wanafunzi wake alimsaliti, mwingine

alimkataa.

Bali wakati huo, upendo mkuu uliwaka ndani ya mioyo yao yote isipokuwa mmoja. Yesu alipofufuka baada ya siku tatu katika wafu, miale ya moto iliwaka zaidi ndani ya mioyo yao. Baadaye alipaa mbinguni akawaacha wanafunzi wake. Bali kabla hajapaa, aliwaambia atamtuma Roho Mtakatifu awe nao.

Hii ndiyo sababu walikusanyika pamoja kwa muda katika chumba cha ghorofani kwa muda wa siku kumi wakiomba na kusafisha mioyo yao ili kuutoa uchoyo unayozimisha ule moto. Walitafuta ahadi ya Roho Mtakatifu na kusubiri.

Mara ghafla... "kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukatokea ndimi zilizogawanyika kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama roho alivyowajalia kutamka" – Matendo 2:2-4.

*Pentekosti!*

Moto uliokuwa umewaka ndani ya mioyo yao kila wakati zaidi ya miaka mitatu uliungana na moto wa ndimi juu yao. Wote tunajua upepo wenye nguvu unavyofanya kwenye moto. Wafuasi wa Kristo waliwaka moto kwa nguvu na shauku ya upendo halisi – wakateketea katika kimbunga cha ari, haraka na azimio lisiloweza kuzimishwa la kuuvuta ulimwengu kwa Bwana na Mwokozi wao aliyefufuka. Waliposhuka kutoka kwenye chumba cha ghorofani;

Petro alisema kwa ajili ya wote, akihubiri kwa msukumo wa nguvu ya Roho Mtakatifu, alipomaliza watu elfu tatu walimkubali Kristo na kubatizwa.

Kanisa la Kikristo lilizaliwa. Na msukumo wake ulikumba ulimwengu wote kwa haraka sana na nguvu nyingi kiasi kwamba kabla ya muda mrefu, baadhi ya watu waliopinga waumini walilalamika kwamba "watu hawa walipindua ulimwengu" – Matendo 17:6.

Inaonekana kwamba kanisa la Kristo – Israeli mpya ya Kristo – lilikuwa limekusudia kuendelea kwa haraka kuuvuta ulimwengu wote kwa Kristo kwa nguvu ya sumaku ya upendo na ukweli wa Kristo. Kwasababu ya upendo wa Kristo – kama kielelezo cha Kristo cha kutokuwa na maisha ya ubinafsi na kafara ya kifo chake – ilikuwa na uwezo wa kufanya kile ambacho hakuna uwezo mwingine unaoweza kufanya hivyo. Iliyeyusha mioyo. Iliharibu mapenzi binafsi na kufanya kiburi kionekane kama kitu kibaya. Na ukweli wa Kristo – kama alivyofundisha na kuishi – ulifunua uongo wa Shetani ulivyo na kumwinua juu Mungu Baba aliyedhamiria kuwarejesha tena watoto wake walio asi kwake.

### *Imara kama kiini cha Mwali wa Moto*

Kumbuka, moto wa Pentekoste haukuwa moto usozimika wakimsisimko usiorekebishwa, au kama urembo mrefu, wimbi kubwa la maji au mwale wa njano wa tochi mpya. La hasha, ulikuwa kama moto wa tochi ambayo imerekebishwa ili mwale wake imara inayolenga nguvu

ya kiini cha tochi yenye betri mpya. Ule mwale wa moto mweupe wa Pentekoste ulikuwa ni matokeo ya kuja kwa Mungu kwa ajili ya kuwajaza walio kubali na nafsi yake. Na kwa vile Mungu ni upendo, kila muumini amekuwa ni mwenge wa upendo wa kuwashia moto toka kwa mtu mmoja hadi mwingine, ukianzisha mfululizo kutoka nyumba moja hadi nyingine, mji hadi mji, na mkoa hadi mkoa.

Na kumbuka pia kwamba moto wa upendo wa Mungu sio sawa na upendo wa kawaida unaosheherekewa katika wimbo, shairi na mchezo wa kuigiza hapa duniani.

Upendo wa Mungu hautoi ili kupata.

Sio pupa ya msisimko.

Hauishi hata kama mambo yanapokuwa magumu – wakati msisimko umekwisha.

Upendo wa Mungu ulionekana wazi zaidi katika msalaba: Kafara kamili ya kujitoa, siyo kwa watu waliostahili, bali kwa watu walio wahitaji. Mungu aliwapenda watu aliowaumba licha ya uasi wao, licha ya nia yao ya kumwangamiza. Aliwapenda kwa sababu aliwaumba. Walikuwa wake – na angetoa uhai wake mwenyewe ili kuwaokoa.

### *Shambulizi*

Angamizo kamili la Shetani lilitiwa muhuri msalabani. Lisingeweza kubadilishwa tena, angeshindwa katika pambano kuu kati yake yeye mwenyewe na Kristo. Kama alitamani kuwa taifa kubwa, ulimwenguni , nguvu yake

sasa ilikuwa imehifadhiwa kabisa. Alikuwa sasa ni mpinzani aliyejeruhiwa kabisa – adui mlemavu.

Lakini kwa kadri alivyoendelea kuwa hai na kupumua, angeendelea kumpinga Kristo na watu wake – kanisa. Angetumia nguvu zake zote za ubinafsi na uongo na kufanya kila anachoweza kuliharibu kanisa changa linalokua kwa haraka.

Kwa watu wenye macho ya kuona na masikio ya kusikia, mashambulizi ya Shetani hayakuwa ya kushangaza. Paulo alipoendeleza huduma yake, kwanza kwa Wayahudi walioongoka halafu kwa wapagani pia, alitoa onyo hili: "Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu, mbwa mwitu wakali wataingia kwenu wasilihurumie kundi, tena kati yenu ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao. Kwa hiyo kesheni mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi" – Matendo 20:29-31.

Shetani angelishambulia kanisa changa kutoka nje – na kutoka ndani. Kutoka nje mbwa mwitu wakatili wangekuja kushambulia kundi. Kutoka ndani, watu wangeinuka kusema mambo mapotovu.

Mambo mapotovu?

Paulo anafafanua katika barua nyingine kwa kanisa: "Maana utakuja wakati watakapo yakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia walimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na

kuzigeukia hadithi za uongo" – 2 Timotheo 4:3, 4.

Mafundisho ya kweli dhidi ya mafundisho ya kubuni Ukweli dhidi ya uongo.

Pambano kati ya ukweli na uongo – kati ya mafundisho ya ukweli na mafundisho ya kubuni – yalikuwa wazi sana katika kanisa fulani ambalo Paulo aliingilia na kukemea kwa maneno ya Nguvu sana: "Ninastaajabu", Paulo aliandika, "kuwa mnaacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawatabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri, kinyume na tulivyo tangulia kusema hapo kwanza, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa na sema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mlioipokea, na alaaniwe" – Wagalatia 1:6-8.

Paulo alisisitiza maonyo yake kwa nguvu juu ya mafundisho ya uongo yaliyoibuka kutoka ndani ya kanisa kwa kueleza mambo ambayo wachache wenye macho wangeona. "Maana ile siri ya kuasi," alisema, "hivi sasa inatenda kazi; lakini yuko azuiaye sasa hata atakapoondolewa" – 2 Wathesalonike 2:7.

Hivyo hata baada ya msalaba, Shetani anaendeleza vita yake dhidi ya Kristo. Hawakuweza kuachia ngazi. Alishambulia tabia ya Mungu, sheria yake, ukweli wake, injili yake, kanisa lake na watu wake.

Kutoka kwa Adamu hadi Nuhu, Nuhu hadi Ibrahimu, Ibrahimu hadi Kristo, – daima kumekuwa na wale

waliokuwa waaminifu wa Mungu na ukweli wake. Wakati fulani walikuwa wengi na wakati fulani (kama wakati wa Nuhu kipindi cha gharika) walikuwa wachache sana kiasi cha watu nane dunia nzima. Hata kama wakiwa wanane kama wakati wa gharika au elfu tatu au zaidi wakati wa Pentekoste, mfululizo wa waaminifu usiokatika umeendelea kuwepo siku zote.

Nani ajuaye idadi ya waamini wa kweli waliomfuata Kristo katika kilele cha mafanikio ya kanisa la awali? Pengine ni mamilioni? Tunachojua tu ni kwamba, kama Paulo alivyoonya hapo awali, adui mkuu angeinuka mwenyewe kuongeza nguvu zaidi ya kushambulia wateule wa Mungu. Angetumia vyote viwili mateso kutoka nje ya kanisa, mafundisho ya uongo na maafikiano ya kutoka ndani kufanya uovu wake.

Historia yote ya kanisa la Kikristo – kutoka pentekoste hadi kuja kwa Yesu mara ya pili kumeelezwa katika kitabu cha Ufunuo. Sura tatu za awali zina ujumbe kwa makanisa saba. Makanisa saba ni mwendelezo hasa wa kanisa isipokuwa katika nyakati tofauti tofauti za historia. Mwanzo na mwisho kamili wa tarehe ya makanisa hayo hayawezi kutajwa kwa uhakika kabisa – kuna tofauti hata kati ya wasomaji wa Biblia (kati ya msomi mmoja na mwingine). Lakini kwa ujumla, hii ni orodha ya makanisa saba na makisio ya nyakati zake katika historia.

| | |
|---|---|
| Efeso | pentekoste hadi kufikia 100 B.K. |
| Smirna | 100 B.K. hadi kufikia 313 B.K. |

| | |
|---|---|
| Pergamo | 313 B.K. hadi kufikia 538 B.K. |
| Thiatira | 538 B.K. hadi kufikia 1517 B.K. |
| Sardi | 1517 B.K. hadi kufikia 1798 B.K. |
| Filadelfia | 1798 B.K. hadi kufikia 1844 B.K. |
| Loadikia | 1844 B.K. hadi mwisho wa wakati |

Katika sura zilizobaki za kitabu hiki, tutafuatilia historia ya watu wa Mungu katika kila kipindi cha vipindi hivyo vya nyakati – chini ya alama za makanisa hayo saba. Sura yetu inayofuata tutazingatia makanisa hayo matatu ya awali kati ya hayo makanisa saba: Efeso, Smirna na Pergamo.

Kutoka hapo tutalifuata kanisa kupitia barabara ndefu ya kipindi cha giza, chini ya alama ya Thiatira. Kanisa la matengenezo linafuatia, chini ya alama ya Sardi. Kutoka kwenye matengenezo hadi mwaka 1844, tumegundua kanisa likiingia kile kinachojulikana kihistoria kama mwamko mkuu wa marejeo" – kanisa la Filadelfia.

Katika mwaka 1844, tunakuta kuinuka kwa masalio – na sura ya mwisho ya kitabu hiki itazingatia umuhimu wa kanisa hilo la masalio. Sura hizi zitakuwa za kuvutia sana na za muhimu kwako na kwangu – kwa sababu zinatuhusu SISI! Ni juu ya upendeleo wetu na wajibu wa kuendeleza ukoo usiokatika wa waaminifu. Ni juu ya vile Mungu anavyotaka kututumia katika maisha yetu kuwarejesha waasi kwake. Ni juu ya kujua kwamba sisi ni nani na kwa nini tupo hapa.

Kuna uhusiano endelevu kati ya Adamu na wewe - na mimi. Hapa katikati, kwa muda wa miaka elfu sita au zaidi,

Mungu amekuwa akiuendeleza mfululizo wa waaminifu. Ninataka kuwa kiungo thabiti ambacho wengine wanaweza kuijunga na kuendeleza zaidi mfululizo huo, mpaka hapo pambano kuu litakapomalizika.

Na litaisha rafiki yangu.

Mapema – bali bado.

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 7

# Leta Mvua

Kama kweli aliwasha moto, historia haiwezi kuelezea kinaganaga. Lakini historia inadhihirisha kwamba alikubali lawama za mwanzo.

Hadi wakati huo, alikuwa na kisingizio.

Wakati kimbunga cha moto kilipofagia jiji la Roma katika mwaka 64 B.K., na kubakia wilaya nne tu kati ya wilaya kumi na nne, tetesi zilienea kwa raia kwamba mfalme mwenyewe – Nero (aliyetawala kutoka mwaka 54 hadi 68 B.K.) – ndiye alichoma jiji moto. Tetesi pia zilienea katika juma ambalo moto ulikuwa ukiendelea, Nero alipiga kinubi chake na kuimba kutoka juu ya kilele cha mlima wakati jiji linawaka moto. Kwa muda wa miaka mingi haya yalikuwa ni maandishi katika hekaya kwamba Nero alipiga fidla (chombo cha muziki) wakati jiji la Roma linaungua – sio hakika, kwa vile fidla ilikuwa bado haijagunduliwa.

Unapoangalia upande mwingine wa tuhuma zisizokubaliwa za umma, Nero aliwashutumu Wakristo waliokuwa wakiishi jijini. Mwana historia mrumi Tacitus aliandika maneno yafuatayo kuhusu shutuma ya Nero:

> "Na hivyo kuondoa tetesi hizi, Nero alifanya njama za kuwatafuta wakosaji na kuwaadhibu na kundi la wadhalimu wakuu waliwachukia kwa machukizo yao,

waliojulikana kama Wakristo. Visingizio vya Nero vilikuwa ni uchaguzi mkamilifu kwasababu kwa muda kitambo uliondoa shinikizo za tetesi mbali mbali zilizokuwa zikiendelea katika jiji la Roma."

Machukizo yao? Kwa nini alifanya ukatili dhidi ya Wakristo hawa wa awali?

Kama vile madai ya uongo yalivyo sababisha kifo cha Yesu Kristo – mwasisi wa kanisa –hivyo tu, uongo wa namna hiyo hiyo ungeenea juu ya wafuasi wake. Katika pambano kuu dhidi ya wema na uovu, dhidi ya Kristo na Shetani, Yesu alishinda vita dhidi ya uongo wa Shetani katika msalaba wa Kalivari, maangamizi kamili ya Shetani yaliwekwa muhuri wakati Yesu aliposema kwa sauti kuu "Imekwisha."

Ingawa maangamizo kamili ya Shetani yalikamilika katika Ijumaa ya utusiutusi masuala mengine katika ushindani kati ya aliyekuwa malaika mkuu mbinguni na mwumbaji wake yalikuwa bado hayajakamilika. Maswali juu ya haki ya Mungu, kuhusu sheria yake, utawala wake, na tabia yake yalipaswa yajibiwe kikamilifu.

Yesu alipotembea katika barabara ya Palestina Shetani aliamsha kila aina ya uongo dhidi yake. Mara Yesu aliporudi kwa upande wa Baba yake mbinguni, Shetani aliendeleza vita vyake dhidi ya wafuasi wa Yesu duniani.

Tetesi zilienea kuhusu moto wa Roma. Zoezi la meza ya Bwana lilisababisha madai ya uongo juu ya kafara ya binadamu na ulaji wa watu. Pumziko la Sabato lilisababisha madai ya uvivu. Wakristo walisemwa kuhusika katika

kufanya karamu ya ulafi na tabia nyingine potovu.

Hivyo Nero alipoondoa tetesi kwa ajili ya moto mkuu kutoka kwake na kupeleka kwa Wakristo, lilikuwa ni jambo lililo kubalika kwa urahisi sana. Wanahistoria wa kipindi hicho wanatoa taarifa kwamba mateso yaliyofuata hayakusababishwa sana na lawama za uchomaji wa jiji, kama wazo la kwamba, Wakristo walikuwa maadui wa wanadamu lilivyoenea.

Na mateso yalikuwa ya kutisha sana.

Tacitus tena anasema: "Wakiwa wamefunikwa na ngozi za wanyama, waliraruriwa na mbwa na kuangamizwa, au waliwambwa msalabani au waliangamizwa kwa miale ya moto wakitumika kama taa usiku, wakati mwanga wa mchana umetoweka.

Wakristo walichomwa wakiwa hai na kugeuzwa kuwa kama tochi kwa ajili ya kutoa mwangu wakati wa usiku. Wengine wao walisulubishwa, na wengine kung'atwa na mbwa wakali walio waumiza sana hadi kufa. Naam, inatisha sana.

"Nguvu za dunia na jahanamu," Ellen White aliandika, "Walijipanga wenyewe kama askari tayari kwa ajili ya vita dhidi ya Kristo katika nafsi ya wafuasi wake. Upagani uliona mbele kama ikiwa injili itashinda, mahekalu na mimbari zake zitafutiliwa mbali; hivyo ulikusanya nguvu zake kwa kuangamiza Ukristo" – *The Great Controversy,* uk. 39.

"Kutoka katika mlima wa Mizeituni Mwokozi alitazama vimbunga vikiwa tayari kuangukia kanisa la kitume,

na kupenyeza zaidi katika siku za mbeleni, macho yake yalifahamu ukatili, dhoruba mbaya ambazo zilikuwa tayari kuwapiga wafuasi wake katika vipindi vya giza kuu na mateso" – *The Great Controversy,* uk. 39.

Katika mlima wa Mizeituni Yesu alisema maneno haya:

"Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawaua, nanyi mtakuwa watu wakuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya jina langu" – Mathayo 24:9.

Mateso ya hao Wakristo waaminifu hayakuishia wakati wa Nero bali yaliendelea kwa karne kadhaa. Historia inatoa taarifa ya angalau mateso makuu kumi ya Wakristo ambayo yalianza chini ya Nero na kuendelezwa chini ya warithi wake (walioshika madaraka baada yake).

- Nero (64 B.K.)
- Domitian (c. 90 – 96)
- Teajan (98 – 117)
- Hadrian (177 – 138)
- Marcus Aurelius (161 – 181)
- Septimus Severus (202 – 211)
- Maximus Thracian (235 – 251)
- Dacuis (249 – 251)
- Valerian (257 – 260)
- Diocletia/ Galerius (303 – 311)

"Mateso haya yalianza chini ya Nero wakati wa mauaji ya kidini ya Paulo, yaliendelea kwa ghadhabu kuu au kidogo

> kwa karne kadhaa. Wakristo walishitakiwa kwa uzushi kuwa ni wahalifu wakuu sana na kutangazwa kwamba wao ndio chanzo cha maafa makuu –njaa, magonjwa ya kutisha na tetemeko la ardhi. Kwa kadri walivyokuwa kusudi la uhasama na tetesi za umma, waandishi walisimama tayari kwa ajili ya faida, kuwasaliti watu wasio na hatia. Walihukumiwa kama waasi dhidi ya ufalme, kama maadui wa dini, na kama wanyama waharifu wa jamii. Idadi kubwa walitupwa kwa wanyama mwitu au kuchomwa wakiwa hai katika majumba ya maonyesho. Wengine walisulubishwa, wengine walivikwa ngozi ya wanyama pori na kutupwa katika viwanja ili kularuriwa na mbwa. Adhabu zao mara nyingi zilifanywa burudani kuu za sherehe ya kuchangisha fedha kwa ajili ya shughuli maalum hadharani. Kundi kubwa lilikusanyika kufurahia na kuwapa salamu za dhihaka wale waliokuwa wanakufa kwa mateso haya makubwa huku wakicheka na kushangilia kwa makofi" – *The Great Controversy*, p. 40.

Kwa hawa waaminifu, Biblia inasema: wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani; wakipigwa na mawe, wakikatwa na misumeno, wakijaribiwa wakizunguka zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa vibaya; (watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na milima na katika mashimo na mapango ya nchi" – Waebrania 11:36-38.

Nini kilikuwa matokeo ya mateso haya yasiyokoma? Je,

mateso yalifanikiwa kuwakatisha tamaa hawa Wakristo wa awali? Je, Wakristo walikata tamaa na kusema utisho huu ni mkuu zaidi? Je, walivunjika mioyo na hatimaye kukata tamaa?

> "Bila mafanikio nguvu za Shetani zilitumika katika kuliangamiza kanisa la Kristo kwa mateso.... Kwa kushindwa walishinda" – *The Great Controversy,* uk. 41.

### *"Damu ya Wakristo ni Mbegu"*

"Kama Tertullian alivyoandika, "Mnavyoendelea kutufyeka, ndivyo idadi yetu inavyoongezeka; damu ya wakristo ni mbegu."

Kile alichokua akijaribu Shetani kilikuwa hakifanyi kazi vizuri. Shetani – adui yetu mkubwa, siyo mjinga! Kipawa cha uwezo wa kiakili alibarikiwa nacho katika uumbaji hakikuisha wakati alianguka kwa ajili ya kiburi. Bali yeye alielekeza tu uwezo wake wa kiakili katika uasi.

Kwa wazi kabisa, ilikuwa ni wakati wa badiliko kamili la mbinu.

> "Adui mkuu sasa alijitahidi kupata kwa ulaghai kile alichoshindwa kupata kwa nguvu. Mateso yalikoma, na badala yake aliweka vivutio vya hatari vya mafanikio ya muda na heshima za kidunia. Ibada ya sanamu ziliongoza kupokea sehemu ya imani ya Kikristo wakati ukweli mwingine muhimu ulikataliwa. Walikiri kumkubali Yesu kama Mwana wa Mungu na kuamini kifo chake na ufufuko wake, bali hawakujiona kuwa na hatia ya dhambi na hivyo

hawakuona haja ya kuungama na kubadilika katika mioyo yao. Kwa sehemu ya makubaliano yao walipendekeza kwamba Wakristo wanapaswa waunganike katika jukwaa la kumwamini Kristo.

"Sasa kanisa lilikuwa kwenye hatari kuu ya woga. Gereza, mateso na moto na upanga vilikuwa na mibaraka ukilinganisha na hali hii. Baadhi ya Wakristo walisimama imara wakijitangaza kwamba hawatafanya maafikiano na uasi huo. Baadhi walikuwa tayari kukubali au kufanya marekebisho ya baadhi ya mambo katika imani zao na kuunganika na wale waliokuwa wamekubali Ukristo kiasi fulani alisema kwamba hii inaweza kuwa ni njia ya wongofu wao kamili. Huu ulikuwa ni wakati wa uchungu mkuu kwa wafuasi waaminifu wa Kristo, chini ya joho la Ukristo wa kujifanya, Shetani alikuwa akijipenyeza mwenyewe ndani ya kanisa, kuvuruga imani zao na kugeuza mawazo yao kutoka kwenye neno la kweli.

"Hatimaye Wakristo wengi waliridhia kushusha viwango vyao vya Ukristo na mwungano baina ya Ukristo na upagani uliundwa" – *The Great Controversy*, pp. 42, 43.

Mateso yalishindwa. Je, makubaliano yalifanikiwa? Hapa kwa kiasi kikuu adui alifanikiwa.

Chini ya alama za makanisa saba, kitabu cha ufunuo kinafuatilia historia nzima ya kanisa la Kikristo kutoka katika mwanzo wake hadi kurudi kwa Mwasisi wake. Ingawa, kama ilivyoelezwa katika sura iliyotangulia,

uhakika wa tarehe ya mwanzo na mwisho wa kila kanisa unatofautiana kutoka kwa msomi mmoja wa Biblia na mwingine, makisio ya wakati wa vipindi vya makanisa matatu ya awali ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Efeso | Pentekoste hadi 100 B.K. |
| Smirna | 100 B.K. hadi 313 B.K. |
| Pergamo | 313 B.K. hadi 538 B.K. |

### *Efeso*

Zingatia sasa ujumbe ambao Mungu anatuma kwa Efeso, kanisa la kwanza kati ya makanisa saba:

> "Kwa malaika wa kanisa liliko Efeso andika haya ndiyo anenaye yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu. Nayajua matendo yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio ukawaona kuwa waongo, tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya jina langu, wala hukuchoka. Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeacha upendo wako wa kwanza. Basi, kumbuka ni wapi ulipoanguka ukatubu. Ukafanya matendo ya kwanza. Lakini usipofanya hivyo naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake usipotubu" – Ufunuo 2:1-5.

Ni nje ya uwezo kwa kisa tunachosimulia katika kitabu hiki kueleza kwa undani kila neno na kifungu cha maneno ya ujumbe uliotolewa kwa makanisa saba. Bali kumbuka sana kuhusu ujumbe wa kwanza: Mungu anatambua

"matendo" na "subira" ya wakristo hawa wa mwanzo kabisa.

Waliongozwa na upendo kwa ajili ya kiongozi wao zaidi ya kifo kilicho wakabili, hawa wakristo wa awali walivumilia mateso ya kutisha sana yasiyoweza kufikirika. Walikuwa waaminifu na wanyenyekevu, bila kujali ni gharama gani wangelipa.

Kwa kadri muda ulivyoendelea, wengine walianza kutetereka. Wengine walianza kupoteza uhusiano na Kiongozi wao "Yesu". Wengine walianza kuona uhusiano wao na Yesu kuwa kitu cha kawaida.

Inatokea mara kwa mara. Maarusi, katika moto wa upendo wa awali, wanaweza kufanya kila kitu kwa ajili ya mwenzake – hata kufa – kama hiyo ingekuwa ni lazima. Lakini kadri muda unavyoendelea, dhiki zinazo wazunguka au hata kutokuwa waangalifu, vyote hivi vinaweza kuleta mabadiliko kidogo kidogo katika upendo, kiasi kwamba huwezi hata kugundua. Upendo wa kwanza unakufa na unaendelea kuwa makaa ya moto – au na hatimaye kupoa na kuwa majivu.

Pengine si jambo la kawaida kwa shauku na msukumo wa nguvu wa upendo wa kwanza kuendelea bila mwisho. Katika ndoa nzuri, pamoja na matatizo yanayo izunguka, mwishoni inageuka kuwa– imara zaidi, muungano wenye mizizi iliyokomaa katika kushukuru, kujitoa na zaidi ya yote upendo wenye moto wa mahaba uliowasha moto wa upendo wao wa kwanza.

Lakini jambo la kusikitisha, "upendo wa kwanza mara

nyingi unatoa nafasi kwa uchoshi, harara na hali ya kutojali, unaacha tu makaa yaliyokufa ya upendo uliokuwepo wakati fulani."

Kwa kanisa la Efeso, Mungu anasema: "Umeacha upendo wako wa kwanza. Tubu na ufanye matendo ya kwanza." Mahusiano mengi yaliyoharibika yanaweza kuokolewa ikiwa wenzi wataanza tena kufanya mambo waliyofanya awali pasipo haja ya kushurutishwa.

Ingawa kwa kukisia mwaka 100 B.K. – ni mwisho mwa wakati wa kipindi cha kanisa la Efeso – mateso yalikuwa tayari yameanza, Mwanzilishi wa kanisa aliona ulazima wa kutoa maonyo kwamba ingawa wengine walibaki imara hata kufa wengine walikuwa wanaruhusu ridhaa ya kubadili upendo wa kwanza wenye shauku.

Mwanzilishi wa kanisa (Yesu) alijua kwamba wafuasi wake wasingevumilia kama bila uangalifu wangekubali hili kutokea. Tubuni rejeeni, rudisheni ari ya mwanzo. Aliwasihi! Wangehitaji sana huo upendo wa kwanza, kwa vile kanisa la Smirna lilikuwa linafuata karibu.

### *Smirna*

Smirna ilikuwa kanisa la pili, kuanzia mwaka 100 B.K. hadi 313 B.K. – hili ni kanisa lililokuwepo wakati wa kipindi cha mateso makali zaidi. Barua ya Mungu kwa Smirna ni barua pekee isiyo na kemeo kati ya makanisa saba.

> "Na kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna andika;
> Haya ndiyo anenayo yeye aliye wa kwanza na mwisho,

> aliyekuwa amekufa na sasa yuko hai. Naijua dhiki yako na umasikini wako, (lakini u tajiri) najua na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali sinagogi la Shetani. Usiogope mambo yatakayokupata, tazama huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwanifu hatakufa, nami nitakupa taji ya uzima" – Ufunuo 2: 8-10.

Kwa wale ambao wangekabili kifo kwa ajili ya imani yao, ni wazi kwamba ilikuwa ni lazima kwamba walifarijiwa na kutiwa nguvu kwa kukumbushwa kwamba Bwana wao "alikufa na kufufuka." Hivyo na wao wangekufa na kufufuka kama Bwana wao.

Ninajua, alisema Kiongozi wao, kile ambacho mnakaribia kukikabili. Ninajua ya kwamba wengine wenu watafungwa gerezani kwa ajili ya uaminifu wenu. Baadhi yenu mtakufa. Bali msiogope. Kama mkiwa waaminifu hata kufa, nitawapa taji ya uzima.

Alichosema Yesu kwa kanisa la Smirna ni kweli kwa kanisa la siku za mwisho kabisa. Mara tu kabla ya kuja kwa Kristo mara ya pili, baadhi ya wafuasi wake tena watakabili kifo kwa ajili ya imani zao. Hii inawezekana ikatokea kwetu sisi tunaoishi katika kipindi hiki. Ahadi ya taji ya uzima walio ahidiwa kanisa la Smirna, ni kwa ajili ya wale wanaoishi katika wakati wa mwisho pia.

"Nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi, Mungu anasema. Ingawa kweli kwamba mateso yaliendelea mara kwa mara wakati wote wa karne ya kwanza katika utawala wa

wafalme mbalimbali wa kirumi, inakubaliwa zaidi kwamba kipindi kilichokuwa cha umwagaji damu zaidi kuliko vyote, kilichukua muda wa miaka kumi, kutoka mwaka 303 hadi 313 B.K., chini ya mfalme Diocletian. Kwa kutumia kanuni ya mwaka mmoja-kwa-siku moja ya kufafanua unabii wa Biblia (angalia Hesabu 14:34, Ezekieli 4:6), siku kumi zingekuwa sawa na miaka kumi.

### *Pergamo*

Tumefika sasa kwenye kanisa linawakilisha ubadilishaji wa mbinu wa Shetani kutoka mateso kwenda kwenye kuafikiana. Kutoka mwaka 313 hadi 538 B.K., upagani na Ukristo ulikuwa sana na kuunganika kuwa kitu kimoja. Na wakati huu, kanisa la kirumi lilitawala Ukristo, liliongoza katika matendo na mafundisho ambayo hayakufahamika na kanisa la awali. Hatimaye, mstari unaotenganisha kanisa na serikali uliendelea kuwa na ukungu zaidi.

> “Na kwa malaika wa kanisa lililoko pergamo andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye na upanga mkali, wenye makali kuwili. Napajua ukaapo, ndipo penye kiti cha enzi cha Shetani; nawe walishika sana jina langu, wala hukuikana imani yangu, hata katika siku za Antipa shahidi wangu, mwaminifu wangu, aliyeuawa kati yenu, hapo akaapo Shetani. Lakini ninayo maneno machache juu yako, kwa kuwa unao huko watu washikao mafundisho ya Balaamu, yeye alimfundisha Balaki atie vikwazo mbele ya Waisraeli, kwamba wavile vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu na kuzini. Vivyo hivyo wewe nawe unao watu washikao

mafundisho ya Wanikolai. Basi tubu, na usipotubu, naja kwako upesi, nami nitafanya vita juu yao kwa huo upanga wa kinywa changu" – Ufunuo 2:12-16.

Bila kujaribu kutoa maelezo ya undani zaidi tena juu ya ujumbe huu, ni wazi kwamba Yesu anawakumbusha watu wake kuwa waaminifu hata kufa, bali anawasihi wawe waangalifu katika kuafikiana juu ya mafundisho yao safi. Wamekubali uongo badala ya ukweli.

Kutoka kwa "uongofu" bandia wa mfalme Konstantino katika mwaka 313 B.K., alipofanya ukristo kuwa dini ya serikali, na baadaye kusimika kikamilifu nguvu ya upapa katika mwaka 538 B.K., Ukristo uliafikiana sana. Sabato ya Biblia (siku ya saba) nafasi yake ilichukuliwa na Sabato ya ugushi ya Jumapili. Biblia ambayo ina mamlaka pekee kwa Ukristo nafasi yake ilichukuliwa na mila na desturi za wanadamu. Uhuru wa kidini uliitwa uasi. Wokovu haukuwa tena zawadi ya bure bali ni zawadi kwa ajili ya jitihada za mwanadamu bila msaada wowote.

Tumeshaona kwamba Shetani alipoona mateso hayafanikiwi katika kuwaangamiza wafuasi wa Kristo, alibadili kwenda kwenye njama ya maafikiano. Je, hii inapendekeza kwamba Shetani aliacha kabisa mateso?

Ushahidi wa kweli kabisa, la hasha.

"Kuna swali jingine na swali muhimu sana ambalo makanisa ya leo yanapaswa kulipa usikivu. Mtume Paulo anaeleza kwamba "na wote wapendao kuishi maisha ya

> utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." – 2 Timotheo 3:12. Kwa nini inaonekana kwa kiasi kikubwa kwamba mateso yanasinzia? Sababu pekee ni kwamba kanisa limekubaliana na viwango vya ulimwengu na hivyo halisababishi upinzani wowote. Ukristo uliopo katika siku zetu siyo safi na wa tabia takatifu iliyotambulisha imani ya Kikristo katika siku za Kristo na mitume wake. Ni kwa sababu tu ya roho ya maafikiano na dhambi inayofanya ukweli mkuu wa neno la Mungu kutojaliwa kabisa. Kwa sasa Ukristo ni maarufu sana duniani na utauwa umekuwa kidogo sana kanisani. Endapo kutatokea uamsho wa imani na nguvu ya kanisa la kwanza, roho ya mateso itaamshwa, na moto wa mateso utawashwa tena" – *The Great Controversy,* uk. 48.

Kama juhudi za Shetani katika karne za kwanza za kulaghai Wakristo katika maafikiano zisingefaulu – kama wangebaki imara na wanyenyekevu, Shetani angerudia tena kuwatesa Wakristo, na pengine angewatesa zaidi.

Kwa nini leo hii hakuna mateso yaliyowapata Wakristo wa Kwanza? Kwa sababu maafikiano yanaendelea vizuri zaidi – siyo tu katika ngazi ya kanisa (kutojali kuhusu ukweli wa Biblia) bali pia katika kiwango cha mtu binafsi (kuafikiana na dhambi).

Kila Mwadventista anajua, kwamba ijapokuwa mvua ya masika inakuja. Tunajua kwamba uamsho mkuu utataokea kabla ya mwisho wa wakati. Tunajua kwamba, utauwa wa awali utatawala tena.

Na hilo litakapotokea, mateso yatakuja tena. Wakati wa taabu utaanza. Yale yote waliyoyapitia Wakristo wa

awali – na zaidi – Watu wa Mungu katika siku za mwisho watayapitia.

Kwa wengine hili ni jambo la kutisha. Ye yote kati yetu anaweza kushangaa kama tuna nguvu za kusimama imara kwa ajili ya kweli, na kwa ajili yake yeye aliye kweli hata katika mateso na kifo. Je, tunaweza kuvumilia mateso? Kufungwa gerezani? Kifo?

### *Wakati Neema Inapohitajika*

"Neema yangu," Mungu anasema, "yatosha; maana uwezo wangu hutimilika katika udhaifu." – 2 Wakorintho 12:9.

Leo hii – wakati huu – unaweza usiwe na neema, kwa ajili ya mateso au kifo. Kwa sababu leo, pengine hukabiliani nayo. Lakini kama wakati ukija ambao Mungu ataita, ama kuruhusu, ama pengine kukutunukia heshima ya kuwa mmojawapo wa kuyakabili mambo hayo, hapo ndipo atakupa neema ya kukabili mateso na kifo.

Jinsi nilivyo mwaminifu leo kwa Bwana wangu, ni maandalizi ya vile nitakavyokuwa mwaminifu wakati wa mateso. Jinsi ulivyo mnyenyekevu na mwaminifu – leo kwa ukweli wa Mungu ni kipimo cha jinsi utakavyokuwa mwaminifu kwa wakati huo.

Kwa kupitia Efeso, Smirna, na Pergamo, Mungu daima amekuwa ana waaminifu wake pamoja na wanyenyekevu wake. Wale wanaosimama katika ukoo usiokatika kuanzia kwa Adamu na utakao endelea kipindi chote cha wakati hapa duniani. Ni mfululizo usiokatika ambao wewe na mimi

ni viungo.

Wakati jaribu kubwa zaidi kuliko yote litakapokuja, tunahitaji kusimama imara. Je, tuna matayarisho yaliyo bora? Tujitahidi kwa kadri inavyowezekana kuunganika na chanzo cha nguvu. Leo – kesho –na kila siku.

Moja ya nyimbo za mwimbaji wa vijijini, Jo Dee Messiana una maneno haya: “Kesho ni siku nyingine...kiu yangu itabaki kuwa vile vile...hivyo leta mvua.”

Je, yupo Mwadventista mahali po pote ambaye hawezi kurudia rudia hilo tamko na kulitumia kwa ajili ya matumaini yetu ya uamsho unaokuja?

Naam, kesho ni siku nyingine, na nina kiu sana, Bwana.

Leta mvua – mvua ya masika.

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 8

# Mwanamke Wa Nyikani

Kiwanda cha filamu cha Hollywood nchini Marekani, ni kama mtu anayecheza na mtumbwi kwenye mawimbi ya bahari – kila wakati akitafuta wimbi kubwa linalofuata.

Kama ikigundulika kwamba vitabu vyenye mambo ya kidini vinaongoza katika orodha ya vitabu vinavyouzwa sana, Hollywood inafanya haraka kuingia huko. Wakati mfululizo wa kitabu "Kubaki Nyuma" kilipokuwa kimechapwa ulimwenguni kote, Hollywood walijitengenezea njia kwa ajili ya muigizaji wa filamu nchini Marekani aitwaye Mel Gibson kutengeneza The Passion of the Christ (Juma la Mateso ya Kristo). Na filamu hiyo ilipouzwa vizuri sana, watengenezaji wengine wa filamu hawakupoteza muda kutoa ya, 'The Da Vinci Code' (Siri ya Da Vinci), 'The Lion' (Simba), 'the Witch' (mchawi) na 'the Wardrobe' (kabati la nguo).

Usijali kwamba Hollywood haionekani kufanya sawa. Kama hawafanyi makusudi kuwavuta watu kimsisimko, wanaeneza dini ambayo kwa wazi kabisa sio sahihi au inapinga Biblia au wanatumia njia ya matokeo mema ambayo sio hakika bali ni njozi tu.

Kama watengenezaji wa filamu wanataka hasa filamu

za kidini kuwafanya watazamaji hwashangazwe – kwa kitu fulani chenye mchezo wa kuvutia na kuwapa utaalamu wa kutengeneza zile sehemu maalum za filamu changamoto – wanapaswa kuweka unabii wa vitabu vya Biblia vya Danieli na ufunuo katika runinga (televisheni) kubwa. Lakini hawawezi kwa sababu wanataka kuiimarisha habari kwa kuibadilisha. Hawawezi kuiacha kama ilivyo.

Lakini huwezi kuimarisha visa vya Danieli na Ufunuo. Chukua kwa mfano kisa cha joka na mwanamke.

Kama Mwadventista, bila shaka unafahamu hiki ni kisa fika, kama ndivyo, hivyo tayari unajua ni kisa kizuri! Hivyo washa runinga (kioo cha televisheni) iliyo pana. TV ya kisasa, skrini kubwa sana katika mawazo yako, na uangalie tena mchezo ulioko kwenye Ufunuo 12.

> "Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili. Naye alikuwa ana mimba, akalia, hali ana uchungu na kuumwa katika kuzaa. Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu aliyekuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu vichwa vyake vilemba saba, na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliyetayari kuzaa, ili azaapo ammeze mtoto wake" – Ufunuo 12:1-4.

Waandishi wazuri wa visa wanatumia ujuzi unaoitwa "kumbusho la ghafla" (flashback) ambayo inaingilia kisa

wanachosimulia pale mwanzo kabisa wa tukio husika. Mtume Yohana – Mwandishi wa Ufunuo –vilevile alikuwa mwandishi mzuri. Katika mafungu ya hapo juu, Yohana anasema kwamba na mkia wake (huyu joka), ulikokota theluthi ya nyota za mbinguni na kuziangusha chini.

Kisa kinaendelea mbele, lakini baadaye Yohana anarudi nyuma wakati nyota za mbinguni ziliangushwa chini.

> "Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, yule joka mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyae ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye" – Ufunuo 12:7-9.

Malaika wa joka – theluthi ya nyota za mbinguni – walitupwa kutoka mbinguni pamoja naye.

Mafungu haya matatu yanaeleza kwa ufupi mwanzo kabisa wa pambano kuu kati ya wema na uovu. Shetani (ameelezwa wazi hapa kama Ibilisi au Shetani – malaika aliyeanguka Lusifa) alipotangaza vita dhidi ya Mungu, yeye na theluthi ya malaika wa mbinguni ambao alikuwa amewalaghai kwa uongo wake walipigana dhidi ya Mikaeli (Kristo).

### *Mwanamke Nyikani*

Bali katika dunia hii, Shetani, yule joka mkuu, aliendelea

na vita vyake dhidi ya Mungu. Usomaji wa uangalifu juu ya kitabu cha Ufunuo, kunafunua wazi kwamba mwanamke ni alama ya kanisa. Hapa katika Ufunuo 12 tunaona mfano wa mwanamke mzuri na hatimaye katika ufunuo 17, unaweza kumkuta mwanamke mbaya sana.

Hapa katika kisa chetu, mwanamke yupo tayari kuzaa, na Yohana anatuchorea picha ya joka mkali akisubiri kumvamia mtoto wake ghafla mara tu azaliwapo. Bali Mungu alimlinda mwanamke na mtoto wake.

> "Naye akazaa mtoto mwanaume, yeye atakayechunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Na mtoto wake akanyakuliwa hata katika kiti chake cha enzi kwa Mungu. Yule mwanamke akikimbilia nyikani, ambapo ni mahali palipotengenezwa na Mungu, ili aweze kulishwa huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini" – Ufunuo 12:5, 6.

Huyu mtoto mwanaume hakuwa mwingine ila Yesu mwenyewe – Mikaeli yule yule ambaye joka alipigana naye huko mbinguni. Sasa Yesu alikuwa amekuja kuzaliwa huku duniani kama mtoto mchanga, kukua kama mtu mzima, na hatimaye kuwa mwokozi wa jamii ya wanadamu.

Lakini baada ya maisha yake, kifo, na ufufuko, Yesu alipaa juu mbinguni kwa Mungu na kukaa katika kiti chake cha enzi. Halafu joka akamgeukia mwanamke kwa umakini wote – yaani kanisa aliloanzisha Yesu kabla hajapaa mbinguni.

Yohana anasema "akaruka kwenda nyikani," ambako

Mungu alimlisha kwa muda wa siku elfu na mia mbili sitini."

> "Na joka yule alipoona kuwa ametupwa katika nchi, alimwudhi mwanamke yule aliyezaa mtoto mwanamume. Mwanamke yule akapewa mabawa mawili ya yule tai mkubwa, ili aruke, aende zake nyikani hata mahali pake, hapo alishwapo kwa wakati na nyakati na nusu wakati, mbali na nyoka huyo" – Ufunuo 12:13, 14.

Wakati na nyakati na nusu ya wakati. Siku elfu mia mbili na sitini. Hii ni nini?

Wakati katika unabii, Biblia inasema siku moja ni sawa na mwaka mmoja (angalia Hesabu 14:31, Ezekieli 4:6). Katika orodha ya unabii mwaka pia una siku 360. Hebu tufanye hesabu kidogo. Siku elfu na mia mbili na sitini (1260) ni sawa na miaka 1260. Kutokana na mafungu ya Biblia, inadhihirika pia kwamba wakati pia ni sawa na mwaka. Hivyo wakati (siku 360) jumlisha 'nyakati' (2 X 360 [siku] au siku 720) jumlisha nusu ya wakati (siku 180) ni sawa na siku 1,260. Vipi tupo sawa, ewe mwana mahesabu?

Siku elfu na mia mia mbili na sitini katika fungu la sita ni sawa na "wakati na nyakati na nusu ya wakati" katika fungu la 14.

Mwanamke alikuwa nyikani kwa muda wa miaka 1,260.

Sasa, hebu tufanye mambo kuwa ya kupendeza zaidi. Angalia hii katika agano la kale, kitabu cha Danieli.

> "Naye atanena maeno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria, nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati na nyakati mbili na nusu wakati" – Danieli 7:25.

Huyu anaye tajwa hapa kama, "Naye" ni mnyama mkubwa wa kutisha mwenye pembe kumi. Angalia jinsi utawala ulivyo watesa watakatifu kwa muda mrefu " wakati na nyakati mbili na nusu ya wakati." Je, ni kama inavyofahamika?

Vitabu vyote viwili; Danieli na Ufunuo vinatabiri kipindi cha miaka 1,260. Danieli anasema kwamba katika kipindi hiki, watakatifu watateswa. Ufunuo anasema katika kipindi hiki, mwanamke atateswa. Mwanamke. Kanisa. Watakatifu. Maneno haya yote yanaongelea kitu kilekile.

Kwa kuangalia vitabu vyote viwili; Danieli na Ufunuo, tunagundua mambo kadhaa yaliyotokea katika kipindi hiki cha miaka 1,260.

- Watakatifu wanateseka (au mwanamke).
- Mwanamke akimbilia nyikani, mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko.
- Utawala mkuu ambao hunena maneno makuu kinyume na Aliye juu.
- Utawala huu unawatesa watakatifu.
- Na utawala huu unakusudia "kubadili nyakati na sheria."

Waadventista Wasabato wengi ambao ni wanafunzi wa

Biblia tayari wanajua kwa undani zaidi juu ya unabii wa miaka 1,260. Kama wewe ni mmoja wa wanafunzi wa unabii, utakuwa unajua kwamba utawala huu mkuu wa kinyama ulikuwa ni muungano Ukristo wa kitume na upagani ambao ulitayarisha kuibuka kwa utawala wa upapa.

### *Kukua Kwa Utawala Wa Askofu Wa Roma*

Maaskofu au viongozi wa makanisa ya Kikristo ya kwanza mwanzoni hawakuwa na utawala mkuu. Lakini kwa kadri wakati ulivyoendelea, kanisa lilianza kuwa na nguvu zaidi katika eneo moja – na askofu wake aliendelea kuwa maarufu zaidi: Kanisa la Roma. Maaskofu wengine wakaanza kutafuta uongozi kutoka katika kanisa hilo – au walitafuta maelekezo ya askofu wa kanisa hilo.

Kama tulivyoona katika sura iliyo tangulia – wakati upagani ulipoingia kanisani, hakuna mahali pengine ambapo hili lilifanikiwa zaidi kuliko katika kanisa la jiji la mfalme. Mapema katika karne ya nne chini ya mfalme Konstantino, Ukristo ukawa dini ya serikali – au angalau aina ya Ukristo. Mpaka sasa, kanisa la kuafikiana lilikuwa limekwisha karibisha kundi la mafundisho na matendo ya upagani ambayo hayakufanana na Ukristo wa Wakristo wa kwanza.

Mamlaka na utawala wa askofu – au papa – katika kanisa la Roma ulikuwa sana kiasi kwamba angetoa amri zilizofuatwa na makanisa yote ya Kikristo. Halafu katika mwaka wa 533 B.K., mfalme wa Roma aitwaye Justinian, alitoa amri ya kumfanya askofu wa Roma kuwa mkuu wa

makanisa yote matakatifu. Lakini tawala nyingine katika himaya ya Urumi zilipaswa ziondolewe kabla amri hiyo haijaanza kufanya kazi. Tawala hizo zilishindwa ilipofika mwaka 538, na kutoka wakati huo na kuendelea – kwa miaka 1,260 iliyofuata – utawala wa upapa ulikuwa juu.

Sura zote mbili hii na inayofuata zitalenga kipindi hiki cha miaka 1,260. Kama umekuwa ukisoma kwa makini, umegundua kwamba tumekuwa tukifuata mfululizo wa makanisa saba ya kitabu cha Ufunuo. Miaka 1,260 inahusisha makanisa mawili kati ya hayo, kanisa la Thiatra kutoka 538 hadi 1517 B.K. na Sardi kutoka 1517 hadi 1798. Hivyo kwa sasa tunalenga kipindi cha wakati wa Thiatra. Na sura ya 9 italenga zaidi juu ya kanisa la Sardi.

Kwa masikitiko kufikia mwaka 538 B.K. kanisa la Roma lilikuwa limeshakuwa ni mfumo wa kutatanisha lenye mafundisho na matendo ya uongo. Desturi za kibinadamu na amri za kipapa vilikuwa na mamlaka zaidi ya Biblia. Watu wote walizuiliwa kuwa na nakala ya Biblia isipokuwa wachungaji. Njia ya kumfikia Mungu ilikuwa ni kupitia kwa mchungaji tu. Wokovu ulikuwa ni kwa kupitia mfumo wa kazi za kidini. Toharani, malipo kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kumwabudu Maria, ubatizo wa kunyunyiza maji, Petro kuwa muasisi wa kanisa, papa kutokukosea, misa, kuubadilisha mkate kuwa Yesu mwenyewe, kuungama dhambi kwa mapadri, kuabudu sanamu – makosa yaliongezeka sana. Yote niliyo taja hayana msingi wowote wa Kibiblia. Yote hayo hayakufanywa wala kufahamika kabisa wakati wa kanisa la Wakristo wa kwanza.

Lakini kama uongo wote huu ulikuwa wa kusikitisha, chakusikitisha zaidi ilikuwa ni ushupavu wa kanisa la Roma, kulazimisha mafundisho yake, matendo yake na matakwa yake kwa nguvu. Wale ambao hawakukubali waliteswa na wengi waliangamia.

Bali kwa kupitia kipindi chote hiki cha giza kutoka mwaka 538 B.K. hadi kukomeshwa kwa nguvu ya upapa katika mwaka 1798 Mungu alikuwa na watu wake waaminifu – wanyenyekevu na waumini waliojitoa kikamilifu na walikuwa watiifu kwa Bwana wao hata kama ingemaanisha mateso.

Hata kama ingemaanisha mateso ya kifo, hawa wangesimama katika kweli ya Mungu bila kujali chochote. Wangeendelea kuabudu siku ya Sabato ya Siku ya Saba ya Mungu – sio Sabato ya Jumapili iliyotengenezwa – na mwanadamu na kulazimishwa kwa nguvu na kanisa la Roma. Wangeendelea kushikilia Biblia – na Biblia peke yake ndiyo yenye mamlaka kwao – siyo desturi na amri za wanadamu wenye makosa. Wangesimama imara katika ukweli wa Biblia juu ya wokovu, ubatizo, au mafundisho juu ya hali ya wafu.

Walipo zingirwa na maadui, waaminifu hawa walikimbilia nyikani. Waaminifu – kanisa mwanamke – walitafuta usalama katika milima na sehemu isiyokuwa na watu wengi. Angalia ufuatiliaji wa Shetani.

> “Nyoka akatoa katika kinywa chake maji kama mto, nyuma ya huyo mwanamke, amfanye kuchukuliwa na mto ule.

> Nchi ikamsaidi mwanamke, nchi ikafunua kinywa chake. Ikaumeza mto ule aliotoa yule joka katika kinywa chake" – Ufunuo 12;15, 16.

### *Nchi na maji*

Maji ni kitu gani? Katika unabii wa Biblia, maji ni alama ya watu (angalia Ufunuo 17:15). Nyoka, joka akatoa maji mengi kama mto nyuma ya mwanamke. Mafuriko ya watu. Na aina ya watu ambao wangetoka katika kinywa cha joka mwovu ni watu wabaya sana.

Bali "nchi ikameza mafuriko ya watesaji, wafuatiliaji waovu. Kama maji ni alama ya watu wengi, hivyo basi kwa uwiano, jangwa ni mahali pasipokuwa na watu wengi.

Sio tu kwamba wafuasi wa kweli wa Mungu walipata kimbilio, wakati wa mateso mabaya sana, katika milima iliyokuwa porini sana bali kabla ya mwisho wa miaka 1,260, mamilioni yasiyo na idadi walikimbia mateso ya kidini na kwenda kwenye nchi mpya iliyokuwa na watu wachache mno.

Miaka 1,260 ilipoanza, kanisa la Roma, na nguvu mpya ya utawala iliyopewa lilianza kwa ujeuri kulazimisha imani na matendo yao wakiwa na lengo la kuufanya ulimwengu wote chini ya utawala wao. Kufanya hivi, kulisababisha mateso ya kanisa la Mungu, mateso ambayo yalidumu kwa karne kadhaa.

Mfululizo wa waaminifu usiokatika haujawahi kukatika hata mara moja. Katika kipindi chote cha karne za giza, baadhi hawakumwacha Mungu kabisa au ukweli wake.

Hawakuafikiana kamwe.

Miongoni mwa hao, angalia visa vya kweli vya Waalbigensia na Wawaldensia. Mwanamke wa nyikani? Hakuna ukweli zaidi kuliko waumini, waliokimbilia kwenye milima mirefu ya Ulaya kuepuka mateso ya kanisa la Roma. Katika sura inayofuata, kisa cha kundi la waaminifu – Wahugenoti, waliosimama bila kutikisika kwa ajili ya kweli wakati wa Matengenezo – utasimuliwa.

### *Waalbigensia*

Mwanzoni mwa karne ya 12, kundi la wakristo wenye mawazo ya matengenezo (ulimwengu wote) wajitenga kutoka kwenye kanisa Katoliki la Roma – hawakuwa tayari kidhamira kukubali au kuamini mafundisho mengi ambayo hayakuwa ya Kibiblia.

Walijulikana kama Waalbigensia (kutoka mji wa Albi kusini mwa Ufaransa – kama maili ishirini na mbili kaskazini mwa mji wa Toulouse wa sasa); waumini hawa walihubiri kinyume na mafundisho ya Katoliki kama uchungaji wa kibinadamu, ibada za watakatifu na sanamu, na kuinuliwa kwa mamlaka ya Biblia. Kufikia mwaka 1167 B. K. Waalbigensia walikuwa ndiyo sehemu kubwa ya idadi ya wakaazi wa kusini mwa Ufaransa.

Je, Waalbigensia walifundisha na kuamini ukweli wote unaofundishwa na kanisa la Waadventista Wasabato leo? La hasha. Je, walikuwa na baadhi ya imani ambazo hatuwezi kuzikubali leo? Ndiyo. Lakini walimpenda Bwana wao na kuchagua kifo kuliko kutokumtii.

Kutokana na tishio la Waalbigensia kwa nguvu na utawala wa kanisa la Katoliki; kanisa lilitumia nguvu kuwapinga. Katika mwaka wa 1208, papa mmoja mkali aitwaye Inosenti III alitoa amri ya mashambulio ya kuteketeza mafundisho yaliyoitwa ya uongo – "uasi." Majeshi ya papa yaliingia katika eneo la Waalbengisia, na miji yote ilishambuliwa. Utaratibu huu wa kuwachinja waumini hawa uliendelea kwa miongo kadhaa, kwa muda kwa kadri kanisa lilivyoongeza kutoa mfululizo wa amri za Mahakama ya Kanisa Katoliki ya papa – hata kampeni za ujeuri zaidi za mateso na mauaji kuteketeza kilichoitwa uasi.

Kampeni ya papa ilifanikiwa. Katika miaka mia moja tangu walipoanza kutawala, Waalbigensia waliteketezwa kabisa. Hadi mwumini wa mwisho, bado tu walibaki kuwa waaminifu kwa neno la Mungu – na waliendelea kupinga mafundisho ya upapa ya uongo na matendo ya kanisa ya upagani.

### *Wawaldensia*

Mwanzoni mwa miaka ya 1170 B.K., Petro Waldo, mfanya biashara tajiri wa Lyons, Ufaransa aliandaa kundi la waumini ambao mwanzoni walijulikana kama Watu Masikini wa Lyons – walei wa Kanisa Katoliki ambao waliwafuata viongozi wao kwa kutoa mali zao, wakiamini kwamba umasikini wakitume ni njia ya ukuaji wa Kikristo.

Katika mwaka wa 1179 walikwenda Roma ambako papa Alexander III aliwabariki, lakini aliwapiga marufuku wasihubiri isipokuwa wakiruhusiwa na padri wa maeneo

hayo. Bali Wawaldensia (au Vaudois, kama walivyojulikana katika lugha ya kifaransa) hawakutii hiyo amri na wakaanza kufundisha ukweli walioupata katika Biblia.

Waliitangaza Biblia kama kiongozi chao kikuu cha imani na matendo ya maisha. Na walihubiri kinyume na mafundisho ya Katoliki kama toharani, upapa, misa na malipo ya kusamehewa dhambi.

Katika mwaka wa 1184 walitangazwa rasmi kama waasi na papa Lucius III – na ilidhibitishwa baadaye katika halmashauri ya nne ya Lateran katika mwaka 1211, zaidi ya Waaldensia themanini walichomwa moto kama waasi kule Strasbourg – mwanzo wa karne kadhaa za mateso.

Idadi kubwa ya Wawaldensia waliishi Dauphine na Piedmont – pia Alps kusini mwa maeneo ya Turin.

Katika mwaka wa 1487, Papa Inosenti VIII alianzisha mateso ya kinyama, kuwaangamiza Wawaldensia. Wawaldensia wa Dauphine walishindwa bali waumini wa Piedmont walifaulu kujitetea wenyewe.

Vyote viwili kanisa na serikali ya Ufaransa viliendelea kuwatesa Waldensia, wengi walikimbilia Alps – Uswizi. Hatimaye katika 1848, Mfalme Charles Albert wa Sevoy aliwapa uraia kamili na uhuru wa dini. Mapema baadaye kikosi cha ziada cha Waldensia kilihamia Kaskazini mwa Carolina katika nchi ya Marekani.

> "Baadhi ya mambo yaliyosababisha utengano kati ya kanisa la kweli na Roma," Ellen White ameandika "ilikuwa ni chuki ya baadaye juu ya Sabato. Kama unabii ulivyokwisha

kusema, utawala wa kipapa ulitupa chini ukweli. Sheria ya Mungu ilikanyagwa kwenye mavumbi, wakati ambapo mila na desturi za wanadamu ziliinuliwa juu .... Katika kipindi hiki cha giza na uasi, kulikuwa na Wawaldensia waliokana utawala wa Kiroma, waliokataa kuabudu sanamu kama ibada ya miungu, na waliyotunza Sabato ya kweli. Chini ya tufani ya ukatili mkuu wa upinzani walitunza imani yao" – *The Great Controversy,* uk. 65.

"Nyuma ya mapango juu ya milima –ndipo palikuwa kimbilio la walioteswa na kunyanyaswa katika vizazi vyote – kamavile Wawaldensia walivyopata hifadhi huko. Nuru ya ukweli iliendelea kuwaka katika giza ya Enzi ya Kati, na kwa miaka maelfu mashahidi wa ukweli walitunza imani ya zamani" – *The Great Controversy,* uk. 65, 66.

Idadi ya namba kamili ya Wawaldensia waliokufa kwa ajili ya imani yao haiwezi kujulikana kamwe. Baadhi ya vyanzo vya habari vinavyotunza mambo ya kale vinakisia kwamba watu 900,000 waliuwawa kati ya mwaka 1540 na 1570 peke yake.

"Mateso yaliendelea kwa karne nyingi dhidi ya watu waliomcha Mungu waliovumilia kwa subira na uaminifu ambao ulimpa heshima Mwokozi wao. Ijapokuwa mashambulio dhidi yao na mauaji yasiyo ya kiubinadamu yaliwakumba, waliendelea kuwa wamishenari kutawanya ujumbe wa thamani. Waliwindwa na kuuwawa, bali damu yao ilimwagilia mbegu iliyopandwa na haikushindwa

kutoa matunda" – *The Great Controversy,* uk. 78.

Unaweza kupata historia zaidi juu ya Wawaldensia, kwa kusoma kwa uangalifu sana sura ya nne ya kitabu cha Pambano kuu. Hakuna chanzo kingine zaidi cha kutia moyo kilichopo cha kutia nguvu kama uamuzi wa kusimama kwa ajili ya kweli, kwa hali iwayo yote.

Mwanamke (ambaye ni Kanisa) aliingia kwenye kipindi cha miaka 1,260, miaka ya giza – karne zenye mateso ya kutisha sana kuliko yote yaliyowakabili waaminifu wa Mungu.

Marafiki zangu ni wangapi kati yetu ambao wana upendo mkuu juu ya Yesu Kristo na ukweli wake ambao hauwezi kukatika kwa ajili ya mateso, shida au kifo? Ni wangapi kati yetu wamejiandaa kuwa waaminifu kwa Mwokozi wetu, kwa hali iwayo yote?

Katika dunia hii katika maisha haya – inatokea mara kwa mara kwamba mwanaume na mwanamke wanapendana. Wanapendana sana kiasi kuwa kila mmoja yupo tayari kutoa maisha yake bila kusita kwa ajili ya mwenzake, je, ni lazima iwe hivyo? Je, tunapalilia aina hiyo ya uhusiano wa karibu na Yesu kila siku, ambao unachochea upendo wenye nguvu sana kiasi kwamba tunaweza kutoa maisha yetu kwa ajili yake wakati wo wote? Je, tunaweza kuwa tayari kutoa maisha yetu kwa ajili yake kama alivyotoa maisha yake bila kusita?

### *Kushinda katika Jaribu*

Kwa sasa, tunaweza kuwa tayari kusimama kwa ajili

ya kweli, na kwa ajili ya Yesu, Mwasisi, wakati wa amani. Lakini kwa hakika wakati unakuja – na kwa karibu zaidi kuliko tunavyodhani – wakati wa kusimama kwa ajili ya Yesu itakuwa ni kualika ghadhabu isiyo na sababu kwa wale wanaompinga Yesu.

Dhidi ya siku ile, je, tunaendelea siku baada ya siku kujitoa wakfu kwa Bwana wetu? Je, tunajenga tabia ambazo zitasimama imara katika shinikizo lo lote la kuafikiana, kukata tamaa au kujiokoa wenyewe? Kumbuka kwamba, ingawa – neema ya ufia dini haihitajiki hadi tutakapokabiliana na huo uchaguzi. Lenga sasa kuimarisha upendo na kujitoa kikamilifu. Kama Mungu amemwita ye yote kati yetu kufanya kafara ya juu kama wengi wa Waalbigensia na Wawaldensia walivyofanya, kwa wakati huo na wakati huo tu Mungu atatupa neema ya kutosha.

Kama unampenda sana mwenzi wako katika dunia hii – au kama ni mzazi wa mtoto – unajua kwamba kama ingehitajika kufa kwa ajili yao kungekuwa manufaa na hadhi. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa yeyote kati yetu ambaye ana upendo kwa Mwumbaji wetu zaidi ya maneno ya kutamka.

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 9

# Huu Ndio Msimamo Wangu

Je, umewahi wakati wo wote kupoteza pochi au mkoba wako au funguo zako?

Kuna uwezekano mkubwa kwamba umewahi kupoteza. Pia kuna uwezekano kwamba ilipotokea, watu walijaribu kusema mambo ya kukusaidia.

Kama: Uliuona lini kwa mara ya mwisho?

Au: Sawa, haukuota miguu na kutoweka.

Au: Haukupotea kabisa.

Kwa wakati huo, unaweza usione maelezo hayo kama yana msaada wa pekee. Pamoja na hayo yana ukweli. Kamwe katika historia yote ya ulimwengu mkoba haujaota miguu na kwenda nje ya mlango. Haijatokea hata mara moja. Na wala pochi haijayeyuka kutoka kwenye yabisi na kuwa gesi. La, hasha!

Hii ina maana kwamba kitu fulani kikipotea bado kinaendela kuwepo mahali fulani. Kinahitaji tu kutafutwa – kugunduliwa kilipo.

Yesu alisimulia visa vya kupoteza sarafu, kupoteza kondoo na mwana mpotevu. Vyote hivi vitatu, hatimaye vilipatikana.

Wapiga mbizi hutafuta hazina zilizopotea za meli

zilizozama zikiwa zimebeba mizigo ya dhahabu na vito vingine vya thamani. Watafiti wa hazina hutafuta madini ya dhahabu iliyopotea – au mali ya thamani ya kushangaza iliyozikwa mahali ambapo ramani ina alama ya "X". Polisi hutafuta watoto waliopotea. Mafundi huondoa tabaka ya rangi ya juu ili kupata mchoro wa sanaa yenye thamani sana iliyoko chini ya tabaka. Wachunguzi nao bado wanatafuta sanduku la agano na safina ya Nuhu.

Kama vitu vinapotea bado vipo. Vinahitajika kutafutwa na kuonekana.

Hazina kuu ya ulimwengu huu hatimaye kuijua, sio kikombe alichotumia Kristo wakati wa Alhamisi kuu ya pasaka au migodi ya Sulemani au baadhi ya maeneo ambayo hayajagunduliwa alumasi yenye ukubwa sawa na mipira ya magongo (baseball). Hazina kuu kuliko zote ulimwenguni ni Mwumbaji, Yesu Kristo. Na alipoondoka duniani, pia aliwaachia wafuasi wake wote hazina ('h'- ndogo), ambayo wangeifurahia na kushiriki pamoja na wengine: ambayo ni ukweli wake.

Lakini baada ya miaka kupita, hazina hii ya ukweli ilianza kufunikwa na tabaka la uongo. Hii haikuwa ajali – ilikuwa ni kazi iliyokusudiwa na adui mkuu wa Kristo, ambaye alikuwa amepenyeza katika kanisa la Kristo mwenyewe na kuliongoza katika maafikiano, ugushi na kukanyaga ukweli ambao kanisa lilikuwa limepewa.

Wakati huo, kila ukweli ulikuwa umezikwa chini ya matabaka ya kanisa – udanganyifu na uongo.

- Ukweli wa wokovu kama zawadi ya bure ulibadilishwa na mafundisho ya uongo ya wokovu kwa njia ya jitihada za mwanadamu.
- Ukweli kwamba Yesu ndiyo njia ya kumfikia Mungu ulibadilishwa na mafundisho ya kwamba njia pekee ya mwanadamu kumfikia Mungu ni kupitia kwa mapadri.
- Mamlaka ya biblia yalibadilishwa na mamlaka ya upapa pamoja na desturi za mwanadamu.
- Msamaha haukuwa tena ni zawadi iliyopatikana bure bali kwa njia ya malipo.
- Siku ya kupumzika ya Sabato ilibadilishwa na kuwa Jumapili – siku aliyochagua mwanadamu.
- Maungamo kwa Mungu pekee yake, yalibadilishwa na kuwa maungamo kwa makasisi.
- Biblia kama zawadi ya Mungu kwa wote, ilikuwa ni marufuku kuisoma au hata mtu yeyote kuimiliki, isipokuwa viongozi wa Kanisa tu waliruhusiwa.
- Hata amri Kumi za Sheria ya Mungu zilibadilishwa kufaa kanisa ambalo lilikuwa limepoteza njia yake.

Pamoja na hayo yote, wingi wa mafundisho yasiyo ya Kibiblia na matendo yalifundishwa kama ukweli – ikiwa ni pamoja na misa, hostia (Iliyodhaniwa kuwa ni kubadilisha mkate mtakatifu na divai ya meza ya Bwana kuwa mwili na damu halisi ya Kristo), maombi kwa ajili ya wafu, utukufu wa Maria na watakatifu wengine na utakatifu wa miungu na sanamu.

Kumbuka kwamba ujumbe muhimu wa pekee sana katika kitabu hiki ni: Mungu daima amekuwa ana wafuasi waaminifu, watiifu kwake na kwa ukweli wake. Katika kila kizazi tangu wakati wa Edeni, Shetani amefanya kila anachoweza kuficha au kugushi au kufunika ukweli, Mungu daima amekuwa ana watu waliokusudia kuamini ukweli huo, kuishi kwao, na kushirikiana na wengine kuhusu ukweli huo.

Kama ni wazee wa imani waliomfuata Adamu, waaminifu wa Israeli, waumini wa kanisa la awali,– au kama wale Waalbigensia na Wawaldensia ambao tumewaona katika sura iliyotangulia, waliosimama kwa ajili ya kweli kwa gharama ya maisha yao – Mungu amekuwa na mfululizo wa waaminifu usiokatika wakati wote.

Katika kipindi cha saa za giza kuu katika Zama za Giza, Mungu alikuwa na mashujaa na watiifu waliokusudia kuufunua ukweli uliopotea na kuuleta tena mahali pa wazi.

### *Ujumbe katika Ubao wa Matangazo*

Ujumbe huu ulianza katika ubao wa matangazo katika Chuo Kikuu kimoja cha Ujerumani.

Katika miaka hiyo, mlango wa kanisa la chuo kikuu mara nyingi ulitumika kama ubao mkuu wa matangazo kwa ajili ya chuo – na tarehe 31 mwezi wa kumi, mwaka 1517, wale walio angalia mlango walikuta hati imebandikwa na aliyekuwa padri na mkufunzi wa Kanisa Katoliki wa Chuo Kikuu. Hiyo hati ingebadilisha dunia, kwa ajili ya hoja 95 za Martin Luther – zilizo kuwa zime ngongomewa

katika mlango wa kanisa hilo la chuo cha Wittenberg Castle. Hoja hizi moja kwa moja zilipinga makosa dhidi ya ukweli wa Biblia, ambayo ilikuwa chanzo cha matengenezo ya Kiprotestanti.

Japokuwa historia inaonyesha kana kwamba hoja 95 za Martini Luther ndio mwanzo wa Matengenezo ya Kiprotestanti, ukweli ni kwamba matengenezo yalikuwa yameanzishwa tayari karne moja au zaidi kabla na John Wycliffe. Ingawa alikuwa miaka mia moja kabla ya kuzaliwa Martin Luther, ambaye alikuja kujulikana baadaye kama nyota ya asubuhi ya matengenezo kwa mafundisho yake shapavu na kuhubiri ukweli wa Biblia. Mvuto wa Wycliffe kwa wanamatengenezo wa kwanza kama vile Luther, ulikuwa wa ajabu – mvuto ambao ulimfanya akawa mtu wa kwanza kuchapa Biblia katika lugha iliyosomwa na watu wa kawaida.

Mwanafunzi na mfuasi wa Wycliffe aitwaye John Hus, pia alikuwa na mvuto mkuu kwa wanamatengenezo wa zamani. Yeye alifundisha karibu ukweli wote ambao Luther na wengine baadaye walifanya kuwa msingi wa jitihada zao za kulitengeneza kanisa ambalo kwa kipindi cha karne kadhaa lilizika ukweli chini ya matabaka ya mafundisho potofu.

Hus bila kuogopa alipinga makosa mbalimbali ya kanisa, ikiwa pamoja na uuzaji wa hati za msamaha wa dhambi – malipo ya ada au kutoa mchango ili kupata msamaha wa dhambi. Kanisa lilimpa Hus jina baya kama mwasi, na katika mwaka 1411, Hus alitengwa kutoka katika

kanisa. Bali aliendelea kufundisha ukweli wa Biblia na kupinga makosa ya kanisa na hatimaye katika mwaka 1415, Kanisa lilimchoma moto katika nguzo iliyokuwa ikitumika kuwachomea watu kama yeye. Jerome wa Prauge rafiki na mfuasi wa John Hus, alikabiliwa na mauti ya namna hiyo hiyo katika mwaka uliofuata.

### *Matengenezo Yaanza*

Viongozi hawa walio kuwepo kabla matengenezo hayajaanza rasmi, walijenga msingi wa Matengenezo yaliyofuata. Wakati Luther alipoweka wazi mada yake iliyo bainisha ukweli na uongo katika mwaka 1517, Matengenezo yalianza kwa bidii. Muda mfupi Luther alijikuta ametengwa na kanisa. Kwa kusaidiwa na mtambo mpya wa uchapaji uliogunduliwa Matengenezo yalienea kwa kasi. Huku nchini Switzerland, jitihada za Luther ziliendelea na kuungwa mkono na Ulrich Zwingli. Mwanatheologia wa Ufaransa John Calvin naye alikutanisha kamba za matengenezo kati ya nchi za Switzerland, Scotland, Hungary, Ujerumani na sehemu nyingine za Ulaya. Mwanatheologia wa Kidachi aitwaye Erasmus ambaye alikuwa na mvuto wa nguvu juu ya Luther, ingawaje alibaki kuwa mshiriki wa Kanisa Katoliki maisha yake yote, aliandika kwa ustadi upinzani wake juu ya makosa ya kanisa.

Wakati muhimu sana wa Matengenezo ulitokea tarehe 16 Aprili katika mwaka wa 1521, wakati ambao Mfalme wa Roma Charles V, akiwa na jeshi la papa, alimwita Luther katika mkutano wa kujadili mashauri ya kikanisa katika jiji

la Worms, huko nchini Ujerumani.

Msaidizi wa askofu mkuu wa eneo lile, Johann Eck, aliomwongoza Luther kwenye meza ambayo ilikuwa imefunikwa nakala za maandishi yake. Eck alimuuliza Luther kama vitabu hivyo vilikuwa vyake na kama bado alikuwa anaamini alivyoandika ndani ya vitabu hivyo.

Luther aliomba muda kabla ya kujibu, ambao alipewa. Luther alifikiria, akaomba, na kushauriana na rafiki zake. Siku iliyofuata alirudi kwenye mkutano ili kujadili mashauri ya kanisa.

Eck sasa alimuhitaji Luther ajibu swali. Utakana vitabu hivi na makosa yaliyomo ndani yake?

Jibu la Luther linapaswa kuwa ni jambo la fahari na changamoto kwa kila mmoja wetu anayetamani kusimama imara kwa ajili ya ukweli aliotupa Mungu:

> "Labda niwe nimeshawishiwa na Maandiko Matakatifu na sababu iliyo wazi," Luther alijibu, "Sikubali mamlaka ya mapapa na mabaraza, kwa sababu yamehitilafiana. Dhamira yangu imetekwa na Neno la Mungu. Siwezi na sitaweza kukana chochote, kwa sababu kuwa kinyume na dhamira si sahihi wala si salama. Huo ndio msimamo wangu, siwezi kufanya vinginevyo. Mungu nisaidie. Amina."

Siku chache baadaye, mkutano wa mashauri ya kanisa uliotoa amri kutangaza kwamba Luther ni mpinga sheria na mwasi. Lakini hadi wakati huu, Luther alikuwa

ameshatoroshwa salama na rafiki zake kwenda ngome ya Wartburg. Akiwa huko Luther alipata nafsi ya kuwasiliana na kumshauri rafiki yake Philipp Melanchthon na kupatana. Melanchton ni mmoja wa baadhi ya watu waliomsaidia Luther baadaye katika kutafsiri Biblia katika Kijerumani ili kwamba watu wa kawaida wawe na fursa ya kuitumia.

Tafsiri ya mwaka 1534 ilikuwa na mvuto wa pekee sana kwa William Tyndale, ambaye baadaye alichapa tafsiri ya Kiingereza ya Agano Jipya. Kazi ya Tyndale baadaye ilikuwa ni msingi katika kuendeleza tafsiri ya Biblia ya King James miongo michache baadaye.

Wazi wazi kabisa, Biblia ambayo ilikuwa imefungiwa na kanisa ilikuwa inajitokeza tena. Kwa kadri ilivyojitokeza – watu waliweza kuona ukweli uliofundishwa kinyume na makosa yaliyofundishwa na uongo – kazi ya matengenezo ilisonga mbele. Kwa kasi.

Luther, mkuu wa Matengenezo aliendelea na kazi ya kufunua na kurejesha ukweli uliopotea hadi wakati wa kifo chake katika mwaka 1546.

Luther, Calvin, na viongozi wengine wa Matengenezo waliondoa karne za mafundisho ya uongo na ugushi na kuleta nuru, ukweli halisi ambao Yesu mwanzoni kabisa alilikabidhi kanisa la awali la mitume ambao walikuwa wakristo wa kwanza.

Kwa kadri muda ulivyokwenda, Matengenezo yalipoteza kasi yake na shauku yake ya kwanza. Kabla ukweli WOTE wa Biblia uliyopotea haujapatikana na kurejeshwa, makanisa ya Matengenezo kwa kiasi kikubwa

yalipoteza mtazamo wao wa ujumbe na kutawaliwa na maswali ya taratibu za mfumo wa kanisa na kujadiliana juu ya tofauti zao.

Ilikuwa ni kazi ya Wakristo wa baadaye kurudisha ukweli mwingine mkuu uliopotea, ambayo ni pamoja na kweli ya Sabato, kurudi kwa Yesu mara ya Pili, kazi ya Kristo kama kuhani wetu na ukweli juu ya hali ya binadamu katika maisha na katika kifo.

### *Sardi*

Katika makanisa saba ya kitabu cha Ufunuo, kanisa la kipindi cha Matengenezo ni kanisa la Sardi. Angalia Mungu alichosema kwa kanisa hili:-

> "Na kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika; haya ndiyo anenayo yeye aliye na hizo Roho saba. Najua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa. Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa. Maana sikuyaona matendo yako kuwa yamekamilika mbele za Mungu wangu. Basi kumbuka jinsi ulivyopokea na jinsi ulivyosikia, yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako. Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja nami hali wamevaa mavazi meupe kwa kuwa wamestahili. Yeye ashindaye atavikwa mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake" Ufunuo 3:1-5.

Kwa mara nyinigine zaidi, sura hii hutoa maelezo ya undani zaidi juu ya ujumbe wa kanisa la Sardi. Lakini angalia haya mambo mawili.

"Una jina lakuwa hai, nawe umekufa", Mungu aliwaambia. Kanisa lilionekana kuwa hai: ibada za kudumu, udhibiti wa mambo ya kidini na kisiasa, ukuhani ulioenea kila mahali, utajiri mkuu na majengo yaliyonakshiwa.

Bali kiroho lilishakufa zamani.

Halafu angalia jambo hili: "Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja nami wakiwa wamevaa mavazi meupe kwa kuwa wamestahili."

Wachache wasiyoyatia mavazi yao uchafu. Wanaostahili. Naam, wachache wale wale ambao tumekuwa tukiwafuatilia wakati wote. Wachache waliobaki kuwa watiifu kwa Yesu na ukweli wake kwa namna iwayo yote.

Hawa wachache, bila shaka ni pamoja na watu kama John Hus, Jerome wa Prague, Luther na wengine wengi waliosimama imara kinyume na uongo na kuutangaza ukweli, bila kujali gharama yake. Lakini pia inawaunganisha waumini wote wale ambao hawajulikani katika historia kwa sababu ya kutokuandikwa.

Miongoni mwa hao walikuwa Wahugenoti wa Ufaransa na Uswisi walioitikia msisimko wa mwito wa matengenezo wa Luther na Calvin. Waliamini kwa moyo wao wote kabisa katika msingi wa mafundisho ya wana matengenezo: wokovu kwa njia ya imani, mamlaka ya Biblia, na uwezekano wa kumwendea Mungu moja kwa moja kwa njia

ya Yesu, siyo makuhani wa kibinadamu.

Wakiwa na msimamo mkali katika upinzani wao dhidi ya Kanisa Katoliki na mafundisho yake na vitendo yake, Wahugenoti mara walikumbwa na ghadhabu ya mateso. Vita vya Kidini vya Wafaransa dhidi yao vilianza na mauaji makubwa yalikuwa Machi ya 1562 ambapo idadi isiyojulikana ya Wahugenoti waliuawa.

Ambayo ilikuja kujulikana kama siku ya mauaji ya mtakatifu Bartholomeo ya Agosti 24 hadi Septemba 17 mwaka 1572, mauaji yalianzia Paris na yalienea katika miji ya jirani na kusababisha vifo vya watu wapatao 70, 000 ambao walikuwa Wahugenoti. Mateso yaliendelea dhidi yao hadi mwaka 1598, wakati ambapo Henry IV, mfalme mpya wa Ufaransa, alipotangaza uhuru wa dini na siasa, lakini katika maeneo yao tu.

Katika miaka ya 1600, Wahugenoti wengi walihamia Afrika ya Kusini pamoja na majimbo kumi na tatu ya Amerika ya Kaskazini. Miongoni mwa hawa alikuwa sonara aliyeitwa Apollos Rivoire, ambaye alimpa mtoto wake jina la kiingereza na la ubingwa, Paul Revere – Mmarekani mwana mapinduzi mashuhuri.

Leo tunaposoma sura hizi, tunafurahia wasaa wa kuishi na kufundisha imani yetu katika hali ya uhuru kamili. Lakini pia tunaishi katika ulimwengu ambao unabadilika siku kwa siku mbele ya macho yetu. Ulimwengu ambao uhuru wa mtu binafsi unaendelea kuwa hatarini katika huduma za usalama wa kitaifa.

Hatutaendelea kuwa na uhuru tuliofahamu siku za

nyuma ambao tunadhani ni wa kawaida tu. Wakati unakuja tena, upinzani hata mateso yataamka tena.

Je, tutakuwa miongoni mwa waaminifu wachache tena?

Njia bora ya kujua jibu hilo sasa ni kuwa na uhakika wa uaminifu wetu sasa. Je, imani yetu imejengwa katika kanuni na kujitoa, au ni jambo ambalo tunafanya wakati upepo unapo kuwa mzuri (hali inayofaa)? Je, utii wetu umejengeka juu ya kweli yote? Yesu alisema, "Mimi ndimi njia, na kweli na uzima" – Yohana 14:6

Kama tukipenda kweli, tutapenda kweli. kama tu watii wa kweli – tutakuwa watiifu kwa kweli

Swali la kufungia sura hii: Je, tutaogopa uwezekano wa mateso? Au kama yakija kama yatakavyo kuja – je, tutakuwa radhi kuikaribisha hiyo fursa na kusimama na kuwa waaminifu kwa Yesu kama tunuku la heshima kuu ipitayo fadhila?

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 10

# Kutoka Kwenye Majivu Kwenda Kwenye Ushindi

Haidhuru mbio za kupokezana kijiti ni ndefu kiasi gani – haidhuru wakimbiaji ni wengi kiasi gani – jambo moja linalobaki ni lile lile kutoka mwanzo hadi mwisho, ni KIJITI.

Kutoka mkimbiaji wa kwanza hadi wa mwisho, kijiti kimekwenda kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Kwanza kimepita kutoka kwa Adamu, kijiti kimechukuliwa kutoka karne nyingi na urithi wa waaminifu – na kitafika salama wakati mbio ndefu zinaisha wakati wa kurudi kwa Yesu mara ya pili.

Kijiti? Hii ni habari Njema ya Kweli, Yesu Kristo – na ukweli wake: alioshuhudia kwa ulimwengu wakati wa maisha yake hapa duniani na ambao anaendelea kushuhudia katika neno lake.

Kutoka karne hadi karne kijiti kilipitishwa:

- Kutoka kwa Adamu na wazee wa imani wa agano la kale...hadi Israeli na manabii wake.
- Kutoka Israeli...hadi kanisa la kwanza la Kikristo.
- Kutoka kanisa la kwanza...hadi kanisa katika kipindi cha Giza kuu.
- Kutoka kanisa nyikani...hadi viongozi mashujaa wa

Matengenezo
- Na kutoka kwa wanamatengenezo...hadi viongozi wa Maandalizi makuu ya kuja kwa Kristo Mara ya pili.

Matengenezo ya Kiprostestanti yalirudisha ukweli uliokuwa umesahaulika kwa muda mrefu sana na kupuuzwa kwa makusudi, ukweli ulirudi katika nuru ya mchana. Ukweli huu uliweka wazi kanisa lililokuwa limeuzwa kwa adui mkuu, makosa na uongo uliokuwa umechukua mahali pa ukweli – na kuwatesa wale ambao walikataa kujitoa kuwa watiifu kwa wanadamu badala ya Mungu.

Watu waliojitoa wakfu walisaidia kubeba kijiti cha ukweli wakati wa Matengenezo na kuupeleka mbele; watu kama Luther, Zwingli, Calvin na Malanchthon. Bali pia maelfu ya waaminifu wanaume na wanawake ambao majina yao hayafahamiki na mtu ye yote walifanya hivyo pia.

Somo la barabara zilizochimbwa chini kwa chini, litatuwezesha kuelewa vizuri mada itakayo fuata muda si mrefu. Mpaka sasa barabara iliyojengwa ya chini kwa chini, na iliyo ndefu kuliko zote duniani ni ile ya Seikan nchini Japan. Barabara hii inatoka katika visiwa vya Honshu hadi Hokkaido. Hii ni njia ya reli yenye urefu wa maili 31. Barabara nyingine ya namna hiyo imejengwa huko nchini Switzerland, ambayo inaitwa Gotthard. Barabara hii, inatarajiwa kumalizika mwaka 2012, na itakuwa na urefu wa maili 35 ambayo ni sawa na kilometa 56!

Fikiria unaingia kwenye barabara iliyoko chini ya

ardhi, ambayo ni kama kutoka mji wa Chicago – mkoa wa Illinois nchini Marekani – na unaendeshwa mpaka mji wa Miami huko mkoani Florida, Marekani – umbali wa maili 1,186 – bila kutoka kwenye barabara hiyo. Fikiria barabara ya chini kwa chini yenye urefu wa maili 1,260. Barabara yenye giza, ya hatari, yenye adha na kona kali nyingi na kundi la waporaji na majambazi, wakiwemo vilevile wahuni wasiofuata taratibu yo yote.

Katika mwaka wa 538 wafuasi wa kweli ya Mungu, waliingia kwenye barabara ya chini kwa chini sio katika maili au kilomita bali katika miaka. Barabara yenye usengenyaji na mateso yaliyofanywa na kanisa tawala lenye kukengeuka la Kiroma. Barabara hii kihistoria inayojulikana kama Zama za Giza. Watu wa Mungu walitegemea neno la Mungu pekee, kuangaza njia.

Katika mwaka 1798, nguvu za upapa zilifikia mwisho wakati papa wa Roma alitekwa na jenerali Berthier – tukio ambalo limeelezwa katika kitabu cha Ufunuo 13:3, kama jeraha "kuu."

Kutoka mwaka 1517, wakati Luther alipobandika hoja zake 95 katika ubao wa mlango wa kanisa la ngome ya Wittenberg, hadi mwaka 1798, matengenezo yalisonga mbele – wakati wa kurejesha ukweli uliopotezwa na kunyanyaswa kwa muda mrefu.

Pamoja na Matengenezo kupoteza ari yake katika mchanga wa taasisi na madhehebu, watafutaji wanyenyekevu wa mabara yote mawili ya Ulaya na Marekani waliendelea kufanya utafiti wa Neno la Mungu na

kupata ukweli zaidi.

Na ukweli mkuu uliibuka kutokana na utafiti huu, uliibuka katika wakati mwafaka. Kwa kipindi kifupi tu cha miongo minne, vuguvugu kuu lilisomba ulimwengu wote wa kidini, likisisitiza juu ya habari ya kuchangamsha sana kutoka kwenye neno la Mungu kuwa kurudi kwa Yesu mara ya pili kumekaribia.

Kuvuka bahari ya Atlantiki kutoka Ulaya hadi Marekani, makumi ya wasomi wa unabii walifikia uamuzi sawa, na Vuguvugu Kuu la kurudi kwa Yesu mara ya pili liliyakumba makanisa kwa matokeo ya kushangaza.

Nchini Marekani, mhusika mkuu wa vuguvugu hili, hakuwa msomi aliyefundishwa kutoka Seminari, na wala hakuwa mchungaji mhubiri maarufu wa kanisa la mjini. Bali alikuwa, kwa hakika, mtu aliyeanza safari yake ya kiroho mwenyewe, akiwa mtazamo finyu juu ya Mungu – au angalau upeo mdogo kuhusu Mungu.

### *Kijana Asiyeamini Ufunuo wa Neno la Mungu (Deist)*

Alizaliwa katika nyumba ya Kikristo, William Miller kama kijana aliacha imani yake ya awali kwa ajili ya imani ya uungu bila kuamini ufunuo wake –falsafa ya dini inayoamini kwamba Mungu ni kama tajiri mwenye nyumba anayekaa mbali na nyumba yake, kwamba aliumba ulimwengu na akauacha ujiendeshe kama saa. Mungu wa namna hii, falsafa hii inasema, hahusiki yeye binafsi na mambo yanayohusu uumbaji wake na bila shaka hafanyi miujiza yo yote.

Nyakati zote ambazo mjomba wake na babu yake, ambao wote wawili walikuwa makasisi wa kanisa la kibaptisti walipomtembelea kumshuhudia kuhusu imani, yeye baadaye alitumia hotuba zao kama dhihaka za kuwaburudisha rafiki zake.

Lakini baada ya kunusurika na kifo akitumika katika vita vya mwaka 1812, William alianza kuangalia upya imani yake. Aliporudi katika jimbo lake la New York – mahali alipokulia katika mji wa Low Hampton alipata utalaam wa kilimo, kazi ambayo waliowengi (9 kwa kila watu 10) ya wakazi wa Marekani kwa wakati huo walifanya. Mashaka juu ya imani yake yaliongezeka na njaa kwa ajili ya kuwa na amani na Mwokozi wake binafsi ilikua zaidi.

Kwa kuchunguza Biblia alimkuta Mwokozi aliyekuwa akimtafuta. Na sasa kama alivyokuwa akiwadhihaki mjombaye na babuye baada ya kumtembelea, rafiki zake wasioamini walimdhihaki yeye, wakimwakikishia kwamba Biblia imejaa maelezo yanayopingana yenyewe.

"Kama Biblia ni neno la Mungu," aliwajibu hivyo kila kitu kilicho ndani yake kinaweza kueleweka, na sehemu zake zote zinapatana. Nipe muda na nitazipatanisha sehemu zinazo onekana kuhitilafiana, au nitaendelea kutoamini ufunuo wake (Deist).

### *Biblia na Itifaki*

Kama Mwadventista, unajua vizuri kilichotokea baada ya hapo. Miller aliviweka kando vitabu vyote alivyokuwa navyo isipokuwa Biblia na Itifaki ya Cruden, na kutoka

Mwanzo 1 akaanza kutafuta njia yake kwa kupitia Neno la Mungu. Alikusudia kutokwenda mbele haraka zaidi ya vile ambavyo angeweza kutatua matatizo au maelezo yaliyoonekana kupingana aliyokutana nayo. Utaratibu wake ulikuwa ni kufanya Biblia ijieleze yenyewe.

Moja baada ya jingine, maelezo yaliyo onekana yanapingana yaliisha. Na sura baada ya sura, Miller alikuta kwamba urafiki kati yake na Yesu unaongezeka nguvu na kuimarika.

Fungu baada ya fungu, aliendelea mbele hadi siku moja, alifika kwenye fungu lililokamata usikivu wake maishaini – na akaanzisha vuguvugu ambalo vivyo hivyo lilikamata usikivu wa taifa changa la Marekani lenye watu milioni kumi na saba tu kwa wakati huo.

Daniel 8:14: "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa."

Miller alianza kutumia muda wake mrefu sana kwa ajili ya kujifunza Biblia, wakati mwingine alijifunza usiku kucha. Alilinganisha andiko na andiko, hatimaye akagundua kwamba katika wakati wa unabii, siku kibiblia inasimamia mwaka. Hivyo siku 2,300 ilikuwa ni sawa na miaka 2,300. Kujifunza zaidi juu ya Danieli sura ya 8 na ya 9, kulimwezesha Miller kufikia uamuzi kwamba 2,300 ilianza mwaka 457 K. K. Ambayo ilimaanisha, alifanya mahesabu kwamba ingeisha mwaka 1843 – miaka michache; miaka ishirini na tano baadaye.

Kwa upande wa mada ya kutakaswa kwa hekalu, Miller alifikia uamuzi kwamba ilikuwa ni kuja kwa Yesu Kristo

mara ya pili hapa duniani. Ndani ya moyo wake kabisa, alisikia sauti ikisema, “Nenda ukawaambie walimwengu.”

Kwa muda wa zaidi miaka mitano, Miller aliutumia muda wake mwingi kuchunguza kwa undani zaidi kile alichokuwa amekigundua – kwa kuangalia kwa makini na kuangalia kwa makini maamuzi yake. Wakati miaka hii ya utafiti ilipoondoa mashaka yake yote, kipingamizi kipya kilizuka, woga wa kuongea hadharani. Kwa muda wa miaka nane, Miller alishindwa kuitikia wito mkuu uliomjia moyoni mwake – kushuhudia alichogundua kwa njia ya kuhubiri. Lakini sauti ndani ya moyo wake, alijawa msisitizo mkubwa wa kuhubiri.

Hivyo Jumamosi moja asubuhi, Miller alifanya makubaliano na Mungu kwamba kwa hakika angetoa kipingamizi. “O Bwana; alisema, “nitafanya agano na wewe. Kama ukimtuma mtu kwangu mwenye mwaliko wa kuhubiri juu ya mambo haya ndipo nitakapokwenda.”

Kwa unafuu mkubwa, Miller alitulia kwenye kiti chake. Hapakuwa na mtu ambaye angemwomba mtu wa miaka 50, tena mkulima asiye na elimu kuhubiri juu ya kuja kwa Yesu mara ya pili.

Si sahihi. Mtu fulani alikuwa amejitayarisha!

Ndani ya dakika thelathini, mtu alibisha kwa kugonga mlangoni mwake kwa nguvu kumwamsha Miller. “Shikamoo, mjomba William” kijana alisalimia akiwa mlangoni.

“Mpwa Irving!” Miller alishangaa. “Imekuwaje umefika hapa asubuhi hii kutoka nyumbani hadi hapa maili kumi na sita?”

Mjomba William, niliondoka nyumbani kabla ya kifungua kinywa kuja kukuambia kwamba mchungaji wa Dresden hawezi kuhubiri katika huduma ya kesho. Baba amenituma nije nikuombe: Anakuhitaji uje kuzungumza nasi juu ya mambo ambayo umekuwa ukijifunza katika Biblia juu ya kuja kwa Kristo mara ya pili. Utakuja?

### *Kuhangaika Katika Kimsitu cha Maple*

Miller aligeuka ghafla bila kusema neno, akamwacha Irving amesimama na kuchanganyikiwa, na kutoka nje ghafla kwenda kwenye kimsitu cha maple. Pale kwa muda wa saa nzima aliposhindana na Mungu kwa nguvu nyingi kama Yakobo alivyoshindana na Malaika wa Agano la Kale.

William Miller alichukia kwa ajili yake mwenyewe kwa kufanya Agano na Mungu. Alikuwa pia ametishika. Aliomba na kumsihi Mungu amtume mtu mwingine. Lakini hatimaye baada ya machozi na maumivu makali alijitoa kwa Mungu – na kujitoa kulimletea amani na furaha. Hivyo sasa Miller alikuwa amejawa na roho, akaanza kurukaruka, akimsifu Mungu kwa sauti kuu, binti yake mdogo Lucy Ann, akiangalia kwa mashaka kutoka mlangoni, alikimbia nyumbani. "Mama, mama – njoo haraka!

Muda si mrefu Miller na Irving walishika njia kwenda Dresden. Hivyo alikwenda Dresden kwa watu waliomsihi Miller ahubiri kila usiku kwa wiki nzima.

Kutoka mwanzo, mwaliko mwingine ulikuja kutoka kwa watu waliosikia ujumbe wake Dresden. Karibuni kutoka kila madhehebu ya dini, maombi ya haraka yalikuja kwake kama

maporomoko makali sana.

Kila mahali alipohubiri Miller, uamsho ulifuata. Miji yote ilibadilika kwa ajili ya ujumbe wake wa kushangaza wa kwamba kuja kwa Yesu mara ya pili kulikuwa karibu mno. Kwa miaka nane, Miller alikuwa na shughuli ya kuhubiri kila wakati katika miji midogo. Baadaye, karibu na mwisho wa mwaka 1839 baada ya mkutano Exeter, New Hampshire, alikutana na kijana ambaye angebadili huduma yake.

Joshua V. Himes alikuwa na umri wa miaka 34 tu, lakini alikuwa tayari anafahamika sana kwa ajili ya kupinga hadharani utumwa, pombe na vita. Baada ya huduma ya Exeter, Himes alijitambulisha mwenyewe na kumwalika Miller ahubiri katika kanisa dogo la Himes katika mtaa wa Chardon, Boston katika jimbo la Massachussetts.

Tarehe 8, Decemba, mwaka 1839 Miller alihubiri mfululizo wa mahubiri yake ya kwanza katika mji mkubwa wa Marekani. Hata pamoja na kuwa na huduma mbili za ibada kwa siku, mamia ya watu hawakupata nafasi ya kuingia ukumbini.

Siku moja usiku Himes alimwuliza Miller. "Je, unaamini kweli ujumbe ambao umekuwa ukituhubiri?"

"Hakika nina amini ndugu Himes, la sivyo nisingekuwa nahubiri."

"Unafanya nini kwa ajili ya kueneza ujumbe huu ulimwenguni?"

Miller alipojitetea kwamba amefanya kila alichoweza kufikia kila mtu katika miji midogo na katika kila kijiji alichoalikwa. Himes alipigwa na butwa. Kila mji mdogo

na kijiji? Vipi kuhusu miji mikubwa? Vipi Baltimore, New York na Philadelphia? Vipi kuhusu raia wote wa Marekani wapatao karibu milioni kumi na saba.

“Kama Kristo anakuja miaka michache ijayo kama unavyo amini,” Himes alisema, “hivyo hakuna muda wa kupoteza, injili inapaswa kuhubiriwa kwa sauti kuu kuwaamsha watu kwa ajili ya maandalizi.”

Himes akiwa na moto wa njozi kwa ajili ya kile kinachotakiwa kufanyika, akawa msaidizi, mwanamipango na msimamizi wa mipango. Baada ya muda mfupi alikuwa amefanya mipango kwa ajili ya Miller kuhubiri katika miji mikuu nchini, na kwa muda mfupi jina la Miller lilijulikana kila mahali.

Himes aliwasihi wachungaji wa madhehebu yake, Christian Connexion kuruhusu mimbari zao zitumike kwa ajili ya mafundisho ya Miller. Katika mmojawapo ya makanisa haya, ujumbe wa Miller uliwafikiwa familia ya Robert Harmon – na hivyo ilimfikia pia binti yao Ellen, mwasisi wa baadaye wa kanisa la Waadventista Wasabato ambaye alitoa maisha yake kwa ajili ya matumaini ya marejeo ya Kristo.

Kama moto wa porini vuguvugu lilisambaa. Himes kwa bidii alianza kuchapa ujumbe uliounga mkono ujumbe uliokuwa unahubiriwa na Miller. Wachungaji wengine pia waliunga vuguvugu kuongeza juhudi zao. Josiah Litch, Mmethodisti, alichapa kitabu chenye kurasa 200 juu ya mahubiri ya Miller. Litch pia alisaidia kumshawishi Charles Fitch, mchungaji wa Congregationalist wa Boston, kuunga

mkono. Litch na Mmethodisti mwengine mashuhuri, Apollos Hale, walitengeneza kile kilichokuja kujulikana kama chati ya 1843, ufupisho wa muda wa unabii uliojengwa juu ya ujumbe wa Miller.

Vuguvugu la Miller lilikuwa limekuwa sana zaidi ya kuongozwa na mtu mmoja. Vuguvugu kuu la kuja kwa Yesu mara ya Pili lilikumba Amerika ya Kaskazini kama tsunami (mafuriko ya bahari) kupitia makanisa. Mikutano ya makambi ya mikutano mingine ilivuta maelfu ya watu.

Kwa muda mrefu Miller alikuwa anaepa kusema siku hasa ya kurudi kwa Kristo, ujumbe wake ulieleza tu kwamba Yesu angeweza kurudi yapata mwaka 1843." Lakini kufikia mwezi wa Kwanza mwaka huo, alifikia uamuzi, ulijengwa juu ya utafiti zaidi – na kwa kuzingatia kalenda ya mwaka wa kiyahudi, Yesu angerudi wakati fulani kati ya Machi 21, 1843 na Machi 21, 1844.

Mwaka mzima ulipopita, na Yesu hajarudi bado, masikitiko makuu yalikumba vuguvugu. Bali mwishoni mwa mwaka 1844 – katika kambi la Exeter, New Hampshire Agosti vuguvugu lilipata nguvu mpya kutokana na ugunduzi uliofanywa na mchungaji wa Millerite aitwaye S.S. Snow. Kujifunza kwake kwa unabii wa Danieli wa siku 2,300 ulimwongoza kufikia uamuzi kwamba Yesu angerudi siku ya kumi ya mwezi wa saba wa Kiyahudi, ambao katika mwaka 1844 ingeangukia tarehe 22 mwezi Oktoba – miezi miwili tu baadaye.

Nguvu mpya ilichochea mlipuko wa shauku. Watu waliondoka kwenye mkutano wa makambi kwenda kueneza

neno. "Tazama Bwana Arusi anakuja!" Muda mfupi Miller, Himes na viongozi wengine wa vuguvugu walikubali kwamba dhana ya Snow juu ya kurudi kwa Yesu kwa hakika ilikuwa ya kweli.

Tarehe 22 Oktoba, 1844 makumi ya maelfu ya waumini walikuwa wakisubiri kutokea kwa Bwana wao. Lakini siku ilipokuja na hatimaye kupita, masikitiko makuu ya pili yaliwapondaponda na machungu sana kiasi cha kutotamkika.

Tarehe 24 Oktoba, Litch alimwandikia Miller, "Ni siku ya huzuni na utusitusi hapa – kondoo wanatawanyika – na bwana hajaja bado."

### *Matokeo ya Baadaye*

Baada ya Masikitiko Makuu, baadhi ya waumini walipoteza matumaini yote na wengine kuacha vuguvugu la kidini, au ukristo wao – au vyote viwili. Baadhi walifikia kwenye uamuzi kwamba hakuna cho chote kilichotokea tarehe 22 Oktoba – kwamba walikosea kabisa kufafanua maandiko. Wengine waliamua kwamba Yesu alikuja tarehe 22 Oktoba, lakini alikuwa amekuja kwa namna ambayo hawezi kuonekana, kuja kwa kiroho. Lakini baadhi walidumu kwa muda mrefu katika masononeko yasiyofarijika. Na baadhi yao, japo wachache, waliendelea kuomba na kufanya uchunguzi, wakiwa wameshawishika kwamba – kwa namna fulani walikosea kitu fulani katika kuelewa kwao kwa Biblia.

Kama kila Mwadventista anavyojua sasa, kutoka katika

kundi hili la mwisho iliibuka idadi ndogo ya wanafunzi waaminifu wa Biblia waliofikia kwenye uamuzi kwamba kwa kweli kuna jambo lililotokea tarehe 22 Oktoba, 1844 tofauti na kuja kwa Yesu mara ya pili, kilichotokea ilikuwa ni kuingia kwa Yesu katika Patakatifu pa patakatifu katika hekalu la mbinguni, kuanza huduma yake ya mwisho ya maombezi.

Watu kama Hiram Edson, O.R.L. Grosier, na F.B. Hahn walisema kwamba hekalu iliyopaswa kutakaswa sio ya duniani – bali hekalu ya mbinguni.

Baada ya muda mfupi wengine waliwaunga watu hawa katika kujifunza na kujiunga katika uamuzi wao. Miongoni mwao ni kijana mkristo mchungaji wa Connexion aitwaye James White; binti wa familia ya Harmon – Ellen Harmon na sasa mke wa James White na kepteni mstaafu aitwaye Joseph Bates.

Kutoka katika majivu ya masikitiko ya uchungu, lilitokea vuguvugu ambalo liliendeleza vuguvugu la kuja kwa Kristo mara ya pili zaidi ya uwezo wake wa kwanza. Kutoka kwenye machozi ya kukata tamaa na kuibuka jambo lenye uhakika juu ya Neno la Mungu ambalo lingefanya watu kuibuka wanaowajibika kutoa wito wa mwisho na muhimu kwa ulimwengu kwamba kuja kwa Yesu kulikuwa ni hakika na karibu sana!

Katika makanisa saba ya Ufunuo, kanisa lililoendelea kutoka kwenye Matengenezo hadi vuguvugu la kidini la kuja kwa kristo mara ya pili lilikuwa kanisa Philadelphia – kanisa la "upendo wa kindugu." Lakini watu wa Mungu

walipoanza kuamka – waliitwa kutoka nje ya Babeli ya machafuko ya makanisa mengine – kanisa la saba na la mwisho lingefuata: kanisa la Laodekia. Na Mungu alikuwa na maonyo makali na makaripio kwa kanisa hili, kama tutakavyoona katika sura inayofuata.

Je, kuna mwendelezo wa waaminifu wa Mungu? Hasa wakati wa miongo ya vuguvugu kuu la kuja kwa Kristo mara ya pili, iliwahusisha viongozi kama Miller, Himes na Fitch – na baadaye Edson, familia ya White pamoja na Bates. Naam, kama kawaida, ilihusisha pia mashujaa wengi waaminifu ambao majina yao hayakutajwa, wale waliokuwa wanyenyekevu kwa – UKWELI – bila kujali lo lote.

Mbio zimekuwa ndefu. Kutoka kwa Adamu na kuendelea, kijiti kimekuwa kikipokelewa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Katika vuguvugu la Kiadventista, kijiti kinaletwa sasa hivi katika mikono yangu, na yako.

Kijiti hicho kipo katika mikono yako, rafiki yangu – hivyo kishikilie sana. Kimesafiri kutoka mbali. Katika kijiti hicho kuna alama za Adamu, Nuhu, Danieli, Yusufu, Danieli – Stefano, Paulo, Petro, na Yohana – ya Wawaldensi, Waalbigensia, na Wahugenoti – ya Luther, Calvin, Zwingli na Wycliffe – ya Miller, Himes, Edson na White. Sasa kitakwenda wapi kijiti hiki kutoka mikononi mwako?

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 11

# Mashujaa Wa Ukweli

Je, umewahi kupotea ukiendesha au hata kutembea kwenye mitaa ya jiji kuu?

Sasa, kwa ukamilifu njia ya kupata eneo lako ingekuwa ni kupaa kimuujiza juu angani kiasi cha kutosha, ili uangalie kwa chini eneo kubwa zaidi na kuona mahali ulipo na pale unakotaka kwenda. Lakini kuelea angani ili kupata ufahamu wa mahali ulipo kimatendo si jambo halisi.

Lakini hakuna shida kama unaishi Marekani, Ulaya, Australia-au sehemu nyinginezo za dunia ambapo una GPS mpya ya kisasa kwenye gari lako au mkononi. Ukiwa na GPS (global positioning system), huhitaji kupanda juu angani, kwa sababu mifumo ya setilaiti tayari iko huko juu—juu kiasi cha kilomita 19,200, kwa hakika—na kupima kwa njia ya pembetatu au kubadilishana mawazo zenyewe kwa zenyewe, zinaweza kuona kwa hakika mahali ulipo.

Ukiwa na GPS mkononi au ndani ya gari lako, siyo kwamba unaweza kuona tu kwenye kioo mahali ulipo lakini pia unaweza kupata mwelekeo wa kule unakotaka kwenda. Kwa mtu ye yote mwenye changamoto ya kutojua mahali alipo au anakotaka kwenda GPS inaweza kuwa ni mbaraka halisi!

Wakati mwingine, inawezekana kupotea hata katika kusoma kitabu, unaweza kugeukia kushoto katika mada fulani na kulia katika mada nyingine, halafu ukasafiri kilomita nyingi katika mfululizo wa aya na sura, na ukawa kama umechanganyikiwa hujui ulianzia wapi na unakwenda wapi.

Hivyo pengine ni wakati mwafaka sasa kusimama kwa kitambo na kupata ufahamu wa mahali tulipo sasa. Hebu turejee tulipoanzia, tulipokwenda na ambako bado tunakwenda.

Tulianza kitabu hiki kwa kujulishwa kwamba kusudi lake ni kusimulia kisa – kisa cha waaminifu wa Mungu katika karne zote. Waaminifu hawa wamekubali ujumbe pekee kutoka kwake – kuwa watetezi wa ukweli.

Na huu ukweli ni wa aina mbili. Unaunganisha ukweli wote ulioshuhudiwa na Mungu katika neno lake na ukweli wote uliofundishwa na hata kupitia vielelezo vya maisha ya Yesu hapa duniani. Lakini sehemu moja ya huu ukweli wote ni ya muhimu sana kuliko sehemu nyingine – ukweli kuhusu tabia ya Mungu.

Adui mkuu anasema kwamba Mungu hawezi kuaminika – kwamba husema uongo, anadai mambo yasiyowezekana, ni wakuhukumu, analipiza kisasi, na amekusudia kuondoa uhuru wetu na kuangamiza furaha yetu. Adui anasema kwamba Mungu anahusika na mateso, mikasa na vifo katika sayari ya dunia – kwamba anapaswa kulaumiwa kwa mabaya yanapotupata katika maisha yetu. Adui anasema kwamba kama angekuwa mtawala wa

ulimwengu, kila mtu angepata furaha kamili.

Hata viongozi wengi wa Kikristo leo wana mwakilisha Mungu ulimwenguni, kama Mungu anayetamani kufanya hukumu na kuangamiza wale walio tenda dhambi.

Hivyo kila wimbi kubwa la maji ya kupwa na kujaa (tsunami) au tufani au tetemeko linapoangamiza maelfu ya maisha ya watu, wengi husema, lazima iwe kwa sababu Mungu amewakasirikia wadhambi na hivyo basi, anavurumisha hukumu zake duniani.

Na adui anachukuwa hatua zaidi kwa kusema, sio tu kwamba Mungu anawaangamiza watu kwa ajili ya kutotunza amri zake, bali anafanya hivyo akiwa anajua kwamba hawawezi kutunza – kwa vile amezifanya amri zake kuwa ngumu kiasi cha kutotunzwa.

Mungu anafananaje hasa? Ni Mungu wa upendo –au ni Mungu mwenye hukumu kali na uangamivu? Je, alitunga sheria akijua kwamba hakuna mtu anayeweza kutunza – halafu kuwahukumu kifo wanaposhindwa kushika sheria hiyo? Je, anashikilia mkononi mwake chakula cha kimbingu mfano wa Karoti na uzima wa milele kama zawadi kwa ajili ya tabia njema, ili tu kutumia fimbo ya adhabu tunapokuwa na tabia mbaya? Anapotuomba tumpende, je, ukichagua kutokumpenda inakuaje?

### *Bandia*

Kwa kila ukweli ambao Mungu ameshuhudia kwa wanadamu aliowaumba adui ametengeneza ukweli bandia. Dhambi ni mbaya sana. Mungu alitoa maonyo. Kaa mbali na

dhambi – itakuua. Shetani naye akasema, Sio hivyo! “Hakika hutakufa.” Hasha, baada ya kufa, nafsi yako inaendelea kuishi. Bado unaendelea kuishi – ila tu katika mfumo mwingine kama vile mbwa, paka n.k.

Siku ya saba ni Sabato, Mungu alisema. Sio hivyo, Shetani naye akageuza. Ni Jumapili siku ya kwanza ya juma. Yesu akija kwa mara ya pili kila jicho litamwona, Biblia inatuambia. Sio hivyo, Shetani anasema. Yesu atakuja kwa siri, kwenye unyakuo, na wachache tu watamwona.

Uongo unaendelea na kuendelea. Kwa nini? Kwa sababu uasi wa Shetani dhidi ya Mungu ulikuwa mkamilifu kiasi kwamba hawezi tena kusema ukweli. Anaweza tu kusema uongo. Kwa kuwa kila ukweli ambao Mungu amewahi kushuhudia kwetu, Shetani ana uongo ambao umekuwa ni mafundisho yanayokubaliwa na watu wengi hata wakristo wa dunia hii. Lakini Shetani haachi kusema uongo tu kuhusu kile alichotufundisha Mungu, kwa hakika anapenda zaidi kusema uongo kuhusu jinsi Mungu alivyo.

Bali kutoka mwanzoni, Mungu amekuwa na watu waliokataa kukubali uongo wa adui – hata unapofundishwa na wale wanaodai kuwa wafuasi wa Mungu. Kutoka mwanzo amekuwa na wafuasi waaminifu wasiopigania tu ukweli ambao Mungu aliwashuhudia kabila za wanadamu, bali yule Kweli ambaye Mungu amewashuhudia kabila za wanadamu – yule aliyejiita “Njia, Kweli na Uzima.”

Yesu alipokuwa hapa, alisema, “Yeye aliyeniona Mimi amemwona Baba” (Yohana 14:9). Yesu ambaye ndiye kweli, alikuja sio tu kushuhudia ukweli kwetu – bali pia

kushuhudia ukweli kuhusu Baba yake.

- Adamu na mashujaa wa imani walipigania ukweli – na Kweli.
- Israeli na manabii wake pamoja na wafalme walipigania ukweli – na Kweli.
- Kanisa la awali lilipigania ukweli – na Kweli.
- Wakizingirwa na mateso na maafikiano, waumini katika karne za mwanzo baada ya mitume walipigania ukweli – na Kweli.
- Wakipigana na kanisa lililoasi, Wana Matengenezo walipigania ukweli – na Kweli
- Wanafunzi wa Biblia baada ya Matengenezo Ulaya na Marekani walizingatia juu ya kuja kwa Yesu mara ya pili na kupigania ukweli – na Kweli.

Halafu ikaja siku ya uchungu wa kukatisha tamaa wakati Yesu hakuja. Bali katika kipindi hicho cha kuhuzunisha sana kiliinuka kile ambacho mwanahistoria Mwadventista aitwaye L.E. Froom, alikiita "vuguvugu la kudura" (destiny) – la mwisho, masalio ya mwisho ya wanyenyekevu wa Mungu waliopigania ukweli – na Kweli.

### *Mfululizo Usiokatika*

Tunapopumzika kidogo katika sura hii kupata ufahamu wa mahali tulipo tunaona kwamba kutoka Edeni na kuendelea, mfululizo thabiti wa waaminifu umeendelea kuwepo karne hata karne hadi sasa. Na tunaona ujumbe wa Mungu kwa wafuasi wa kweli haujabadilika kamwe. Kwa

ukatili na aibu adui mkuu vivyo hivyo, naye ameiga na kutumia kupotosha wengi. Ujumbe wa Mungu unapaswa ushuhudiwe na kupiganiwa sana, kwa bidii na kweli. Ujumbe kumhusu Bwana na Mwokozi wetu sote, Yesu Kristo.

Matengenezo yalifufua ukweli uliopuuzwa na kupotea kwa muda mrefu. Pia ilifungua karne ya makosa, uongo na ugushi. Miongoni mwa zawadi kuu kwa ulimwengu ilikuwa ni msisitizo wa mamlaka ya Biblia – sio taratibu za mwanadamu – na juu ya wokovu kwa imani katika Yesu – sio kwa imani katika jitihada za mwanadamu.

Lakini Matengenezo yalipoteza kasi yake kabla hayajakamilika. Ukweli mwingine muhimu ulikuwa haujarudishwa katika hali yake. Mwamko mkuu wa marejeo uligundua na kupigania ukweli wa kuja kwa Kristo mara ya pili, pamoja na kutoelewa vizuri unabii wa Biblia mwanzoni.

Sasa kama wanariadha wa mbio za kijiti tuligundua hapa awali katika kitabu hiki kwamba kijiti kilikuwa karibu kinapokelewa na mkimbiaji wa mwisho. Mungu alikuwa awaite watu wa mwisho, watu waliosalia kupigania ukweli wake – na kweli yake – katika miaka ya mwisho ya kufunga historia ya dunia. Angempa huyu mkimbiaji wa mwisho kazi muhimu kuliko zote.

Naam, hili kundi la mwisho la waaminifu wa Mungu – hili kundi la masalio wangegundua ukweli mwingi uliopotea au kupuuzwa; Sabato, huduma ya Yesu katika hekalu la mbinguni, asili ya mwanadamu katika maisha na kifo, na ukaribu wa kurudi kwa Yesu hapa duniani.

Bali pia aliwapa wanamasalio wa mwisho ujumbe muhimu sana, ujumbe ambao, ulikuwa hauja shuhudiwa kamwe duniani, ujumbe wa malaika watatu kama unavyopatikana katika unabii wa kitabu cha ufunuo.

Ujumbe huu wa malaika watatu unaopatikana katika kitabu cha Ufunuo 14:6-12 ni wito wa mwisho wa Mungu – na onyo lake la mwisho – kwa mabilioni ya watu wanaoishi katika kipindi cha mwisho wa dunia. Kama Nuhu alivyotoa wito na kuuonya ulimwengu wa wakati wake na kama vile Yohana Mbatizaji alivyotoa wito na kuuonya ulimwengu kabla ya kuja kwa Kristo mara ya kwanza, Mungu ana watu ambao kazi yao na fursa yao ni kutoa wito na kuuonya ulimwengu huu wa mwaka 2009 B.K na kuendelea kwamba karibu sana Yesu anakuja.

Kwa ufupi ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo ni:

1. Injili ya milele, imesisitizwa kwa sababu ya saa ya hukumu
2. Wito wa Mungu kwa watu wake watoke nje ya Babeli ya machafuko ya dini za bandia.
3. Onyo kwamba kukaa kwa muda mrefu katika dini ya uongo kuna hatari ya kupata alama ya mnyama ya adui mkuu.

Naam, kuna maonyo ya muhimu sana hapa. Naam ni lazima kwa wanamasalio wa mwisho wa Mungu kupambanua bayana ukweli katika makosa na mambo ya bandia. Lakini ukumbuke kwamba ujumbe wa malaika watatu unaanza na injili ya milele. Hakuna kitu muhimu

kuliko ujumbe huu. Ni kipaumbele. Kuuambia ulimwengu ukweli kuhusu Mungu – kuubainisha sana kiasi kwamba hakuna anayeweza kukosa kuelewa juu ya maisha na kifo cha Yesu – ndiyo kazi ya msingi kwa wafuasi wa kweli wa Mungu waishio katika kipindi hiki cha mwisho.

> "Kwa wale wote wanaokiri kuwa wakristo," Ellen White aliandika, "Waadventista Wasabato wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kumwinua Kristo mbele ya Ulimwengu" – *Gospel Workers*, p.156.

Vipi kuhusu mafundisho yote na ukweli kutoka kipindi cha masikitiko cha mwaka 1844 hadi leo yaliyopatikana, ama kugunduliwa na kurejeshwa na wanasalio wa Mungu? Karibu na kweli...Je, ukweli si wa muhimu sana?

Kwa nadra sana – Chanzo cha ukweli wote kuhusu nini? Nani amefundisha ukweli huo?

Bali tunahitaji uongozi juu ya makosa makuu mawili: Jambo la kwanza ni kuangalia yanayotuzunguka na kusadiki kwamba kwa yale makanisa mengine hayafundishi ukweli huu bali kwa sasa yanazingatia juu ya Yesu na wokovu, kwamba tunapaswa kuwaachia mafundisho haya, na sisi kutumia jitihada zetu zote katika kushuhudia mafundisho pekee ya kweli ambayo Mungu ametuwezesha kugundua. Kosa la pili ni kuufundisha ukweli huu kana kwamba unasimama wenyewe na hauna uhusiano na mafundisho mengine. Kwa kuwa hakuna ukweli – au fundisho – ambalo ni sahihi au linaweza kueleweka, isipokuwa likionekana

limeunganika na ukweli (Yesu).

Mafundisho yote, ukweli wote, unaanza na kuishia kwa Yesu – kwa jinsi inavyotusaidia tuelewe tabia yake ya upendo. Hekalu sio tu alama na huduma, ni kielelezo kinachoweza kushikwa kuhusu jinsi upendo wa Yesu unavyotuokoa.

Angalau baadhi ya dini za ulimwengu huu zilizokanganyikiwa zinafundisha na kumhubiri Yesu. Bali kwa urahisi sana wanaacha njia sahihi na kufundisha neema rahisi au mtu akishaokolewa, ameokolewa moja kwa moja; au kwamba Mungu amekwishaamua juu ya wale wataokolewa na wengine watakao potea.

Mungu amewapa masalio wake wa mwisho ujumbe ulio wazi zaidi, sawasawa na wa kueleweka sahihi kuhusu wokovu kwa namna ambayo ulikuwa haujafunuliwa kamwe kwa jamii ya wanadamu. Pamoja na hayo ameonyesha jinsi kila fundisho, kila kanuni ya Biblia inavyoeleza juu ya Yesu – jinsi ambavyo kila moja ya ukweli unavyotusaidia kufahamu jinsi Mungu alivyo hasa.

## *Masalio*

Kama Mwadventista – iwe umebatizwa siku za karibuni au ni mshiriki tangu utotoni – labda umeshawahi kusikia neno hili 'MASALIO'. Huo siyo wito wa biashara iliopigiwa kura na kamati fulani ya kanisa. Ni maelezo ya Mungu mwenyewe juu ya wafuasi wake waaminifu wa mwisho.

Angalia Ufunuo 12:17 "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao

wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari."

Joka, Shetani, unabii huu unasema, alimkasirikia "mwanamke" – wafuasi wa kweli wa Mungu, kanisa lake – na akaenda kufanya vita juu ya "masalio ya wazao wake." Masalio: kile kilichobaki. Sehemu ya mwisho.

Na haya masalio, unabii unasema, yanaweza kutambuliwa kwa mambo mawili:

- Wanatunza amri za Mungu,
- Wana "ushuhuda wa Yesu Kristo."

Tutaangalia kwa undani zaidi katika alama hizi mbili za utambulisho wa masalio katika sura inayofuata. Bali kwa sasa, ni tahadhari. Ingekuwa rahisi sana kuhitimisha kwamba kanisa la Waadventista Wasabato – "vuguvugu la kudura" ambalo Dr. Froom aliandika – kuwa ni nyumba pekee ya watu wa kweli wa Mungu – na kwamba kwa kuwa mshiriki wa kanisa hili tu, unaweza kuhakikishiwa wokovu.

Kando na ukweli kwamba Biblia iko wazi kuwa, wokovu haupatikani kwa njia ya kuwa mshiriki wa kanisa ila kwa imani katika Kristo pekee, ukweli ni kwamba hiyo siyo masalio yote ya kweli ya Mungu – wafuasi wake wanyenyekevu – wapo pia katika makanisa mengine kando na kanisa la Waadventista Wasabato.

"Ingawa giza ya kiroho na mfarakano kutoka kwa Mungu juu ya mambo yanayoendelea kuyafanya makanisa mengi kuwa kwenye umoja wa Babeli," Ellen White

aliandika, kundi kubwa la wafuasi wa kweli wa Kristo bado linapatikana katika umoja wao" – *The Great Controversy*, uk. 390.

Je, hii ina maana kwamba kanisa la Waadventista Wasabato siyo masalio? Siyo hivyo hata kidogo. Lakini siyo watu wote wa masalio ya Mungu wako tayari katika kanisa la Masalio. Kwa hakika baadhi ya watu hao wa masalio wamekufa – au wanaweza kufa – kamwe bila kupata nafasi rasmi ya kujiunga na kanisa la Masalio.

Lakini kama Mungu atasema, "Tokeni Babeli" atasema pia "Njoni katika Masalio!" Na haya masalio ni ushirika wa walioitwa kutoka nje – kundi lililoagizwa kuchukua jukumu la kufanya. Mungu hakufanya masalio ili kutoa wokovu kama fadhila ya ushirika. Alianzisha kanisa la masalio kuwa ni mahali ambapo wafuasi waaminifu wa Mungu watakutana pamoja kujifunza namna ya kuunganisha jitihada zao pamoja ili kuwa watetezi wa Mungu – na Yeye aliye Kweli.

Je, umewahi kupambana na kamba mshipi au mpira wa kumwagilia maji bustanini unaonekana kujifungafunga? Unaufunguaje, hatimaye? Unapaswa kutafuta ncha mojawapo – na uanze hapo.

Sisi Waadventista Wasabato tunatumia muda mwingi sana na nguvu wakati mwingi na hata mabishano, kujaribu kufungua mambo. Tunajadili viwango vya kanisa, tu wepesi wa kukosoa theologia, tunapishana hata katika namna ya kutumia kanuni za kanisa, tunachambua mafundisho kwa undani zaidi.

Muda mwingi zaidi ungeokolewa – na tungekuwa na mafanikio makubwa zaidi – kama wakati ambapo vitu vinaonekana kusokotana tungepaswa kurejea nyuma na kutafuta "ncha". Kwa kuwa kila jambo – kila fundisho, kila kiwango cha kanisa, kila tendo la kanisa, linaanza – na kuishia kwa Yesu Kristo. Kama tungeanzia hapo tu na kuishia hapo msokotano ungetoweka. Tungepatana na kila mmoja wetu – na kuacha kuhangaika na mambo madogo madogo.

Tuna kazi nyeti, kazi ya muhimu sana kufanya. Tuna kazi ya kumwinua Mwokozi juu kwa wale wote wanotuzunguka. Tuna ukweli wa kusuhudia. Kuna makosa ya kuwaonya watu. Kuna ujumbe wa kurudi kwa Kristo tunaopaswa kutangaza.

Sio ajali kwamba wewe ni Mwadventista Msabato. Umeitwa kutoka nje na kuteuliwa . Naam, wewe. Mungu amekualika kuchukua nafasi yako katika ukoo mkuu wa waaminifu wake. Amekuomba uchukue kijiti na ukimbie mbio za mwisho za mashindano. Amekuomba kuwa mtetezi kwa ajili ya ukweli – na kwa ajili ya Kweli.

Hivyo nenda darasani leo. Nenda kazini. Fanya matembezi yako ya malengo. Angalia watoto wako. Ishi maisha yako ya kawaida. Lakini uwe tayari kwa ajili ya Mungu leo. Uwe mfereji wake. Uwe ni sauti yake. Uruhusu upendo wa Mungu ububujike kupitia kwako kwenda kwa waliopotea, kuchanganyikiwa na wanaotafuta. Amini juu ya kazi ya uteule wa kiungu ulioitiwa. Uwe tayari kwa ajili ya kushuhudia.

Fikiria jinsi Mungu alivyokupa hadhi, jinsi gani ulivyopendelewa – kwa kuwa sehemu ya vuguvugu lake la majaliwa la mwisho. Kwa kadri tunavyoshuhudia zaidi juu yake na ukweli wake kwa wale wanaotuzunguka ndivyo tutakavyo uona uso wake.

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 12

# Zawadi Isiyofanana Na Zawadi Yo Yote

"Una nini mkononi mwako?" Mungu alimwuliza Musa.

- Fimbo. Fimbo tu ndogo, tena ya mti. Bali kwa kuitumia Musa aliwaokoa Waisraeli.
- Katika mikono ya watu mia tatu Mungu alitumia tarumbeta, mienge, vigae kumsaidia Gidion na jeshi lake kuwashinda Wamidiani
- Katika mikono ya Yesu, mikate mitano na samaki wawili, aliwalisha watu elfu tano.

Siku zote Mungu hutumia vitu vya kawaida, vinyenyekevu, vile vinachoonekana kuwa vinyonge.

Kwa kadri kanisa la Waadventista Wasabato lilivyoanza kujulikana kutoka kwenye majivu ya Masikitiko makuu ya mwaka 1844, Mungu alimtumia kijana wa kike kuwa mjumbe wake mteule kwa ajili ya masalio.

Ellen Harmon – alizaliwa katika mwaka 1827 – alipokea njozi ya watu wa Mungu katika safari yao ya kwenda mbinguni, alipokuwa na umri wa miaka 17. Hii ilikuwa ni njozi ya kwanza kati ya njozi kama 2000 ambazo alizipokea katika kipindi cha maisha yake ya huduma. Katika mwaka

1846, Ellen aliolewa na James White, mchungaji kijana aliyeshirikiana naye katika msimamo wa kwamba Yesu karibu anarudi. Muda mfupi baada ya ndoa yao, James na Ellen pia walikubali ukweli wa Biblia juu ya Sabato ya siku ya saba.

Ellen na mume wake James, pamoja na nahodha mstaafu Joseph Bates, wanakumbukwa kama waasisi wakuu wa kanisa la Waadventista Wasabato, lililoanzishwa rasmi mwaka 1863.

Waadventista wasomaji wanajua kwamba mama White – au "Dada White" kama pia anavyojulikana kanisani – alikuwa mwandishi mkuu aliyeandika zaidi ya vitabu arobaini na makala 5,000 kwenye majarida yanayotolewa kila baada ya kipindi fulani. Tangu alipokufa mwaka 1915, vitabu vingine vingi vimechapwa kutokana na kazi ambazo zilikuwa hazijachapwa na pia kukusanywa kutoka kwenye kazi zake. Leo hii vitabu ambavyo ni zaidi ya mia moja, vinachapwa katika lugha ya Kiingereza, akiwa ndiye Mmarekani mwandishi wakike ambaye vitabu vyake vimetafsiriwa katika lugha mbalimbali kuliko ye yote yule katika kipindi chote.

Wakati wa huduma yake ya muda mrefu, yeye binafsi alikuwa nyenzo ya kuanzisha huduma ya afya, uchapaji na elimu kanisani. Na bila shaka mashauri yake mengi yaliyochapwa yamejengwa juu ya njozi zake – yalisaidia kuliongoza kanisa changa katika miaka yake ya awali, kama yanavyoendelea kuliongoza kanisa hata leo.

Tangu mwanzo, Waumini wa Kiadventista

wanashawishika kwamba Mama White alikuwa na kweli ya Kibiblia ya unabii. Wanaamini pia kwamba Ufunuo 12:17 na 19:10 vinaweka wazi kwamba karama hii ya kiunabii ni mojawapo ya alama mbili za kuwatambua watu wa masalio ya mwisho ya Mungu.

Ingawa Ellen White hakuwahi kudai mwenyewe kuwa nabii badala ya mjumbe wa Mungu, kwa kutumia vipimo vya Biblia vya nabii kwa mama White na maandishi yake, Waadventista wameshawishika kwamba alikuwa na kipaji halali cha unabii.

Kwa ufupi hapa ni ufunguo wa vipimo Biblia inatupa kwa ajili ya kutambua kama mtu anayo au hana karama ya kweli ya unabii:

**1. Kipimo cha Utimilifu wa utabili** – Yeremia 28:9 "Nabii atabiriye habari za amani, neno la nabii yule litakapotokea, ndipo nabii yule atakapojulikana, kuwa BWANA amemtuma kweli kweli."

Kipimo hiki cha Biblia ni lazima pia kizingatie kanuni za masharti ya unabii – kukiri kwamba baadhi ya unabii unategemea utimilifu wake kutegemea mwitikio wa watu wa Mungu. Ni Yeremia pia anayeweka msingi huu.

> "Wakati wo wote nitakapotoa habari za taifa, na habari za ufalme, kung'oa, na kuvunja, na kuangamiza, ikiwa taifa lile nililolitaja litageuka na kuacha maovu yake nitaghairi, nisitende mabaya yale niliyoazimia kuwatenda. Na wakati wowote nitakapotoa habari za taifa, na habari za ufalme, kuujenga na kuupanda, ikiwa watatenda maovu mbele za

macho yangu, wasiitii sauti yangu, basi nitaghairi, nisitende mema yale niliyoyaazimia kuwatendea" – Yeremia 18:7-10.

**2. Kipimo cha kukubaliana na Biblia** – Isaya 8:20 "Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili; bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Katika kipindi cha Biblia – pia baada ya karne kadhaa – unabii wote wa mwanzo ulipimwa, Maandiko Matakatifu ilikuwa ndiyo kipimo ambacho kilitumia kwa kila nabii aliyefanikiwa unabii wake ulipimwa. Ingawa baadaye manabii walitoa nuru mpya katika ukweli wa neno la Mungu, mawazo haya kamwe yasingepingana na ukweli mkuu ambao tayari ulikuwa umefunuliwa na manabii wa mwanzo wa Biblia.

**3. Kipimo cha kuzaa matunda** – Mathayo 7:15-20 "Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua – kwa matendo yao. Je, Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri, na mti mbovu huzaa matunda mabaya, wala mti mbovu hauwezi kuzaa matunda mazuri.... Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua.

Kipimo hiki – hakifanani na vipimo viwili vya kwanza – kinachukua muda, kama vile ambavyo tunda halikui na kuiva mara moja. Bali kwa kadri tabia ya nabii, huduma na ujumbe unapokuwa wazi zaidi, uchunguzi maalum utadhihirisha kama tunda hili ndilo linalotegemewa kuzaliwa na mti wa unabii.

**4. Kipimo cha kushuhudia asili ya uungu na**

**ubinadamu wa Yesu Kristo** – 1 Yohana 4:1-3. "Wapenzi, msiamini kila roho bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu, kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani. Katika hili mwajua Roho wa Mungu; kila roho akiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo ambayo tumesikia kwamba yaja na sasa imekwisha kuwako duniani."

Nabii wa kweli hakiri tu kwamba Yesu aliishi hapa duniani. Nabii wa kweli anakiri na kusema kwamba Yesu alikuwa Mungu kamili – na mwanadamu kamili. Kufanyika mwili kwa Yesu ni kiini cha huduma na ushuhudiaji wa nabii wa kweli.

**5. Kipimo cha chanzo** – manabii wa kweli hawatengenezi unabii wao wenyewe bali huwakilisha kwa watu wengine kile tu kilichofunuliwa kwao na Roho mtakatifu – 2 Petro 1:21: "Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu."

Vivyo hivyo manabii wa kweli hawatoi tafsiri zao binafsi au za kisiri za unabii. "Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani" – 2 Petro 1:20.

Tangu siku za mwanzo kabisa za vuguvugu la kurudi kwa Yesu mara ya pili hadi sasa, mamia, maelfu, na mwishowe mamilioni wamejifunza maisha na ujumbe wa Ellen G. White na kupima huduma yake kwa vipimo hivi

vya Biblia vya nabii wa kweli. Katika kila mwongo, uamuzi umekuwa sawa. Ellen White kwa kweli amedhihirisha katika maisha yake, hotuba zake na maandishi alama za nabii wa kweli.

Lakini vipi, baadhi wanaweza kuuliza, je, maandishi ya Dada White yanahusiana na Biblia? Je, ni nyongeza ya biblia? Kama ni hivyo, jinsi gani wazo hilo linakubaliana na Matengenezo ya kweli ya Biblia – na Biblia pekee?

Katika miaka ya kwanza ya kanisa, Waadventista waliainisha maswali haya. Katika mwaka 1863 mhariri na mwandishi Uriah Smith aliandika makala katika gazeti la kipindi maalum la kanisa – Review and Herald – yenye kichwa kifuatacho: "Je, tunaikana Biblia kwa kukubali njozi," katika makala hayo alisisitiza kanuni hii kuu ya Matengenezo – Biblia – na Biblia pekee.

### *Nahodha wa Bandarini*

Makala ya mzee Smith yalitumia kielelezo cha meli baharini inayoelekea karibu na bandari. Kutokana na kanuni za meli, kabla haijaingia bandarini, chombo kinaongozwa kusimama na kumruhusu nahodha wa bandari kupanda chomboni nahodha anayefahamu udanganyifu wa maji yaliyopo mbeleni.

"Roho ya unabii," aliendelea kuandika akisema, "imetolewa kwa nahodha wetu katika kipindi hiki cha hatari, na popote na katika ye yote tunaona udhihirisho halisi katika hayo, tunalazimika kuheshimu, wala hatuwezi kufanya vinginevyo kwa sasa na kukana Neno la Mungu,

ambalo linatuelekeza kuupokea. Sasa ni nani wanaosimama juu ya Biblia na Biblia pekee?" – *Review and Herald*, Jan. 13, 1863.

Kwa kadri kanisa la masalio linavyokaribia bandarini, Biblia inasema kwamba huyu masalio atapewa "nahodha" – karama ya roho ya unabii – kuliongoza kupitia maji ya hatari ya mwisho wa safari.

Kama hiyo ni kweli ambayo Biblia inasema – na tayari tumeshaona katika ufunuo, nani basi...mzee Smith aliuliza, anaamini kwa hakika katika Biblia na Biblia pekee – Je, ni wale wanao mkubali huyu nahodha au wanao mkataa?

Ellen White mwenyewe kamwe hakuona maandishi yake kama nyongeza kwa Biblia, bali kama nuru ndogo kuongoza katika nuru kuu. Kama Yesu alivyokuja kumdhihirisha Baba, na kama roho mtakatifu anavyomwinua Yesu, maandishi yake ya kiunabii yanainua juu Biblia na kuiheshimu.

Bila shaka, makanisa mengine pia yana manabii wao – au vitabu vilivyovuviwa. Bali kunatofauti kubwa. Mormons – kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho – ambalo liliinuka wakati huo huo ambao kanisa la Waadventista Wasabato lili inuka, vile vile wana kitabu chao cha Mormon na vitabu vingine ambavyo wanaviona kuwa vimevuviwa. Vitabu hivi, vinapewa uzito sawa na kiwango cha Biblia – na kama nyongeza ya Biblia. Hii ni kweli pia kuhusu Apocrypha, vitabu visivyo thibitishwa ambavyo kanisa Katoliki la Roma linaviona kama ni sehemu kamili ya maandishi matakatifu sawa na Biblia yenyewe.

Maandishi ya Ellen White – ambayo Waadventista wanaita maandishi ya “Roho ya Unabii – yanachukuliwa kama miwani ya kukuza au taa yenye nuru kali ambayo inaangaza Biblia ili iwe rahisi kuona na kuelewa ukweli wake.

Kuna tofauti nyingine kuu kati ya Waadventista na makanisa mengine ambayo yanadai kuwa na manabii au maandishi yaliyovuviwa. Kanisa Katoliki kwa mfano huyapa maagizo ya papa na desturi za kanisa uzito zaidi ya Biblia – yanachukua nafasi ya kwanza juu ya Biblia hata kama vyanzo hivi viwili vya ukweli havipatani. Bali Waadventista wanaamini kwamba karama zote na ishara za Roho mtakatifu lazima vithaminiwe na Biblia – na kwamba cho chote kisichokubaliana na Neno la Mungu hakiwezi kukubaliwa.

### *Kwa nini Karama za Kiroho?*

Tutaonaje umuhimu wa Roho ya Unabii kanisani? Makusudi yake nini? Kwa nini Mungu aliona kwamba kanisa linahitaji Roho ya Unabii. Tafakari hayo maswali.

**1. Kama ilivyokuwa kundi dogo la Mungu la waaminifu katika karne kadhaa likipigania ukweli wa Biblia uliopuuzwa na kudharauliwa, Roho ya Unabii inaelekeza nuru katika ukweli ambao Mungu anaurejesha katika siku hizi za mwisho wa historia ya mwanadamu**: Sabato, hekalu, hali ya wafu, kuja kwa Kristo mara ya pili na ukweli mkuu wa haki kwa imani katika Yesu.

Hebu tusikubali kamwe baadhi ya mashitaka ambayo baadhi ya watu wanashambulia Waadventista Wasabato

juu ya mafundisho tuliyo nayo – wakidai kuwa, hawa wamejenga jumla ya ukweli wao – kwa kutegemea kimsingi katika maandishi na njozi za Ellen White.

Kwa mfano ukosoaji wa awali ulidai kwamba fundisho kuu juu ya hekalu la mbinguni ulijengwa na kusimama kimsingi juu ya njozi ya Dada White. Katika mwaka 1874, Mzee Uriah Smith – wakati huu alikuwa mhariri wa gazeti la Review and Herald, alikutana na dai hili katika tahariri:

> "Mamia ya makala yameandikwa juu ya mada hii. Bali hakuna mojawapo kati ya hayo ambayo ni njozi ambazo zilichukuliwa kuwa na mamlaka katika mada hii, au kutoka kwazo. Rufaa ni Biblia isiyobadilika, ambayo ina ushahidi tele kwa ajili ya mtazamo tunaoshikilia juu ya mada hii" – *Review and Herald*, Desemba 22, 1874.

Uchunguzi wa uangalifu wa historia yetu ya awali kama kanisa utaonyesha kwamba maneno yale yale aliyo yaandika mzee Uriah Smith kuhusu ukweli wa hekalu unaweza kutumika katika kweli zote walizo zigundua Waadventista kwa kadri walivyokuwa wakichunguza neno. Mara nyingi, hata hivyo, baada ya wanafunzi Waadventista wa Biblia walipogundua ukweli muhimu wa Biblia kwa kutumia muda mrefu wa kusoma na kuomba ukweli huo ulithibitika kama kweli na muhimu katika njozi iliyowakilishwa kwa Dada White. Na katika miaka iliyofuata, maandishi ya Dada White yaliinua, heshimu na kusistiza umuhimu wa ukweli huo.

**2. Roho ya Unabii ni ya thamani sana kwa Waadventista katika ujumbe wao kuuambia ulimwengu juu ya ukweli kumhusu Mungu na tabia yake ya upendo**. Katika pambano kuu baina ya Yesu Kristo na Shetani, adui amejitoa mwenyewe kushambulia tabia ya Mungu. Siku zote wafuasi wa Mungu wa kweli wamekuwa na fursa ya kuutetea na kueleza ukweli kuhusu Mungu anayetawala ulimwengu alivyo hasa. Na kwa kadri Pambano kuu linavyo elekea kufikia mwisho wa vita, ujumbe huo – ambao kwa sasa ni kazi ya masalio – haijawahi kuwa wa muhimu na wa maana kama ilivyo sasa.

Mungu sio mwanzilishi wa mateso, mauti na mateso.

Mungu sio mwangamizaji.

Mungu sio jaji mlipiza kisasi anayetuvizia atushike tukifanya makosa.

Katika lugha yenye madaha na wazi, Ellen White aliandika ukweli kuhusu Mungu – na kile alichoandika katika vitabu kama Njia Salama (*Steps to Christ*), Tumaini la vizazi vyote (*The Desire of Ages*) na Vielelezo vya maisha ya Kristo (*Christ's Object Lessons*) – anachora picha ya Mungu ambayo Waadventista wanaweza kushuhudia kwa shauku kwa wale ambao wamedang'anywa na uongo wa Shetani.

**3. Roho ya Unabii inaeleza wazi na kwa ukamilifu kisa cha pambano kuu.** Je, umegundua kwamba hakuna kanisa lingine linalofundisha au hata kuelewa kiini cha kisa cha Biblia – mada ya pambano kuu? Ni ujumbe wa pekee kwa Waadventista Wasabato, na ni upendeleo pekee tunaopaswa kuushuhudia kwa wale ambao bado hawajasikia au

kuelewa. Mada ya pambano kuu ni picha kubwa. Ni kisa kikuu cha kupambana baina ya wema na uovu. Ni mtazamo wa msitu mzima unao onyesha umuhimu wa nafasi ya kila mti ndani ya msitu.

Pambano kuu ni mada pekee inayoweza kujibu maswali makuu ya ajabu kuhusu maisha: Nilitoka wapi? Kwa nini niko hapa? Ninakwenda wapi? Kwa nini ulimwengu umejaa uovu ikiwa Mungu ni mwema? Kwa nini watu wasio na hatia wanateseka?

Mada ya pambano kuu haituambii tu jinsi uovu ulivyoanza inaonesha wazi jinsi utakavyokwisha. Inatupa ahadi kwamba dhambi na mauti vitatoweka milele muda si mrefu na kwamba tunaweza kuwa na tumaini la uzima wa milele mahali penye amani kamili na pasipokuwa na dhambi.

Hatimaye pambano kuu ndiyo mfumo pekee unao onyesha jinsi ambavyo kila ukweli wa Biblia unavyo husiana na mwingine. Je, ungependa kufahamu jinsi ukweli wa milenia unavyohusiana na Sabato? Mada ya pambano kuu, kila ukweli unachukua nafasi yake kama kipande cha chemsha bongo ya kuunga vipande.

Watu wanapenda visa, visa vinasaidia watu kuelewa mambo ya kudhania. Na hakuna kisa kikubwa, chenye maana, kilicho imara kuliko kisa cha pambano kuu

**4. Roho ya Unabii inawaongoza wasomaji wake kwenye neno la Mungu.** Biblia yenyewe inajiita Neno – lakini pia ni wazi kuwa Yesu mwenyewe ni Neno la Uzima. Na kama kulikuwa na sababu ya muhimu zaidi kuliko

yoyote ambayo ilimwezesha Mungu kutoa karama hii kuu kwa watu wake wa masalio, ilikuwa ni kuwaongoza katika yote mawili, Neno la Uzima na Neno lilioandikwa.

Maandishi ya Ellen White yanapumua upendo na tabia ya Yesu, Neno. Mzigo wake mkuu ulikuwa ni kuwaleta wasomaji katika kina, uhalisi ukuaji na uhusiano wa siku kwa siku na Yesu. Amemwinua Yesu katika maandishi yake yote. Na ukijua kwamba ufufuo wa Yesu pengine umeelezwa vizuri zaidi katika Biblia kuliko mahali pengine po pote, pia ameiinua Biblia na kuinua juu kwakusema, "Ndugu ninakipendekeza kitabu hiki kwenu!"

**5. Kupitia njia ya Roho ya Unabii Mungu hashuhudii tu namna ya kuwa na furaha na utakatifu, – bali namna ya kuwa na afya pia**. Moja ya karama kuu zaidi alizotoa Mungu kwa watu wake kupitia karama ya roho ya unabii ni kile ambacho Waadventista wanaita "Ujumbe wa afya."

Leo sayansi ya tiba na uchunguzi inaendelea kufikia uamuzi wa kudhibitisha yale aliyoyasema Ellen White kuhusu afya, maradhi na mwili wa mwanadamu miaka mia moja au zaidi iliyopita. Wakati madaktari walipokuwa wanawaandikia watu kuvuta sigara kama tiba kwa ajili ya mapafu, aliwaonya juu ya madhara makuu ya nikotini. Alidhibitisha miongo kadhaa kabla ya wakati wake kwa kutoa maonyo juu ya vyakula vya nyama, kula kupita kiasi na pombe. Na leo huduma za afya zitumiazo mvuke zenye gharama kuu zinatumia njia rahisi za asili za uponyaji – ambazo aliziandika miongo kadhaa iliyopita.

**6. Pia kwa kupitia karama ya roho ya unabii, Mungu**

**ametoa maagizo na matarajio kwa watu wake kwa wakati mwafaka.** Mapema katika huduma yake, kabla hata vita havijaanza, Ellen White alitoa maonyo ya mkasa wa vita vya wenyewe kwa wenyewe (civil war) ambavyo vingekuja. Pia alitabiri kuinuka kwa umizimu – ambayo imedhihirika sana katika kipindi chetu; Philosofia ya karne mpya (New Age); mafundisho ya kumfikiria Mungu kwa fikira ya imani ya mashariki, utabiri, kuwasiliana na wafu na mengine mengi. Leo mahusiano ya pekee ni utabiri wake kuhusu nafasi ya upapa na jinsi ilivyo na mahusiano na nchi ya Marekani katika utimilifu wa unabii wa Biblia.

Naam, kama Mungu kwa hakika anaweza kutoa karama hii kuu ya kinabii kwa watu wake wa masalio, unaweza kuwa na uhakika kwamba adui atalishambulia kundi la Mungu kwa ukali sana. Na amefanya hivyo. Kila shitaka linalowezekana, swali na dai amelitoa. Kila shaka na kidokezo kinachowezekana vimeinuliwa. Lakini kama vile Neno la Mungu lenye hadhi ya juu lilivyo stahimili mashambulizi ya karne kadhaa, vivyo hivyo karama ya unabii ya masalio ya Mungu itasimama imara.

### *Tumebarikiwa . . .na kuheshimiwa*

Zaidi ya maswali yote, Ellen White alikuwa ni mtu wa kawaida kama yeyote yule kati yetu. Katika uandishi wake, angaliweza hata kufanya makosa. Hata hivyo katika kazi yake yote, ukiangalia neno moja moja au sentensi moja moja, utaona kwamba ujumbe wake ni thabiti, wenye busara na wa kupatana na nuru kuu (Biblia). Baadhi ya

Waadventista wanaona aibu kuwa tuna nabii. Lakini je, Israel kama taifa walikuwa na aibu ya kuwa na hekalu na madhabahu, manabii wao wenyewe, ambao pia walikuwa watu wateule? Tunapaswa kujisikia kwamba tumebarikiwa na kuheshimiwa, na kwamba Mungu ametukabidhi karama hii ya ajabu kwetu sisi katika masalio yake ya mwisho.

Mungu hajatuacha tutafute njia yetu kwa kupitia njia za miamba sisi wenyewe – ametutumia nahodha kutufikisha bandarini.

Hii inamaana gani kwetu sisi? Je, inatuonyesha nini kumhusu yeye?

Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 13

# Sisi ni Nani?

Mapema baada ya masikitiko makuu ya mwaka 1844 – wale walioongoza katika kile kilichokuja kujulikana kama kanisa la Waadventista Wasabato wote waliweza kukutana pamoja sebuleni au katika chumba cha maongezi cha nyumba ya aina ya kipindi hicho.

Kufikia mwaka 1863 kanisa lilipoanza rasmi lilikuwa na washiriki wapatao 3500. Kufikia mwaka 2006, kulikuwa na washiriki wa kanisa kama milioni 15, na katika miaka ya karibuni linazidi kuwa na kiwango kikubwa cha ongezeko la washiriki wapya milioni moja kila mwaka.

Ukuaji huu wa pekee bila shaka ni sababu ya kweli ya kushangilia. Ni kipimo kimojawapo kinacho onyesha jinsi ambavyo kwa mafanikio watu wa Mungu "walioitwa kutoka nje" wamefanya jitihada za kuwaleta watu wengine kwa Yesu na ukweli wake wa siku za mwisho. Ingawa ni kweli pia kwamba kanisa la Waadventisa Wasabato ni dhehebu rasmi, hawajioni kama ni sawa na kanisa lolote. Badala yake Waadventista wanajiona wenyewe kama vuguvugu la dini lenye watu wanaoishi si kwa sababu tu Mungu alitabiri kwamba wataishi, bali kwamba wakati uliotabiriwa

ulipofika waliitwa kutoka nje ya machafuko ya Babeli ya makanisa mengine ili kuwakilisha ujumbe wa mwisho kwa ulimwengu.

Waadventista kama Waisraeli wa zamani, wameshawishika kuwa ni watu pekee walioteuliwa. Lakini wanafahamu kwamba kuwa wateule hakuna maana kwamba wao kwa namna fulani ni bora kuliko wengine. Kinyume chake wanatambua kwamba wateule wana ujumbe wa pekee na wa haraka wa kushuhudia kwa ulimwengu. Ni wapekee kwa sababu hakuna watu wengine duniani walio na mfumo kamili wa ukweli kama huo duniani. Ni ujumbe wa haraka kwa sababu wakati umekwisha na kuja kwa Yesu kumekaribia sana.

Ukuaji wa kanisa kwa miongo kadhaa sasa, ni sababu nzuri ya kushangilia na kufurahia. Hata hivyo pia, lazima tutambue pia kwamba ukuaji ambao hauna mipango maalum unaweza kuleta maafa. Kila daktari anaweza kukuambia kwamba saratani ni chembe zisizo na mpangilio, zenye machafuko zinazo zaana kwa kasi kubwa sana.

Hivyo katika historia ya kanisa letu, kuna vipindi ambavyo ilitubidi kama taasisi kujipanga na kufanya mabadiliko ya mara kwa mara kwa ajili ya ufanisi wa kazi. Na kabla kazi yetu haijamalizika hapa duniani na Yesu hajaja tena, tutaona mabadiliko zaidi kwa jinsi tutakavyojisimamia kama kanisa kwa ajili ya huduma.

Kwa hakika namna ambavyo tulivyojiendesha kama kanisa hapo awali, tukiwa washiriki wapatao 3500 tu, haiwezekani kabisa leo kuongoza washiriki milioni 15 bila

kuwa na mfumo (taasisi) wenye mpangilio.

Kwa kadri kanisa lilivyokua tulitambua kwamba ili tufanikiwe zaidi katika kuupeleka mbele ujumbe aliotupa Mungu, tunapaswa kuipanga kazi katika vikosi vidogo vya kijiografia. Mwanzo kabisa kulikuwa na General Conference – makao makuu ya kazi yetu. Baadhi ya majimbo na maeneo madogo pia yalikuwa na kanda za hapo hapo. Kwa kadri kanisa lilivyokua haraka haraka, lilitambua kwamba kungekuwa na ufanisi zaidi kuweka kanda kadhaa pamoja katika kanda ya union, hivyo katika mwaka 1901 kanda za union ziliundwa.

Leo tuna hatua au ngazi zifuatazo za utaratibu wa kanisa:

- Kanisa
- Konferensi au Field
- Union
- General Konferensi na divisheni zake

Divisheni za General Konferensi – ambazo zinaweza kuwa bara zima, sehemu za mabara au maeneo ya visiwani, zinaitwa "Divisheni" kwa sababu zinachukuliwa kama matawi ya General Konferensi katika maeneo yao ya ulimwenguni. Divisheni za General Konferensi, siyo ngazi za kujitegemea za kanisa kiuongozi, badala yake hizi ni divisheni za Genereral Konferensi zinazofanya kazi katika maeneo yao ya ulimwenguni. Kwa sasa tuna divisheni za namna hii kumi na tatu ulimwenguni:

- Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati
- Divisheni ya Ulaya na Afrika
- Divisheni ya Ulaya na Asia
- Divisheni ya Amerika ya Kati
- Divisheni ya Amerika ya Kaskazini
- Divisheni ya Kaskazini mwa Asia na Pasifiki
- Divisheni ya Amerika ya Kusini
- Divisheni ya Kusini mwa Pasifiki
- Divisheni ya Kusini mwa Asia na Pasifiki
- Divisheni ya Afrika ya Magharibi
- Divisheni ya Asia ya Kusini
- Divisheni ya Ulaya ya Kaskazini na Mashariki ya Kati
- Divisheni ya Kusini mwa Afrika na Bahari ya Hindi

Katika divisheni hizi kuna Union Konferensi na Union. Kwa mfano, Divisheni ya Amerika ya Kaskazini ina union Konferensi tisa – kila mojawapo ina majimbo kadhaa, sehemu ya majimbo au mikoa.

Kila ngazi ya kanisa letu iko kwa ajili ya kuhudumia taasisi katika eneo lake – kutoa raslimali, uongozi, mafundisho na motisha wa kiroho. Kila kundi – kila daraja la mfumo wa kanisa hupokea maelekezo yake kutoka kwa maamuzi ya uwakilishi au kanisa la ulimwenguni kwa pamoja – au washiriki katika eneo hilo la kijiografia. Ngazi mbalimbali za kanisa zinawajibika kwa kila mojawapo kwa ajili ya kukamilisha malengo yao bila kujali kama ni kanisa la hapo hapo, konferensi au union.

Kwa mfano, makanisa mbalimbali katika konferensi

fulani yanawajibika – na kuishi kwa ajili ya jimbo zima la konferensi. Kama ilivyo kwa wajumbe wawakilishi katika mikutano ya kawaida ya jimbo katika konferensi husika wanawajibisha uongozi na halmashauri kuu, kanisa moja moja katika konferensi husika yanapaswa kuwajibika kwa ajili ya mapenzi ya makanisa yote ya konferensi husika.

Kama Mwadventista bila shaka utakuwa unajua fika utaratibu wa kanisa letu, hivyo hakuna ulazima wa kuandika sura nzima ya kuorodhesha kila kanisa na konferensi duniani – au historia na majukumu ya kila ngazi ya kanisa katika eneo lake la ulimwenguni. Unaweza kupata habari hizo kwa urahisi katika kitabu cha kila mwaka cha Waadventista au katika ensaklopidia ya Waadventista Wasabato – ama toleo lililochapwa au katika toleo la mtandao wa kompyuta.

Hapa kuna jambo muhimu la kuzingatia kutoka kwenye majadiliano ya sasa – unaweza kujivuna kwamba kama lilivyo jeshi limejipanga kwa ajili ya kukamilisha ujumbe wake, ndivyo lilivyo kanisa lako! Uko kwenye kanisa linalofanya vizuri sana kwa ufanisi ili kutoa matokeo yaliyo bora zaidi. Katika jambo hili faida sio kubwa sana kwa wadau au mafanikio ya kijeshi. Matokeo tunayotafuta ni ya kuleta watu pamoja kwa kadri inavyowezekana katika dunia hii kwa ajili ya Yesu na Kweli – na ukweli wa siku za mwisho.

Kwa kadri unavyo hudhuria kwenye kanisa lako la nyumbani la Waadventista, unaweza pia kujua kwamba wewe ni sehemu ya kile ambacho kimekuwa ni vuguvugu

la ulimwengu – kwamba una kaka na dada mamilioni kuzunguka dunia yote wanoamini kama unavyoamini na kushuhudia njozi ya "Kazi iliyokwisha" na kurudi kwa Yesu!

Ingawa kanisa lilianzia Amerika ya Kaskazini, washiriki wake na viongozi wake tangu mwanzo walithamini njozi ya dunia kwa ajili ya kupeleka ujumbe wa Mungu wa mwisho kwa ulimwengu wote.

Katika mwaka 1874, J. N. Andrews aliondoka nchini kwake Marekani, akasafiri kwenda Switzerland kama mmishenari wa kwanza wa ng'ambo wa kanisa. Muda mfupi baada ya hapo wamishenari wa Kiadventista walikuwa wakiondoka kwenda kutumika katika mataifa na nchi nyingine kila mwaka – mwanzoni walikuwa wachache tu, bali baadaye kama kukimbia kwa maji ya kujaa na kupwa, – wanaume na wanawake walianza kuitangaza injili katika nchi nyingine.

Baadhi ya wamishenari wangine wa ng'ambo waliofuata nyayo za J. N. Andrews – wengi waliambatana na familia zao – ikiwa ni pamoja na wanaume na wanawake wafuatao:

| | |
|---|---|
| 1874: | C.M. Andrews; A. Vuilleumier kwenda Uswisi |
| 1875: | James Erzberger kwenda Ujerumani |
| 1875: | D. T. Bordeau kwenda Uswisi |
| 1876: | D. T. Bordeau kwenda Ufaransa |
| 1877: | J. G. Matteson kwenda Norway |
| 1877: | Bwana na Bibi William Ings kwenda Uswisi |
| 1878: | J. N. Loughborough kwenda Uingereza |
| 1878: | Maud Sisley kwenda Uingereza |

1879: Bwana na Bibi J. P. Jasperson kwenda Norway

Kuanzia mwaka 1880 idadi ya wamishonari ilikua ghafla, kiasi kwamba muda mfupi wamishenari chungu mzima walikuwa wanaondoka kwenda ng'ambo walikopangiwa kila mwaka.

Australia, visiwa vya Karebia, India, Trinidad, Amerika ya Kati na Kusini, Afrika ya Kusini, New Zealand, Visiwa vya Hawaii, Mexico na Polynesia – baada ya muda mfupi wamishenari wa Waadventista Wasabato walienea dunia yote.

Leo hakuna nchi au sehemu ya kijiji cha ndani – ambako kazi ya Mungu haijaelekea. Pengine hakuna kanisa lingine duniani ambalo ni la kiulimwengu kama la kwetu.
Ni kweli, bila shaka kwamba amri ya kusonga mbele ya uinjilisti – kuendelea mbele kwa kazi iliyomalizika – kwa sasa haiendi sawa kila mahali duniani. Kuna mlipuko ndio ukuaji huu wa kubatiza watu wengi katika mabwawa ya kuogelea – na makanisa mapya yanaanzishwa kwa kasi ya kushangaza.

Katika sehemu nyingine za ulimwenguni hali ya kutojali ya Loadikia bado inaendelea. Ukwasi, kufanya kazi kupita kiasi na mvuto wa burudani huchangia kuliwaza washiriki wa kanisa katika usingizi wa kutofanya kazi. Watu wanaweza tu kushuhudia uzoefu na ufahamu wao. Na kama upendo wao wa kwanza umepoa na hawawezi kukumbuka kwa nini ni Waadventista, hawana hamu au motisha ya kushuhudia jambo lo lote kwa wengine.

Lakini habari njema ni kwamba mwishoni mvua ya

masika ya Roho Mtakatifu itaenea katika kanisa zima la ulimwenguni, kuleta shauku mpya, nguvu na njozi – hamu mpya na yenye nguvu ya pekee kwa washiriki ili kuwaleta wengine kwa Yesu ambaye wamefanya naye upya uhusiano wa upendo nao.

Wakati huo utakapofika, ukuaji wa kanisa utakuwa kwa haraka sana ulimwenguni kote kote. Uinjilisti utakuwa wa kimataifa – na utaendelea mbele sio tu kwa mikutano ya hadharani bali hata kwa jeshi la walei lililopata moto moto. Upendo ni nguvu ya pekee ulimwenguni, na inapokuwa ndio chanzo cha msukumo wa nguvu kwa wafuasi wa kweli wa mwisho wa Mungu, ulimwengu mzima utakabiliwa na uchaguzi wa mwisho wa milele; kati ya kuwa watiifu Mungu au kumtumikia adui, kimsingi katika mfumo wa kujitumikia mwenyewe.

### *Kuufikia Ulimwengu Wote*

Unapotafakari kuufikia ulimwengu mzima na huduma ya kanisa lako, fikiria tena njia muhimu ambazo zinagusa maisha ya watu. Duniani kote, Waadventista wanashughulika, wako motomoto, wakiwahusisha Wakristo. Shughuli hizi ziko katika mifumo mbalimbali – mifumo mikuu kati ya hiyo ni kama ifuatavyo hapa chini.

UINJILISTI – Kwa njia ya mikutano ya hadharani (hasa katika siku za karibuni kwa kutumia setilaiti kufikia wasikilizaji wengi), mafundisho ya Biblia ya mtu kwa mtu, kugawa vijizuu, matangazo ya radio na televisheni, semina

za afya, na njia nyingine, tunawafikia jirani zetu na marafiki kwa kushuhudia injili ya Yesu Kristo.

ELIMU – Waadventista wanaendesha karibu shule 6,000 ulimwenguni – kutoka ngazi ya shule za msingi hadi vyuo na vyuo vikuu.

AFYA NA TIBA – Zaidi ya hospitali 500 za Kiadventista viwanda vya vyakula, zahanati na kliniki nazo zimeenea duniani kote.

MSAADA WAKATI WA NJAA NA MAAFA – Kwa kupitia jitihada za shiriki la Waadventista Wasabato la kutoa misaada wakati wa shirika na maafa (ADRA), kanisa letu lina uwezo wa kutoa msaada haraka zaidi wakati wa maafa mahali po pote duniani. Misaada ya chakula, nguo, na huduma ya madawa na tiba. Zaidi ya haya ADRA inafanya miradi ya kimaendeleo, na ile ya kusaidia katika njaa na ukame unaokumba maeneo mengi ya dunia.

HUDUMA ZA JAMII – Makanisa mengi yaWaadventista Wasabato huendesha vituo vya huduma za jamii, ambayo wafanyakazi wake ni washiriki wa kanisa wa kujitolea wanaowasaidia watu wenye shida na wasio na mahali katika jamii yao.

UCHAPAJI – Tunazo nyumba za uchapaji kama 60 duniani kote, Waadventista Wasabato wamejitoa kikamilifu

kushuhudia habari njema ya Mungu kwa ulimwengu kwa kupitia karatasi zilizochapwa.

MAWASILIANO –Waadventista walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza kuleta injili ya Yesu Kristo kwa njia zote mbili ya redio na televisheni. Leo wanarusha habari kwa kupitia "Sauti ya Unabii", gazeti la mtindo wa maisha, Pumzi ya Uzima na Imeandikwa. Vituo hivi vinawafikia mamilioni ya watu duniani kote.

> "Ni jambo la pekee kufahamu kwamba sisi ni kanisa linalokuwa – kanisa lenye utaratibu, familia ya dunia nzima. Lakini pia tunahitaji kuwa makini. Hata hivyo, kanisa la saba na la mwisho katika Ufunuo ni Loadikia.
> "Na kwa malaika wa kanisa lililoko Loadikia andika: haya ndio yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke kwenye kinywa changu. Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu, nawe hujui ya kuwa wewe ni mnyonge, na mwenye mashaka, na masikini na kipofu, na uchi. Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. Wote wanipendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu. Tazama, nasimama mlangoni nabisha, mtu

akisikia sauti yangu, na kufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye na yeye pamoja nami" – Ufunuo 3:14-20.

Tunapaswa kulinda nini? Uzoefu wa Roho ya Uvuguvugu. Hivyo inaweza kutokea wakati ambapo mwunganiko wetu binafsi na Yesu umeruhusiwa kunyong'onyea. Inaweza kutokea tukawa na shughuli nyingi sana kiasi kwamba tunasahau kuwekeza katika uhusiano wetu na Yesu.

Ni kitu gani kingine tunachohitajika kulinda? Kuona kwamba tunajitosheleza. Kushawishika kwamba tunafanya vizuri, wakati ambapo hatufanyi vizuri. Nahiyo inaweza kuwa kweli kwa namna zote mbili na mienendo yetu binafsi kama wakristo na namna tunavyofanya kazi kwa pamoja na kama kanisa. Makanisa pia yanaweza kujitegemea yenyewe, yakategemea program na mipango na utaratibu badala ya chanzo pekee cha nguvu – Roho Mtakatifu wa Mungu.

Bali ujumbe kwa Loadikia husema, tunaweza kutubu, tunaweza kutafuta dhahabu ya Mungu, mavazi meupe na dawa ya macho – Haki yake, upendo na Roho Mtakatifu. Na tunaweza kumwalika anavyosimama na kubisha hodi mlangoni.

Hebu fikiria unamwacha Yesu anasimama mlangoni bila kumkaribisha! Lakini tunaweza kuwa katika hatari ya namna hiyo – mtu binafsi na pia kama kanisa zima. Hivyo tunapofikiria juu ya maana ya kuwa sehemu ya masalio – tunapofikiria kwamba ina maana gani hasa kuwa Mwadventista –hebu tuwe makini na ubainishaji wa

maradhi ya Laodikia. Kwa sababu tu Laodikia!

Katika madarasa ya chuoni, wakufunzi wazuri wanatumaini kwamba katika kila mada ya somo, wanafunzi watapata angalau neno moja watakalo kumbuka maishani. Kitabu hiki pia kina ujumbe wa kuchukua nyumbani angalau wazo moja muhimu – wazo kuu la somo. Ujumbe wake ni huu. Wewe ni sehemu ya kitu fulani KIKUBWA – kitu fulani cha umuhimu wa kutikisa dunia, kitu fulani ambacho kikubwa chenye kipaumbele kuliko kitu cho chote unachoweza kusikiliza katika matangazo ya taarifa ya habari katika televisheni. Wewe ni kiungo – kiungo cha mwisho – ya cha mfululizo wa waaminifu wa Mungu tangu Edeni iliyopotea hadi Edeni itakayorejeshwa. Una sehemu muhimu ya kufanya. Mungu anakuhitaji – naam WEWE – kutafuta na kutumia karama za kiroho ulizopewa na Bwana – Anakuhitaji kuendeleza shauku kwa wale wasiomjua kama unavyomjua yeye. Anakuhitaji wewe uwe tayari kwa ajili yake kila siku ili kwamba aweze kuwafikia wengine kwa kupitia kwako. Mungu anakuhitaji uwe sauti yake, mikono yake, kuwepo kwake kwa wale waliopofushwa na uongo wa Shetani juu yake. Anakuhitaji wewe ili uwalete watu wengine katika pendo lake. Anakuhitaji wewe ili aishi ndani yako ili wengine waone tabia yake ya upendo wa karibu na binafsi kupitia kwako!

### *Utambulisho Wetu*

Tunapotembea katika safari ya maisha, kila mmoja wetu anapambana na swali la utambulisho wetu binafsi: “Mimi

ni nani?" Wakati mwingine tunachanganya utambulisho au kile ambacho wengine wanafikiri juu yetu. Lakini wewe ni wapekee. Mimi ni wapekee. Kila mmojawetu ni wapekee kabisa. Na ni muhimu kugundua jinsi tulivyo hasa, kando ya kazi zetu, kando ya wajibu tulio nao katika maisha, kando ya mawazo ya watu wengine.

Na kama wewe ni Mwadventista Msabato, pia unapambana na swali lingine kuu la utambulisho. Sio utambulisho binafsi, bali utambulisho wa kundi letu "Sisi ni nani?"

Mwadventista ni nani? Tupo hapa kwa ajili ya nini? Kwa nini tunaishi?

Ensaikolopidia (Kamusi) ya dini za Marekani inatoa taarifa kwamba kuna zaidi ya madhehubu au makundi mbalimbali 1588 ya imani katika nchi ya Marekani peke yake. Na ensaikolopidia ya dunia ya Kikristo inaonyesha dini mbalimbali 10,000 duniani kote. Dini mojawapo ya dini hizo; Ukristo, una madhehebu mbalimbali 33,830 ulimwenguni kote.

Hivyo sisi kama Waadventista ni moja tu ya maelfu ya makanisa na madhehebu duniani? Je, kuna jambo hasa la pekee kuhusu kanisa hili? Je, tu masalio, kimbilio ambalo Mungu anawaitia waliodanganywa na kupotea katika mafundisho ya uongo ya Babeli waje kupumzika? Je, sisi ni vuguvugu la kidini la mwisho lenye ujumbe muhimu kuhusu mwisho wa dunia?

Naam, ni kweli, sisi Waadventista wakati mwingine tunavutwa na mawazo mengine, hadi tunapoteza mwelekeo

wetu! Tunaishia kuacha njia kwa muda tunapoingia kwenye mabishano juu ya mafundisho au viwango vya kanisa au kama karama ya roho ya unabii bado inafaa. Ni dhahiri kwamba adui mkubwa hatuachi pekee yetu. Anashambulia ndoto za Waadventista, shule za Waadventista, taasisi za Waadventista na hata viongozi Waadventista.

Lakini rafiki zangu, hata kama Shetani anafanya uovu wake, Mungu tayari anafanya kila analoweza. Na bado tutaona nguvu kamili ya mvua ya masika iliyotabiriwa – umwagikaji wa nguvu wa Roho wa Mungu. Mvua ya masika italeta nguvu kwa watu wa Mungu – nguvu ya Pentekoste ambayo haijawahi kutoka kwa ajili ya ushuhudiaji.

Ufunuo 7 – inatuambia kwamba katika mwisho wa wakati, watu wa Mungu watapokea muhuri wa Mungu. "Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka mawio ya jua, mwenye muhuri wa Mungu aliye hai, akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari, akisema, Msiidhuru nchi au bahari, wala mti, hata nitakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao" – Ufunuo 7:2, 3.

Vipaji, akili ... mioyo: Wale waliopokea muhuri wa Mungu wametulia katika uaminifu wao kwake na ukweli wake kiasi kwamba hawawezi tena kuondolewa – kujitoa kwao kwa Mungu hakuwezi kugeuzwa tena. Wamefikia mahali katika ukristo wao ambapo ni heri wafe kuliko kuchagua njia ya ubinafsi tena.

Huku kutulia ni hatua imara na inachukua muda – kunapatikana kwa kipindi cha muda mrefu, pengine miaka

au hata miongo. Kwa wengine inawezekana isiwe ni kwa haraka, na kwa wengine ikawa muda mfupi zaidi. Hatua hii ya kutulia katika ukweli pengine inafana na kitu kama namna ambavyo zege la simenti inavyomwaga pole pole lakini kwa uhakika inavyotulia. Baadaye zege huwa ngumu na imara – na hiyo njia ya uimara haiwezi kugeuzwa tena.

Mara watu wa Mungu wanapokuwa wametulia katika ukweli – na katika uaminifu usioweza kugeuzwa toka kwa Mungu wao – halafu...hatimaye TENA.... Mungu anaweza kuwamwagia Roho Mtakatifu katika nguvu isiyo na kipimo kwa ajili ya kumaliza kazi mapema ambayo amewakabidhi wajumbe wake wa masalio.

### *Kuonyesha na Kuambia*

Wakati watu wa Mungu wanaposhuhudia imani yao – ni zaidi ya kuwa wahubiri. Kama vile kila mwalimu mzuri anavyo sisitiza juu ya somo kila siku, vivyo hivyo ndivyo tupasavyo kusisitiza ushuhuda wetu. Kushuhudia kunakoongozwa na Roho ni zaidi sana ya kushuhudia kwa maneno – ingawa inaweza kuwa ni pamoja na hayo. Kimsingi kumshuhudia kwa watu wa Mungu sio tu yale ambayo watu wanasikia wakisema – bali yale watu wanavyoona namna yao ya kuishi.

Hatimaye, watu wa Mungu wataonyesha katika maisha yao ni nguvu kiasi gani hasa Mungu ametumia kubadili mioyo ya wanadamu wanapotoa mwaliko usio wa masharti kufanya hivyo. Katika maisha yao, watu wa Mungu wataonyesha kwamba kama ambavyo Yesu angeweza

kumtii Baba yake kutegemea nguvu za kiungu, hivyo pia wafuasi wa Yesu leo wanaweza kumtii Mungu, kama Yesu kiongozi wao alivyo mtii Mungu.

Mungu anatamani kuliko kawaida kumaliza pambano kuu na maafa yote na masikitiko yanayo sababishwa nayo. Lakini madai ya uongo ya Shetani kwamba Mungu ametunga sheria ambayo haiwezi kutuzwa (udhuru wake kwa ajili ya uasi wake) lazima yakanushwe kabisa. Hivyo Mungu ataendelea kuwa mvumilivu kiasi cha kutosha kuruhusu muda wa kutosha – muda kwa ajili ya watu wake kwenye maisha yao wenyewe kutoa uamuzi juu ya madai haya ya uongo ili yafutiliwe mbali. Sisi tuliopo hapa duniani tunaweza tusiwe wavumilivu kwa ajili ya mwisho wa pambano. Kama ndivyo, kwa kuwa tayari kwa ajili ya Mungu kila siku, kwa kumkubali atatubadili mpaka tumetiwa muhuri kuwa watu wake daima – tunaweza kusaidia kuharakisha kurudi kwa Mwokozi na Bwana wetu.

Katika sehemu nyingine za ulimwengu, kazi ya kanisa tayari inaenda kasi sana kama moto kwenye msitu wenye nyasi kavu. Mtu fulani anaweza kukisia kwamba, huu ni mwanzo wa awali wa mvua ya masika iliyotabiriwa. Hata hivyo kuna sehemu nyingine za ulimwengu ambapo kazi inaenda taratibu sana ukilinganisha na sehemu nyingine.

Lakini mambo karibu yatabadilika. Ushuhuda wa kila matukio ya kutisha tunayo yaona ulimwenguni, yanapaswa kuwa ni ishara ya kutuamsha. Mazingira na hali ya hewa inazidi kubadilika na kuzorota kuelekea ubaya. Uhuru na usalama wa nchi navyo viko hatarini kila mahali. Ufisadi na

imani za kiShetani unaongezeka kwa hali ya juu duniani. Kabla habari moja ya kutisha kupotea kwenye mawazo ya watu, habari zingine mbaya zinasomwa kwenye ukurasa za magazeti siku hadi siku.

Bila shaka tungeshtuka na kukosa la kusema, kama tungejua hasa muda uliosalia ni mfupi kiasi gani.

Muda mfupi ujao makabiliano ya ana kwa ana baina ya wema na uovu yatatawala kila jambo. Na wafuasi wa mwisho wa Mungu masalio watakuwa katikati ya ulingo hayo yanapotokea. Jambo la mwisho katika maonyesho, Mungu atawaita akina Nuhu, Daudi na Luther.

Vipi rafiki yangu, unafikiri katika wakati huu tunaokaribia sana kufunga historia ya dunia, tunapaswa tuwe tunafanya nini?

Inawezekana jibu ni rahisi sana kama umekuwa kwenye mapenzi. Pengine unafahamu mapenzi ya mzazi, mtoto, kaka, dada au rafiki. Au pengine unajua mapenzi ya mahaba au mapenzi ya mtu na mke.

Kama umewahi kuwa na uzoefu wa upendo wa ndani sana, unajua kwamba unaweza kufanya lolote lile kwa mtu unayempenda. Na unajua vilevile kwamba, furaha moja ya mambo unayoyapenda sana ni kuwaambia wengine jinsi ambavyo mtu unayempenda alivyo wa pekee.

Tunapaswa tuwe tunafanya nini sasa? Tunapoendelea kusubiri tangazo la nguvu la pambano kuu, kitu gani kinapaswa kutawala?

Angalia tena maneno katika aya mbili za nyuma. Ikiwa unampenda Yesu Kristo, utafanya kitu chochote kwa ajili

yake. Hasa upo tayari kuyatenda yale unayojua anapenda uyatende. Anahitaji sana uwaonyeshe watu wengine namna alivyo ili nao waweze kumruhusu aishi maisha yake ndani yao. Wakati mwingine, anaweza kukuuliza ili ushuhudie unachofahamu kuhusu ukweli wake. Anaweza hata akakupa karama maalum kwa ajili ya kufundisha, kuhubiri au kushuhudia. Lakini anachotaka kutoka kwa kila Mwadventista Msabato – na anachokihitaji leo – ni kwa kila mmoja wetu kuwa mfereji wake wa upendo na baraka kwa watu wengine. Anatuhitaji kuakisi tabia yake kwa uwazi zaidi kiasi kwamba mtu hawezi kushindwa kufahamu. Anahitaji kwa umuhimu wa pekee sana watu watakao waeleza wengine jinsi yeye mwenyewe alivyo hasa! Kwa njia hiyo, atawavuta maadui zake watakapoona upendo wake umeonyeshwa katika kiwango cha karibu mno.

Tunapokuwa na upendo wa Yesu Kristo, pia tunakuwa hatuogopi haya hata kidogo juu ya kuwaambia wengine habari zake. Naam, ni kweli tuna ukweli mwingi wa kushuhudia kwa watu wanaotuzunguka. Bali ujumbe wetu wa kwanza ni kuwafanya wamfahamu na kumpenda. Mara watakapo mfahamu na kumpenda, kuwashawishi kuhusu ukweli wake wa siku za mwisho kutahitaji jitihada kidogo tu.

Waaminifu na watiifu wasio na idadi tangu wakati wa Adamu hadi wakati huu wa miaka 2009 walisimama imara kwa Mungu waliyempenda. Hawakuweza kuyumba kutoka kwenye kweli – wasingeweza kukubali makosa au kuyatumikia.

Siku moja, hivi karibuni, bila shaka mapema mno kuliko tunavyo jua sisi Waadventista Wasabato, tutakuwa na upendeleo wa kukutana "ng'ambo nyingine" na watiifu waliotutangulia. Tutawauliza watuambie ilikuwa na maana gani kwao kusimama bila kuyumba kwa Yule (Yesu) waliyempenda. Bila shaka nao watapenda kufahamu, ilikuwa na maana gani kwetu katika kizazi cha leo.

Je, kuna sababu yoyote nzuri ya kutaka tuendelee kubakia kwa muda mrefu katika sayari hii ya mateso? Unasemaje, kuhusu kwenda nyumbani? Unasemaje, tunajitoa kabisa kukamilisha utume ambao Mungu ametupatia?

> Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

SURA YA 14

# Wewe Ni Nani?

**Wewe ni Mwadventista Msabato.**

Labda ulizaliwa katika nyumba ya Kiadventista, ulisoma katika shule za Kiadventista, na umekuwa Mwadventista maisha yako yote. Labda ulifahamu kanisa la Waadventista ukubwani na ukaacha kanisa lako la awali na ukajiunga na kanisa la Waadventista Wasabato, kanisa jipya. Labda umekuwa Mwadventista kwa muda mfupi.

**Wewe ni Mwadventista Msabato.**

Sio Mkatoliki wa Kanisa la Waroma, sio Mbaptisti, sio Mpentekosti wala sio Mmethodist. Sio mshiriki wa imani ya kiyahudi, sio mshiriki wa kanisa la Assemblies of God, wala mshiriki wa Kanisa la Kristo la Mitume wa Siku ya Mwisho. Sio Mwislam, Mhindu au Mbudha, sio mshiriki wa wasiomwamini Mungu, au mshiriki wa watu wenye kutilia mashaka neno la Mungu (agnostic) au mshiriki wa deism.

**Wewe ni Mwadventista Msabato.**

Kwa namna hiyo, uko kwenye kanisa linalofanana na makanisa mengine, lakini kwanamna ya pekee, halifanani kabisa na makanisa mengine. Je, imani ya makanisa mengine yana uhusiano gani muhimu kuhusu mwaka 1844? Ni wapi tena unakosikia mtu ye yote akiongelea juu ya hekalu ya mbinguni na hukumu ya upelelezi – au pambano kuu? Ni

waumini wachache tu wanao amini juu ya Sabato ya siku ya Saba ya Bwana, roho ya unabii kati yao, au kwamba wafu hawajui neno lolote.

**Wewe ni Mwadventista Msabato.**

Ina maana gani kwako?

Unajisikiaje kuwa Mwadventista?

Kwa muda mrefu "Sesame Street" kipindi cha televisheni cha watoto, tabia ya Kermit ambaye ni Chura, anaimba wimbo wenye kichwa cha maneno yafuatayo: "Sio rahisi kuwa kijani." Wakati ambapo sio wewe pekee yako ambaye angalau ni mdogo. Kuwa "tofauti" kunaweza kuwa dhihaka na aibu ya kuto fanana na kundi kubwa. Inawezekana wakati mwingine kuwa Mwadventista imekuwa sio jambo rahisi kwako.

Kusali kabla ya kula hotelini, kuagizia chakula kisicho najisi, au kuto tumia vileo n.k, vinakufanya unakuwa tofauti. Pengine ni kujitetea shuleni au hata kazini ili kupata nafasi ya kutunza Sabato. Kujaribu kueleza umuhimu wa Ellen White na viwango vya kanisa lako kwa wengine, pasipo kunyamazishwa kuwa ni kikundi tu cha dini ambayo huleta taathira za kimawazo kwa waumini kutokana na shinikizo lake.

**Wewe ni Mwadventista Msabato.**

Na kama Mwadventista Msabato, unakila sababu ya kuwa na fahari (sio kujivuna au kuwa na kiburi) juu ya ufunuo wa pekee na muhimu ambao Mungu ametupa. Una kila sababu ya kushuhudia kwa wengine kila unachoamini bila kuona aibu.

Ina maana gani kuwa Mwadventista Msabato? Angalia majibu machache yaliyo orodheshwa kati ya majibu mengi yanayoweza kupatikana juu ya swali hilo:

1. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana kwamba wewe ni sehemu ya vuguvugu la kanisa la Mungu lililotabiriwa maelfu ya miaka iliyopita kwamba lingetokea kama lilivyotokea wakati ulipowadia. Inakupasa kuamini kila kinachoaminiwa na hilo kundi, na uzijue na alama za wazi ambazo kwazo kundi linaweza kutambuliwa. Ina maana kwamba wewe ni sehemu ya watu wa unabii –"masalio" ambao waliinuka mwishoni mwa miaka 2,300 na 1,260 ya unabii.
2. Kuwa Mwadventista Msabato kuna maana kwamba – haidhuru vile wanavyofikiria mawakala wa magazeti kuwa ni muhimu – wewe ni sehemu ya kile MUNGU anachofikiri kuwa ni muhimu hapa duniani katika siku hizi za leo. Wewe ni sehemu ya mfumo wake wa kutoa ujumbe, ujumbe wa Mungu wa mwisho na muhimu sana ambao haujawahi kutolewa katika sayari hii. Wewe ni sauti yake – na maisha yako ni kielelezo – kwa wale wanaokuzunguka, – kwamba upendo na kweli wa Mungu vinabadilisha na yakwamba kurudi kwa Yesu kumekaribia.
3. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana kwamba unatambua kwamba Mungu analipenda kanisa hili kiasi cha kulipa kila kitu, ikiwa ni pamoja na karama ya kiroho na karama ya unabii – karama ambayo imefaulu viwango vyote vya Biblia vilivyotolewa kwa ajili ya

kutofautisha karama halisi na karama ya ugushi.

4. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana kwamba wewe ni sehemu ya vuguvugu la kanisa lililojitoa kurejesha kweli kamili ya Mungu katika dunia hii. Ukweli uliyogunduliwa katika enzi ya Matengenezo. Upekee wa ukweli huu hasa katika siku hizi za mwisho utawasaidia watu kwa ajili ya kujitayarisha kwa kurudi kwa Yesu Kristo.
5. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana kwamba una faida ya ajabu ya kujua namna ya kuwa na afya bora na furaha, maana ya kuwa mtakatifu; kuwa mtakatifu kama Mungu anavyokuhitaji uwe.
6. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana kwamba una mtazamo mpya wa kuangalia sheria ya Mungu –Amri Zake. Huzioni kama katazo la kukunyima furaha na kukutumbukiza kwenye hali mbaya sana ya kukunyima kila kitu chema – bali ni uongozi wa Mungu mwenye upendo wa juu unao kuondolea maumivu, hasara na hatimaye kifo. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana ya kuwa huru kufanya yale ambayo Biblia inasema ufanye, sio kwa sababu una lazimika ila kwa sababu umegundua raha ya kufuata njia ya Mungu kwa sababu unahitaji kufanya hivyo.
7. Kuwa Mwadventista Msabato ni kujifunza kwa uzoefu maana ya haki kwa imani. Mtazamo wako wa wokovu unakuzuia neema rahisi (cheap grace) kwa namna moja na kwa namna nyingine kuokolewa kwa ajili ya kutunza amri za Mungu (legalism). Ina zuia jambo lolote lisilo

sawa kati ya kile Mungu alichokwishafanya kwa ajili yako na kile anachohitaji kufanya ndani yako.

8. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana kuwa tofauti na makundi mengine yasiyo fahamu wito wao, kwa kujua makusudi maalum ya kanisa lako. Unajua kwamba lina ujumbe wa pekee katika historia ya ulimwengu – kazi muhimu sana ya kuelekeza sayari hii juu ya ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo unaoambatana na ujumbe wa upendo wa Mungu katika vitabu vya injili vya Agano Jipya.
9. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana kwamba wewe siyo sehemu ya kanisa linalokufa maji au kuelea kwa kutapatapa majini. Wewe ni sehemu ya vuguvugu la kidini lenye nguvu, linalokuwa haraka sana kiasi cha kuwashangaza watu wanaosomea ukuaji wa makanisa.
10. Kuwa Mwadventista Msabato maana yake ni kwamba wewe siyo mshiriki wa kanisa dogo, au kikundi fulani kidogo, cha dini ambayo huleta taathira za kimawazo kwa waumini kutokana na shinikizo lake. Wewe sio chipukizi (offshoot). Wewe ni sehemu ya vuguvugu la kanisa la Ulimwengu wote linalojulikana sio tu kwa ajili ya ukuaji wake, bali kwa huduma yake za tiba, elimu, na huduma ya kijamii.
11. Kuwa Mwadvenstista Msabato maana yake ni kwamba kanisa lako lina mambo ya kipaumbele yaliyo wazi. Halitangitangi – na kamwe halitatangatanga – katika mambo ya nadharia za kisiasa na karne mpya (New Age) pamoja na Saikolojia ya kujisaidia mwenyewe. Kanisa

lako halioni ujumbe wake kama kundi la kuhalalisha uadilifu bali linamwinua juu yeye anayeweza kutuumbia mioyo ya uadilifu. Kanisa lako halijibadilishi bidhaa yake kutegemea upepo wa kibiashara – lina bidhaa moja tu; Yesu na Ukweli wake.

12. Kuwa Mwadventista Msabato ina maana ya kuelewa jinsi kanisa lako – na jinsi wewe – unavyoingia kwenye picha kubwa ya enzi ya pambano kuu baina ya wema na uovu, baina ya Kristo na Shetani. Wewe ni sehemu ya waaminifu wa mwisho, viungo vya mwisho vya mfululizo wa wafuasi halisi wa Mungu usiokatika katika historia. Umeunganishwa kwa waaminifu wote wa zamani; Wazee wa zamani na manabii wateule wa Israel, mitume na waumini wa kanisa la kwanza la Wakristo, walioteseka katika karne ya kwanza, watiifu katika Zama za Giza, Wanamatengenezo imara katika kipindi cha matengenezo, wanafunzi Shujaa wa Biblia wa vuguvugu la kidini la kuja kwa Yesu mara ya pili, waasisi wa kanisa lako mwenyewe. Husimami peke yako. Unasimama kwenye kweli, kifahari, bila kushtuka kwa ajili ya Mungu wako, aliyemtoa mwana wake kwa ajili yako. Unasimama kama sehemu ya watu wa Mungu wa mwisho, watu wanaofahamu umuhimu wa muda mfupi uliobaki –wakati watu wengi bado hawajatambulishwa kwa Mwakozi wao na ukweli wake.

Wewe ni mmojawapo wa wajumbe wake wa masalio wanaofahamu namna ya kutoka katika sayari hii wakiwa hai

na wakiwa wamebeba ujumbe na bahati ya kushuhudia kwa watu wengine.

**Wewe ni Mwadventista Msabato.**

Wewe ni mmojawapo wa wateule wa Mungu.

Je, unaaibika? Unatishwa? Uko tayari kuficha umaalum na upekee wa nuru yako chini ya pishi? Tafakari kwamba dunia INAHITAJI SANA kile ulicho nacho. Watu wengi sana wahitaji kupata ulichopata. Wewe sio mtu wa ajabu ajabu, tofauti na wenzako! Wewe una mkate ambao waabuduo wenzako katika sayari hii wanauhitaji sana. Wewe sio mgeni. Wewe ndiye mwenye ramani ya mahali palipo na dhahabu.

Au unaogopa? woga – Je, waogopa kwamba hatimaye unaweza kuteswa hasa unapoangalia nyuma katika historia ya waaminifu wa kwanza wa Mungu? Je, unaogopa kwamba itakulazimu kupita wakati mgumu wa mateso? Vyema, kando ya ahadi kutoka kwenye Biblia kwamba hutakosa chakula na maji – na kando ya ahadi za pekee za Zaburi 91 – kumbuka kitu kingine zaidi. Mungu anajua nani ataweza kuvumilia, sio mateso tu bali hata kufa kwa ajili ya imani. Hatakuita kwa ajili ya hayo isipokuwa amekupa yote aliyowapa walioteseka katika zama zilizopita. Hivyo shikilia ahadi zake bila kuogopa. Hapendi yeyote kati yetu aishi kwa woga na hofu.

Badala yake zingatia katika furaha inayotarajiwa tunapokaribia mwisho wa maisha ya mateso. Sherehekea kwa ajili ya kukaribia kwa mwisho wa maumivu, machozi na kifo, na hatimaye kuihama dunia na kwenda kwenye usalama kamili, furaha na ukamilifu wa milele na kila

shauku yako ya kuishi bila dhambi.

Wewe ni Mwadventista Msabato.

Wewe ni mmoja wa waaminifu wa mwisho.

Wewe ni sehemu ya mfululizo wa waaminifu usiokatika. Una bahati sana - unabarikiwa sana.

Katika kila kizazi, Mungu DAIMA amekuwa na watu wake waaminifu na wanyenyekevu, walioitwa na wateule, na bado ana watu pekee leo.

# TOKA HAPO KALE ...
# HADI SASA

*Picha chache toka kwenye*
*Album ya familia ya Kiadventista*



William Miller (kushoto) alisaidia kuzindua Vuguvugu kuu la kurudi kwa Yesu katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa.

Kanisa dogo (kulia) la William Miller.





Nyumba ya William Miller (kushoto) katika shamba lake huko Low Hamption –New York.





Ellen G. White (juu kushoto – akiwa na mume wake James juu kulia) pamoja na nahodha Joseph Bates (chini kushoto) walikuwa waasisi wa Kanisa la Waadventista Wasabato. Mtoto wa kiume wa Mama White, William C. (Willie) White (chini kulia), alikuwa ni msaidizi aliyejitoa sana kwa mama yake miaka yote ya huduma ya mamaye.











Elmshaven (juu) ilikuwa ni nyumba ya Ellen G. White Kaskazini mwa California katika miaka yake ya baadaye.

Mwishoni mwa miaka 1800, John Kellogg, M. D., tabibu wa Mwadventista, aliongoza katika uanzilishi wa hospitali ya kulaza wagonjwa huko Battle Creek – jimbo la Michigan. Katikati kushoto hospitali ya wagonjwa wa muda mrefu ilivyokuwa ikionekana kabla ya kuteketezwa kwa moto mwaka 1902. Chini kushoto: Hospitali ya wagonjwa wa muda mrefu, ikiwa imejengwa upya tena kwa ukamilifu katika mwaka 1929.



Katika mwaka 1905, Ellen G. White, kwa msaada wa mchungaji John Burden, aliongoza ununuaji wa sehemu ya kituo cha afya cha awali chini ya kilima huko Loma Linda kusini mwa Califonia (angalia picha ya juu). Kutoka katika mwanzo huo mdogo, Loma Linda ilikuwa katika ulimwengu –ikimiliki chuo kikuu na kitivo cha afya (angalia Kituo Kikuu cha Afya/Majengo ya Kitivo cha Afya katika mwaka 2005 picha ya chini.)






Mwanzoni kabisa mwa miaka ya karne ya ishirini, kliniki ndogo ilianzishwa katika mtaa wa Boyle kusini ya kati ya Los Angeles, California. Ushuhuda wa kiafya ulioanza pale umekua katika kutandaa kwa Kumbukumbu ya Kituo cha Afya cha White (chini), imeitwa kwa ajili ya mwasisi mmojawapo wa kanisa la Waadventista Wasabato Ellen G. White.



Kanisa la Waadventista Wasabato linamiliki karibu nyumba za uchapaji 60 kote ulimwenguni. Mbili kati ya hizi, zina hudumia Amerika ya kaskazini ni; Review and Herald Publishing Association Hagerstown, Maryland (kulia) –na Pacific Press Publishing karibu na Boise, Idaho (chini).







Majengo ya Makao Makuu ya Kanisa la Waadventista Ulimwenguni (juu –General Conference) – na kibao cha majengo Makao Makuu ya Kanisa la Waadventista Ulimwenguni. Picha hatimiliki ya 2005, mali ya Makao Makuu ya Waadventista Wasabato Ulimwenguni.

